

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Saba – Tarehe 9 Februari, 2022

(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)

D U A

Spika (Mhe Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa, tukae.

Katibu!

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

MHE. NEEMA W. MGAYA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2021.

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2021.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea.

Katibu.

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali, tutaanza na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Temeke, sasa aulize swali lake.

Na. 67

Uhaba wa Walimu na Vifaa vya Maabara – Temeke

MHE. DOROTHY G. KILAVE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaajiri Walimu wa Sayansi katika Shule za Sekondari za Kata Wilaya ya Temeke pamoja na kumaliza tatizo la uhaba wa Vifaa vya Maabara kwenye shule hizo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Temeke, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 iliajiri Walimu 6,949 ambapo kati yao asilimia 79 walikuwa Walimu wa sayansi ambao walipangisha vituo katika Shule za Sekondari za Serikali, kipaumbele kikiwa ni shule zenye upungufu mkubwa kulingana na mahitaji ya

wakati huo. Serikali imefanya tathmini ya mahitaji ya Walimu wa sayansi katika shule za sekondari na kubaini kuwa Manispaa ya Temeke ina upungufu wa Walimu wa Sayansi 631, sawa na asilimia 71.05 ya mahitaji. Serikali itaendelea kuajiri Walimu wa fani zote na kuwapangia vituo kulingana na mahitaji ya shule za sekondari zote nchini, zikiwemo Shule za Sekondari za Manispaa ya Temeke.

(b) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali ilinunua na kusambaza vifaa vya maabara katika Shule za Sekondari za Kata zipatazo 1,258 nchini zikiwemo shule 14 Manispaa ya Temeke ili kuwafanya wanafunzi waweze kujifunza kwa vitendo masomo ya Sayansi. Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo ya Elimu nchini itaendelea kununua na kusambaza shulenii vifaa vya maabara katika shule za sekondari nchini, zikiwemo Shule za Sekondari za Manispaa ya Temeke. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

MHE. DOROTHY G. KILAVE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini naomba niongeze maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Serikali imefanya jithhada kuweza kuleta Walimu, lakini utaona kwamba, asilimia 71 ni kubwa sana kwa jimbo letu la Temeke au Wilaya nzima ya Temeke. Sasa je, Serikali haioni kwamba, inaweza kufanya jithhada za ziada ili kuweza kupata vibali kwa halmashauri zetu kuweza kuajiri Walimu kwa mikataba, hao wa sayansi ili tuone kwamba, elimu sasa inaendelea mpaka hapo Wizara itakapokuwa imepata namna ya kuweza kuajiri?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kuhusiana na vifaa katika sekondari zetu, je, bado haionekani ya kwamba, tunaweza tukapata vibali hivyo tukaweza kununua vifaa hivi kwa ajili ya maabara zetu, badala ya kusubiria wadau na sisi tuna fedha katika manispaa zetu? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Serikali imeendelea kufanya jitihada za makusudi, ili kupunguza pengo la upungufu wa Walimu wa sayansi katika shule zetu za sekondari, lakini mikataba ya ajira kwa watumishi wa umma; tayari Serikali ilishaandaa *modal* ya mikataba kwa halmashauri zetu kuajiri watumishi kwa mkataba kwa kutumia mapato ya ndani ya halmashauri.

Kwa hiyo, kibali kilishatolewa na watumishi wote wa sekta ya afya, sekta ya elimu na wengine ambaeo halmashauri kwa uwezo wa mapato ya ndani wana uwezo wa kuwalipa mishahara kwa mikataba, kibali kilishatolewa na tunatia shime kwamba, waendelee kutumia fedha za mapato ya ndani kuajiri watumishi kwa ajili ya kupunguza pengo la upungufu wa watumishi hao.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na vifaa vya sayansi kwa shule za sekondari, nalo linafanana na jibu langu la kwanza kwamba, mapato ya ndani ni sehemu ya fedha za Serikali kwa hiyo, kazi yake ni pamoja na kutatua changamoto zikiwemo za upungufu wa vifaa vya sayansi katika shule zetu. Kwa hiyo, lazima halmashauri zitenge fedha hizo ili kupunguza mapengo ya vifaa hivyo. Nakushukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Chaurembo, swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ina upungufu wa Walimu 6,300. Je, Serikali haioni haja ya kuleta Walimu wapya kujaza nafasi zote za Walimu waliofariki na kustaafu wa Manispaa ya Temeke?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chaurembo Abdallah, Mbunge wa Mbagala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, watumishi wetu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na maeneo mengine ya Serikali, wale ambao kwa sababu moja ama nyiningine wanastaafu ama kufariki dunia, utaratibu wa kujaza nafasi zao unaifuata utaratibu wa ajira za kawaida, lakini kwa kuzingatia uhitaji katika halmashauri husika.

Kwa hiyo, wale watumishi ambao katika Halmashauri ya Temeke wamestaafu, wanafahamika idadi yao, lakini waliofariki idadi yao inafahamika na wakati wa vibali vyaa jira moja ya maeneo ambayo yanawekewa kipaumbele ni kujaza nafasi hizo. Nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Pauline Nahato, swali la nyongeza.

MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO: Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali ambalo linaendana na hilli la tatizo la shule ya sayansi kwa Wilaya ya Temeke; kwamba, tatizo la wasichana kusoma sayansi bado ni changamoto.

Je, Serikali ina mawazo gani kujenga mabweni kwa hawa wasichana ambao wanasoma sayansi katika shule za sekondari nchini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, unao uhuru wa kujibu swali hilo, lakini kama huna majibu linaweza kuja kama swali la msingi. Uchaguzi ni wako, kama unataka lije kama swali la msingi, niambie, mimi nitamwambia alete swali la msingi. Washa kisemeo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, nashauri lije kama swali la msingi.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato utapeleka swalii la msingi kwenye hoja hiyo muhimu kabisa ya kujenga mabweni kwa ajili ya watoto wa kike kwenye shule za sekondari.

Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Mbunge wa Muhambo, sasa aulize swalii lake.

Na. 68

Ujenzi wa Soko – Muhambo

MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa soko la ujirani mwema katika Kijiji cha Mukarazi ikiwemo miundombinu na ujenzi wa Kituo cha Forodha cha Pamoja katika Jimbo la Muhambo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Folrence George Samizi, Mbunge wa Jimbo la Muhambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Soko la Mukarazi ulianza kutekelezwa Juni, 2018 na kukamilika Oktoba, 2020. Ujenzi wa Soko hilo umegharimu kiasi cha shilingi milioni 442.61 na kwa sasa soko limekamilika kwa asilimia 100 na linatumika mara mbili kwa wiki.

Mheshimiwa Spika, ili kufanya soko hilo kutumika kikamilifu Halmashauri imetoea kiasi cha Shilingi milioni 5.6 kwa ajili ya kupima viwanja 145 katika eneo la soko kwa ajili ya

matumizi mbalimbali ikiwemo biashara, huduma za polisi na forodha. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, swali la nyongeza.

MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa jinsi ambavyo inaendelea kupambana kuwasaidia wananchi ili waweze kujikwamua kiuchumi:-

Mheshimiwa Spika, soko hili la ujirani mwema ni soko kati ya nchi ya Tanzania na Burundi. Kama nilivyouliza kwenye swali langu la msingi, mahali pale Serikali imeweka pesa kujenga yale mabanda kwa ajili ya biashara, lakini hakuna kituo cha polisi, hakuna *TRA*, wala hakuna uhamiaji, hivyo, kufanya utendaji wa soko lile kuwa hafifu kwa sababu ya hatarishi hii.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa mpaka uko kilometa tano ndani ya nchi ya Tanzania kwa hiyo, hata pale ambapo uhamiaji wanafanya shughuli zao za kawaida inasababisha usumbufu sana kwa wananchi. Hivyo, napenda kujua ni lini Serikali itaweka vile vipaumbele vyta *One Stop Centre* kama nilivyouliza kwenye swali langu la msingi, ikiwamo forodha? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, Mbunge wa Muhammwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Florence kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwasemea wananchi wa Muhammwe, lakini nimhakikishie

kwamba, hoja hizi zote ambazo amezileta Serikali imeanza kufanya kazi, likiwemo suala hili la kupima maeneo ya viwanja 145 kuzunguka soko, ili tuweze kupata maeneo kwa ajili ya kujenga Vituo vya Polisi, Forodha, lakini pia nae neo la Uhamiaji. Kwa hiyo, mara baada ya ramani zile kukamilishwa ambazo tayari mchakato unatarajiwa kuanza wakati wowote, sasa tutaenda kuomba kwenye sekta husika waweze kujenga vituo hivi na kuwezesha soko kufanya kazi vizuri. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, Mji wa Bukoba uko katika mkoa unaopakana na nchi jirani zaidi ya tatu. Je, ni lini Serikali itajenga soko kuu Bukoba Mjini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oliver Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mji wa Bukoba ni miongoni mwa miji ambayo iko kwenye mpango mkakati ambao utakwenda kujenga masoko, barabara, vituo vya mabasi vya kisasa. Nimpongeze sana Mheshimiwa Oliver Semuguruka, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Stephen Byabato, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Mjini, amekuwa mfuatiliaji wa mara kwa mara na Serikali iko kwenye hatua za mwisho za kuanza utekelezaji wa mradi huo. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba, soko hilo, lakini pamoja na maeneo hayo mengine yatafayiwa kazi baada ya mradi huo kuanza. Nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe, sasa aulize swali lake.

Na. 69

Kutoa Pori la Kanegere kwa Wananchi – Mbogwe

MHE. NICODEMUS H. MAGANGA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia Wananchi Pori la Kanegere kwa matumizi ya Wafugaji kwa kuwa Pori hilo limepoteza sifa ya kuwa Hifadhi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Henry Maganga, Nicodemus, Mbunge wa Jimbo la Mbogwe, kama ifatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Pori la Kanegere lina ukubwa wa hekta 725.24 na lipo kwenye Kijiji cha Kanegere ambacho kina eneo lenye ukubwa wa hekta 4,443.35. Kijiji hicho tayari kimeandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Kijiji Na.5 ya mwaka 1999 na Sheria ya Matumizi Ardhi Na.6 ya Mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, Pori la Kanegere linamiliikiwa na kijiji na sehemu kubwa ya pori hilo ipo katika safu ya milima. Eneo hilo halifai kwa ajili ya shughuli za ufugaji kwani ni eneo lenye miinuko mikubwa ya milima.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mpango wa Matumizi ya Ardhi ulioandaliwa, wananchi wamelitenga eneo hilo kwa ajili ya kuhifadhi na kupunguza mmonyoko wa udongo unaoathiri mazingira ya kijiji kwa ujumla wake. Aidha, kwa

upande wa wafugaji mpango huo umetenga eneo la malisho lenye ukubwa wa hekta 405.02 ambalo inashauriwa wafugaji kulitumia kwa ajili ya mifugo yao.

Mheshimiwa Spika, hivyo, natoa wito kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe kushirikiana na Mamalaka husika ili kukamilisha taratibu za pori hilo kutangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali kwa manufaa mapana ya Kijiji, Halmashauri na nchi kwa ujumla. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Henry Maganga Nicodemus, swali la nyongeza.

MHE. NICODEMUS H. MAGANGA: Mheshimiwa Spika, Ahsante. Nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini namwomba Waziri apate muda twende tukafanye ziara kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe. Mbogwe ni mji ambao umezingirwa na mapori mengi, hivyo wananchi wa pale wanapata tabu sana jinsi ya kuishi na mapori katikati japokuwa mapori yale hayana sifa ya kuwa na hifadhi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri siku moja twende tuongozane naye ili kusudi twende tukashauriane vizuri ili wananchi wale waweze kuishi katika hifadhi zile. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ombi hilo la kuongozana na Mheshimiwa Mbunge au kwenda kufanya ziara kwenye jimbo lake.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, nimepokea ombi hilo na baada ya kikao hiki tutapanga baada ya Bunge tuweke ratiba ya kwenda Mbogwe. Nashukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Matatizo yaliyoko kwenye Pori la Mbogwe

ni sawa kabisa na matatizo yaliyoko kwenye Jimbo la Geita Vijijini, Hifadhi ya Rwande, ambayo kimsingi ilishapoteza sifa ya hifadhi.

Sasa ombi langu Mheshimiwa Waziri, atakuwa tayari baada ya vikao hivi kutembelea Jimbo la Geita Vijijini ili aweze kuja kuona lile pori badaye tuwe na utaratibu wa kuwarudishia wananchi waweze kuendelea kulima?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mbunge wa Geita Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, niko tayari kuambatana na Mheshimiwa Musukuma kwenda jimboni kwake na kutembelea pori hilo ili pamoja na Wizara ya Ardhi na wadau wengine tukubaliane namna ya kuli-manage ili wananchi waweze kupata fursa nzuri. Nashukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana. Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira; Mheshimiwa Juliana Didas Masaburi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 70

Kudhibiti Uchafuzi Unaofanyika Pembezoni mwa Ziwa Victoria

MHE. JULIANA D. MASABURI aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje katika kudhibiti uchafuzi unaofanyika pembezoni mwa Ziwa Victoria ambao unapunguza samaki kuzaliana?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MUUNGANO NA MAZINGIRA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Juliana Didas Masaburi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uchafuzi wa mazingira unaofanyika pembeni mwa Ziwa Victoria unatokana na shughuli za kibinadamu zisizozingatia hifadhi ya mazingira. Shughuli hizo ni pamoja na utiririshaji wa majitaka kutoka katika maeneo ya makazi, utupaji taka ngumu kutoka majumbani na viwandani, kilimo kisicho endelevu kinachosababisha uchafuzi wa maji kutokana na kuongezeka kwa tabaki, matumizi yasiyo sahihi ya viuutilifu na mbolea za viwandani na uchimbaji wa madini usio endelevu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuandaa Kanuni, miongozo na mikakati ya kudhibiti uchafuzi wa mazingira katika maeneo ya maziwa. Aidha, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa tathmini ya athari za kimazingira (TAM) inafanyika kwa miradi ya maendeleo iliyopo inayotarajija kufanyika pembezoni mwa Ziwa Victoria ili kuhakikisha udhibiti wa vyanzo vya uchafuzi wa maji ya Ziwa Victoria inayotokana na shughuli za kibinadamu zisizohusisha miradi hiyo unazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa tathmini ya athari za kimazingira (TAM) inafanyika kwa miradi ya maendeleo iliyopo, inayotarajija kufanyika pembezoni mwa Ziwa Victoria ili kuhakikisha udhibiti wa vyanzo vya uchafuzi wa maji ya Ziwa Victoria inayotokana na shughuli za kibinadamu zisizohusisha miradi hiyo, inazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile Serikali imepiga marufuku matumizi ya mifuko ya *plastic* kwa ajili ya kubebbea bidhaa ambayo kwa kiasi kikubwa ilikuwa ikichangia uchafuzi pembeni mwa Ziwa Victoria.

SPIKA: Mheshimiwa Juliana Masaburi, swali la nyongeza.

MHE. JULIANA D. MASABURI: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina swali moja la nyongeza. Inasemekana samaki na dagaa za Ziwa Victoria zina madini ya zebaki:-

Je, Serikali imefanya tafiti juu ya hili? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kumpongeza sana dada yangu Mheshimiwa Juliana, kwa kweli yeye ni mwanamazingira mzuri sana. Katika upande huo kuhusu samaki na dagaa wanaopatikana katika Ziwa Victoria kwamba inasemekana wana madini ya zebaki, jambo hilo tuseme kwamba si sawasawa kwa sasa hivi, kwa sababu tunafahamu kwamba tuna-*export* samaki wengi nje ya nchi na samaki hao wamekuwa wakinufaisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wataalamu wetu hivi sasa wanaendelea kufanya kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba katika suala la kanda ya ziwa matumizi mbalimbali ya kemikali yanadhibitiwa, lakini hata hivyo mpaka hivi sasa tafiti mbalimbali zimefanyika na hazijaonyesha kwamba samaki hawa wanaathirika.

Kwa hiyo, kikubwa zaidi tuwaombe wananchi katika maeneo mbalimbali kuendelea kuzingatia masuala mahususi ya kimazingira kwa lengo kubwa la kuendelea kulinda Taifa letu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Waheshimiwa mnagonga meza mpaka sielewi nani achaguliwe na nani asichaguliwe. Mheshimiwa Asya swali la nyongeza.

MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Changamoto hizi za uchafuzi wa kimazingira ambazo zinatokea katika maziwa mbalimbali vile vile hutokea katika fukwe za bahari yetu. Nataka kujua:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti uchafuzi huu wa kimazingira kwenye fukwe ukizingatia fukwe hizi tunazihitaji zaidi katika vivutio vyetu nya utalii?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la dada yangu Mheshimiwa Asya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza kama Serikali tumeweza kutoa miongozo na hasa kuona jinsi gani tunafanya uratibu wa kufanya *recycling process* wa taka zote zinazoingizwa baharini. Hata hivyo, mnakumbuka hivi karibuni tuliweza kutoa baada ya kuona pale kuna changamoto kubwa licha ya kuzuia mifuko ya *plastic*, lakini imeonekana kwamba katika *recycles* vile vifuniko nya chupa havirejesheki na hivyo mara nydingi sana vimekuwa vikisababisha changamoto kubwa hasa katika samaki baharini.

Mheshimiwa Spika, hivyo, ndiyo maana tumetoa miongozo mbalimbali ya kuhakikisha tunalinda mazingira. Kubwa zaidi tumesilitiza ajenda ya usafi katika maeneo ya miji yote inayozunguka ufukwe wa bahari. Tulitoa maelekezo tulipokuwa pale Kinondoni kwamba maeneo yote yanayozunguka ufukwe wa bahari, Maafisa Mazingira katika maeneo hayo kuhakikisha kwamba ajenda ya usafi kwa wakazi wote inaendelea kwa lengo la kuhakikisha kwamba tunakuwa na mazingira rafiki kwa ajili ya utalii. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan Mbunge wa Chakechake sasa aulize swalii lake.

Na. 71

Faida za Mifuko ya Kuwaendeleza Vijana, Wanawake na Wajasiriamali – Zanzibar

MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN aliuliza:

Je, Programu za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (*YDF*), Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (*WDF*), Mfuko wa Taifa wa kuendeleza Wajasiriamali (*NEDF*) na Mfuko wa kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali wadogo (*SMF*) zimewasaidiaje Vijana, Wanawake na Wajasiriamali wa upande wa Zanzibar katika kujikwamua kiuchumi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, Mbunge wa Chakechake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Program ya Mifuko yote hiyo iliyotajwa ya kuwaendeleza vijana, wanawake na wajasiriamali, inafanya kazi Tanzania Bara na haitekelezwi upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mifuko hiyo ilikuwa ni Mfuko wa *YDF*, *WF*na *NEDF*. Namshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na mamlaka inayohusika na mifuko hii kwa upande wa Zanzibar ambayo ni Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuona namna ya bora kuwasaidia vijana, wanawake na wajasiriamali wa Zanzibar. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, swalii la nyongeza.

MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la

nyongeza. Pamoja na majibu mazuri yaliyojibwa na Mheshimiwa Waziri, lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, jibu lake linaonesha kwamba hii mifuko haifanyi kazi Zanzibar na inafanya kazi Tanzania Bara, lakini wapo Watanzania Bara wanaoishi Zanzibar ambao nao walipaswa kunufaika na mifuko hii; ambao hawana sifa ya kunufaika kwenye mifuko kama hii wakiwa Zanzibar. Hawa wananaufaikaje? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la rafiki yangu sana Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan. Ni kwamba kwa wote wanaoishi Bara na kufanya shughuli zao huku Bara, kwa zile fursa zinazohusika na mambo ya Bara zinawagusa huku upande wa bara na wale wote wanaoishi kule Zanzibar na fursa zinazohusika katika mifuko mbalimbali ya Zanzibar, wanapata fursa hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika jambo hilo halina shida yoyote, kwa sababu siyo suala la kimuungano. Kwa hiyo, turidhie tu utaratibu wa sasa. Bahati nzuri kule kuna Wizara Maalum inafanya michakato hiyo. Ninaamini, kama kuna maeneo kidogo yanataka uboreshaji, basi inawezekana kwa ushauri mzuri wa upande wa pili, kufanyika uboreshaji wa ziada. Kwa hiyo, hiyo ndiyo hali iliyopo sasa.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu hoja yake ni nzuri, inachochea kuona pande zote za Muungano zikiwa na vitu mbalimbali ambavyo vinaweza vikasaidia wananchi katika maeneo haya. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Charles Kimei, swali la nyongeza.

MHE. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa biashara ya gesijoto imeshamiri sana duniani na imekuwa inaendelea kwa miaka mingi; na nchi nyingi zimefaidi kwa kuuza gesijoto ambayo inahifadhiwa kwenye misitu; na Tanzania yenyewe hii tunayo misitu mingi iliyohifadhiwa ambayo mojawapo ni ule wa *KINAPA* na ni mkubwa; naomba njue mkakati wa Serikali wa kuingia kwenye biashara hii ya *carbon trading* kwa sababu itatupa fedha kule kwenye vijiji vyetu. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri ili tupate majibu ya uhakika kwenye swali hili muhimu sana, lije kama swali la msingi. Labda kama unayo hayo majibu ya uhakika kwa swali hilo, karibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu aliyeliliza swali ni mtu mzito katika Kamati ya Mazingira, licha ya kumwomba alete swali hili kama swali la msingi, kwa faida kubwa ni kwamba tuna *success story* ndani ya nchi yetu katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika. Jambo hili, watu wa Tanganyika zaidi ya *3.2 billion* wanakusanya kutokana na *Carbonate Hydrates Program*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani jambo hili tutaenda kulichakata vizuri, lakini litakapokuja katika swali la msingi tutalifanyia kazi vizuri kwa heshima ya Mheshimiwa Mbunge. Ahsante.

SPIKA: Sasa nisaidie mimi ambaye siyo mtaalam, umeshalijibu swali lake ama swali lake utalijibu likija kama swali la msingi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, swali lake lije kama swali la msingi.

SPIKA: Tunaelekea Wizara ya Fedha na Mipango. Mheshimiwa Katani Ahmed Katani, Mbunge wa Tandahimba sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Cecil Mwambe.

Na. 72

**Wakulima Kulipwa Fedha Walizoweka Iliyokuwa
Benki ya *Covenant***

MHE. CECIL D. MWAMBE K.n.y. MHE. KATANI A. KATANI
aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itawalipa wakulima wa Korosho fedha zao walizofanya biashara msimu wa 2017/2018 na iliyokuwa Benki ya *Covenant* iliyofungwa kabla ya wakulima hawajatoa fedha zao?

SPIKA: Sioni nani amesimama kama ni Waziri ama Naibu Waziri. Ahaa, Naibu Waziri wa Fedha, karibu kwa majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Katani Ahmed Katani, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu ya Tanzania ilifutia leseni iliyokuwa Benki ya *Covenant* mnamo tarehe 4 Januari, 2018 kwa mujibu wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Kifedha ya mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuifutia leseni, Benki Kuu iliteua Bodi ya Bima ya Amana (*DIB*) kuwa mfilisi wa Benki hiyo kwa mujibu wa sheria. Kuanzia mwezi Machi, 2018, Bodi ya Bima ya Amana ilianza zoezi la kulipa fidia ya Bima ya Amana ya kiasi kisichozidi shilingi 1,500,000 kwa wateja waliostahili kulipwa Bima ya Amana wakiwemo wakulima wa korosho wa Wilaya ya Tandahimba na zoezi hilo bado linaendelea kwa wateja ambaa hawajajitokeza kuchukua fidia hiyo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Desemba, 2021, jumla ya shilingi 332,715,894.00 zililipwa kwa wakulima wa

korosho 1,078 kati ya wakulima 1,346 wa Wilaya ya Tandahimba waliokuwa na amana katika Benki ya *Covenant*. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 98 ya kiasi cha shilingi 337,992,095.00 zilizotengwa kwa ajili ya kulipa fidia katika Kituo cha Tandahimba.

Mheshimiwa Spika, aidha, Bodi ya Bima ya Amana inaendelea na zoezi la ufilisi wa Benki hiyo kwa kukusanya mali na madeni ya Benki hiyo ili kupata fedha za kuwalipa wateja waliokuwa na amana zinazozidi shilingi 1,500,000 ambapo kwa mujibu wa sheria na taratibu za ufilisi kiasi kitakacholipwa kitategemea fedha zitakazopatikana kutokana na kuuza mali za Benki hiyo. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Cecil Mwambe, swalii la nyongeza.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, majibu ya Serikali ni mazuri kama tulivyosikia, lakini swalii: Mpaka sasa kiasi kinacholipwa kutoka kwenye dhamana ni shilingi 1,500,000 tu hata kwa mteja aliyeweka pesa nyingi sana na wanabubiri kuuza mali za benki ndipo waweze kuwalipa; na benki nyingine hazina mali za kutosha.

Je, Serikali haioni kuna haja sasa ya kuleta sheria kwenye Bunge hili ili kuweza kuwasaidia wateja wa benki hizi? Benki ya Greenland, pamoja na benki ya *FBME* na zenyewe zimefilisika kwa muda mrefu na sasa tunaona *Covenant Bank* lakini hakuna muda mahususi wa kufanya minada na kuwalipa wateja:-

Je, Serikali na yenye haioni kuna haja ya kupanga *specific time* ili kuweza kuuza mali hizo na ikishindikana Serikali ichukue dhamana hiyo? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cecil Mwambe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Cecil Mwambe kwa maswali yake haya mazuri, maana yake maswali yake yanaonekana ni mawazo ushauri. Mfano swali la mwanzo, Serikali inalichukua wazo hili na ushauri huu wa kuongeza idadi ya kulipa hiyo fidia ya shilingi milioni moja na nusu kwa wale ambao amana yao iko zaidi ya shilingi milioni moja na nusu.

Mheshimiwa Spika, la pili pia inaonekana ni ushauri kwetu. Kwa hiyo, Serikali itatenga muda mahususi au wakati mahususi wa kukusanya mali na madeni kwa zile Benki ambazo zimefilisiwa na Serikali kwa mujibu wa sheria. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kumekuwa na malalamiko ya wakulima wa korosho wa Kata ya Lwilo na Kata ya Masasi Wilayani Ludewa dhidi ya Benki ya *NMB* ambayo iliwakopesha pembejeo wakulima mwaka 2019/ 2020, kwa sababu benki hii imekuwa ikiwakata wakulima ambao hawakukopa pembejeo:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa maelekezo kwa benki hii kusitisha makato hayo wakati Serikali inaenda kujiridhisha kwamba wakulima hawa wanatendewa haki?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kama unayo majibu mahususi kwa hoja hiyo. Kama huna, Mheshimiwa Mbunge alete swali la msingi.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni jambo jema Mheshimiwa Mbunge alete kama swali la msingi ambalo ni mahususi linahusiana na *NMB Bank* kwa shughuli hiyo ambayo inahitaji utafiti.

SPIKA: Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 73

Ukarabati wa Vituo vya Kulelea Wazee Nchini

MHE. BAHATI K. NDINGO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa Vituo Vya Wazee nchini?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, majibu:-

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM aliibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu. Pia namshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniyamini na kunitfea kuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum. Napenda kumhakikisha Mheshimiwa Rais kuwa nitafanya kazi kwa uwezo wangu wote na kwa kudra za Mwenyezi Mungu, nitatekeleza majukumu yangu ipasavyo katika kuleta maendeleo ya Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha utoaji wa huduma, Serikali imeendelea kuboresha majengo na miundombinu ya makazi ya wazee kwa awamu ambapo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 na mwaka wa fedha 2020/2021 ukarabati umefanyika katika makazi saba ya wazee ikiwemo; Nunge (Dar es Salaam), Kolandoto

(Shinyanga), Njoro (Kilimanjaro), Magugu (Manyara), Kiilima (Kagera), Fungafunga (Morogoro) na Sukamahela (Singida). Aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa Makazi ya Wazee Wasiojiweza nchini kwa kadri ya upatikanaji wa rasilimali fedha zitapopatikana. Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, swali la nyongeza.

MHE. BAHATI K. NDINGO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini nilikuwa na maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kutokana na tafiti ambazo zinaendelea inaonyesha kwamba kutakuwa kuna ongezeko kubwa la wazee duniani ikiwemo na Tanzania. Sasa Wizara inajipangaje kuhakikisha inaongeza vituo vya kulelea wazee, aidha kutoka mikoa angalau basi twende hata kwenye Wilaya.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, pamoja na ukarabati ambaao unaendelea kwenye hivyo vituo:-

Je, Serikali imejipangaje kuweka vifaa tiba na mahitaji muhimu kwa ajili ya wazee wetu ndani ya hivyo vituo?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bahati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Bahati na kumpongeza kwa kujali wazee, kwani wazee ni tunu ya Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, swali lake na mwanzo Mheshimiwa Bahati Mbunge, ushauri wake umepokelewa na kuzingatiwa katika mapendekezo ya bajeti katika kipindi cha mwaka 2022/2023. Hata hivyo kila mwaka tunaboresha mahitaji ya wazee kuhakikisha kwamba wanapata mahitaji muhimu kama vile mavazi, chakula, malazi na afya bora. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalii lake la pili ambalo linasema kwamba wazee wapewe msaada wa kisaikolojia. Makazi ya wazee yanaongozwa na kusimamiwa na Maafisa wa Ustawi wa Jamii, wataalam ambao wanatoa msaada wa kisaikolojia kwa wazee wetu. Hata hivyo, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano, mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, anawajali sana wazee, anawapenda na kuhakikisha kwamba wanapata haki zao za msingi kila wakati na pale inapohitajika. Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, swali la nyongeza.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na vituo vya wazee, Wizara ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba hawa wazee ambao wamelitumikia Taifa letu kwa jasho na nguvu zao zote kuhakikisha kwamba wanalipwa pensheni hata kama ni kidogo ili walingane na wazee wenzao wanaotoka au wanaoishi Zanzibar?

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ngoja nitoe maelezo kidogo, kwa sababu swali hilo pia litaihusu Wizara ya Fedha, ili kama huna majibu

mahuusi useme Mheshimiwa Mbunge alete kama swali la msingi.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Oscar Kikoyo alete swali hili kama la msingi.

SPIKA: Mheshimiwa Issa Mtemvu, swali la nyongeza.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa Wizara hii tayari inaona ina changamoto sana ya kupata fedha kwa ajili ya kundi hili la wazee, lakini bado wazee hawa wana changamoto sana ya uwezo.

Je, Wizara ya ina mkakati gani sasa wa kutumia ile sera ya asilimia 10 kuweza kuwaweka na wazee kupata kama asilimia mbili ili ziwasaidie?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri kama una majibu mahususi, maana hiyo ni sheria tulitunga sisi hapa Wabunge wenyewe. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Issa Mtemvu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake, Mheshimiwa Issa tunakuomba kwamba sheria bado zinafanya kazi na zitakapokamilika basi wazee hawa watapewa haki zao na watapewa msaada wa kuongezewa kiasi cha fedha kwa ajili ya mahitaji ya maisha yao. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana, Wizara ya Mifugo na Uvumi, Mheshimiwa Denis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi sasa aulize swali lake.

Na. 74

Ufugaji wa Samaki katika Bwawa la Zombo Mikumi

MHE. DENNIS L. LONDO aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Bwawa la Zombo linatumika kikamilifu kwa ufugaji wa samaki na kuondoa tatizo la ajira kwa vijana?

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi naomba kujibu swali la mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mifugo na Uvubi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ina mpango endelevu wa kufanya tathmini ya mabwawa yaliyopo katika halmashauri mbalimbali nchini ili kufahamu uwekezaji unaofaa kwenye bwawa husika kulingana na jiografia ya eneo hilo. Kwa kuwa shughuli hii ni endelevu na hufanyika kwa awamu, Bwawa la Zombo litaingia kwenye mpango wa tathmini katika mwaka wa fedha 2022/2023 ili kujuua aina ya uwekezaji unaofaa katika Bwawa hilo.

Mheshimiwa Spika, vile vile, wataalam wa Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji cha Kingolwira – Morogoro watatoa mafunzo maalum ya ufugaji samaki kwa vijana wa Jimbo la Mikumi ili kuwapa stadi za ufugaji samaki wenye tija kwenye mabwawa kwa lengo la kutengeneza ajira. ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Denis Lazaro Londo, swali la nyongeza.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Serikali ambayo yanatoa tumaini kwa vijana wa Jimbo la mikumi. Swali langu la kwanza; kwa kuwa Serikali itaangalia uwekezaji unaofaa katika bwawa hilo, je, mpango huo unahusisha pia uzalishaji wa

vyakula vya samaki katika viwanda vidogo na vya kati katika eneo la Jimbo la Mikumi ili kukuza ufugaji wa samaki?

Mheshimiwa Spika, la pili, karibu na Zombo kuna reli ya mwendokasi ambako kuna mashimo makubwa ambayo walikuwa wanachimba kokoto wakati wa ujenzi huo. Mashimo haya makubwa yana *potential* ya kubadilishwa kuwa mabwawa kwa ajili ya ufugaji wa samaki lakini pia kwa ajili ya mifugo. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba wakati umefika wa kuyatengeneza mabwawa haya ili kutatua tatizo letu? Nashukuru.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvubi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Denis Lazaro Londo, Mbunge wa Jimbo la Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, umuhimu na uhitaji wa vyakula vya mifugo nchini hususan samaki ni mkubwa sana na kwa kadri tunavyoendelea kuhamasisha ufugaji wa samaki umuhimu umezidi kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Londo, kwamba tunahitaji uwekezaji zaidi. Katika Mkakati tulio nao ndani ya Serikali ni kuvutia uwekezaji wa uzalishaji wa chakula cha samaki.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mabwawa ama mashimo yaliyotokana na ujenzi wa reli ya *SGR*, nakubaliana naye na ni wazo jema sana.

Mheshimiwa Spika, sisi katika Wizara tumeanza mazungumzo na wenzetu wa reli ili kuhakikisha kwamba mabwaya yale tunayaongezea thamani kwa kuyatengeneza miundombinu ili yaweze kutumika kwa ajili ya shughuli za ufugaji pamoja na shughuli za ufugaji wa samaki. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, swali la nyongeza.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali inatambua ufugaji wa samaki kwenye mabwawa kule ukanda wa Ziwa Victoria na maeneo yote yanayozunguka na hasa maeneo ya kandokando kwenye miji mikubwa, zoezi la ufugaji wa samaki kwenye vizimba linaendelea kukua kwa kasi na tunaamini linaweza likatoa ajira nydingi sana kwa vijana.

Je, ni upi sasa mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba vijana wengi zaidi wanaingizwa katika shughuli hizi na kupewa fedha ili waweze kuwekeza kwenye ufugaji wa vizimba?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mbunge wa Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mkakati wetu ndani ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, ni kwamba tumeweka hela kiasi cha shilingi milioni 154. Pesa hizi ni kwa ajili ya kwenda kufanya mpango wa matumizi bora, kwa lugha nyepesi, katika eneo la Ziwa Victoria, Mkao wa Mwanza na Mkao wa Kagera. Tunakwenda kufanya *demarcation* na pesa hii tumeipeleka katika Taasisi yetu ya Utafiti ya TAFIR/kwa lengo la kutuandalia maeneo mahsus ambayo vijana watakwenda kuyatumia kwa ajili ya ufugaji wa vizimba.

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi, vijana hawa tutawaweka katika ushirika ambao utawasaidia kuweza kupata mikopo na kuweza kujifanyia shughuli zao.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali Wilaya ya Bunda inaishi karibu sana na Ziwa Victoria na Jimbo la Bunda ni kilometra 45 kutoka Ziwa Victoria. Sasa kwa sababu kuna *pressure* kubwa ya uvuvi wa samaki na kwa sababu sasa tunataka kupunguza hiyo pressure ya wavuvi wa samaki.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuweka mikakati ya kuweka vizimba katika Jimbo la Bunda na hasa pale kwenye mabwawa ya kuchimbwa kwa ajili ya kufuga samaki?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni mkakati endelevu tulionao wa kuhakikisha kwamba tunakwenda kwenye eneo hili la ufugaji wa samaki na hasa upande wa Ziwa Victoria ambako kuna ufugaji wa kutumia vizimba na hivyo Jimbo la Bunda nalo litafikiwa.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Jafary Chege, swali la nyongeza.

MHE. JAFARY W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa shughuli hii ya ufugaji wa samaki inafanyika pia katika Jimbo la Ranya, kwa maana ya wilaya nzima, hasa ukizingatia kwamba umbali wa kutoka ziwa kuelekea kwenye maeneo ya wananchi haizidi hata mita tano. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia vijana wa maeneo yale ambao wanaishi karibu na ziwa ili kufanya na kuanzisha ufugaji huu wa samaki?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chege, Mbunge wa Rarya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza, kwamba ufugaji wa samaki, hasa kwenye vizimba, upande wa Ziwa Victoria ndicho kipaumbele chetu cha kule tunakolekea ili kupunguza *pressure* ya uvuvi ule wa asili. Ili kuweza kufanikiwa katika lengo hili tunahamasisha uundaji wa vikundi, hasa vikundi vya Ushirika, hivyo namwomba Mheshimiwa Chege na Waheshimiwa Wabunge wengine wote wa eneo hili waweze kuwahamasisha vijana wale wajunge katika vikundi ili tuweze kupata mikopo kuititia Benki yetu ya Kilimo na hatimaye kuweza kuifanya shughuli hii ambayo itawaingizia kipato na kukuza pato la Taifa letu.

SPIKA: Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, swali la nyongeza.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula (*FAO*) limetangaza mpango maalum wa ufugaji wa samaki katika maneo mbalimbali duniani ikiwemo Ziwa Tanganyika. Je, Serikali yetu imechukua hatua gani za haraka za kushirikiana na shirika hili katika kufanikisha mpango huo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, swali mahsusи hilo kwa mpango fulani. Kama mpango huo unaufahamu majibu tafadhali, kama huufahamu Mheshimiwa Mbunge atashauriwa alete swali la msingi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *FAO* ni wadau wetu wakubwa na tunashirikiana nao kama Serikali. Hata hivyo, kwa jambo hili mahsusи alilolisema Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda ninaomba nimkaribishe kula swali mahsusи ili tuweze kulifanyia kazi. Ahsante.

SPIKA: Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, Mbunge wa Misungwi, sasa aulize swali lake.

Na. 75

Ujenzi wa Barabara ya Mwanangwa – Misasi - Kahama kwa Kiwango cha Lami

MHE. ALEXANDER P. MNYETI aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Mwanangwa – Misasi – Kahama?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, Mbunge wa Misungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mwanangwa – Misasi – Kawekamo – Solwa – Kahama yenye urefu wa kilometa 150, ilifanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kukamilika mwaka 2017 kwa gharama ya shilingi milioni 798.8. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikiendelea na juhudzi za kutafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*), inaendelea kuifanya matengenezo mbalimbali ya barabara hii ili iendelee kupitika kipindi chote cha mwaka. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya shilingi milioni 2,809.304 zimetengwa kwa matengenezo mbalimbali pamoja na ujenzi wa madaraja saba katika maeneo yanayoathiriwa na mafuriko. Madaraja hayo ni madaraja mawili katika eneo la

Mwanzugi, madaraja matatu katika eneo la Mwakitalyo na madaraja mawili katika eneo la Solwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kuitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) imekamilisha ujenzi wa kilometra 5.15 kwa kiwango cha lami katika eneo la Kahama kuelekea Solwa. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Alexander Pastory Mnyeti, swali la nyongeza.

MHE. ALEXANDER P. MNYETI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Barabara hii tunayoizungumzia hapa ni barabara ambayo imekuwa kwenye Ilani ya Uchaguzi kwa mihula mitatu mfululizo, 2010, 2015 mpaka 2020; na Mheshimiwa Rais alipokuja Misungwi aliahidi barabara hii ianze kutengenezwa kwa kiwango cha lami haraka iwezekanavyo na Mheshimiwa Waziri tulikuwa naye pale, maelekezo ya Rais yalitoka hadharani kuwa barabara hii itengenezwe. Sasa anaposema kwamba anatafuta fedha sijauja yeye ni *TRA* ama ni nini, kwa sababu mwenye *TRA* ambaye ni Mheshimiwa Rais amesema barabara ianze kutengenezwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, swali langu la nyongeza ni kwamba, ni lini Wizara itaanza kujenga barabara hii? Kwa sababu imekuwa ikikarabati vipande vidogo vidogo ambavyo havina tija yoyote kwenye barabara hii. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pastory Mnyeti, Mbunge wa Misungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tayari jitihada za Serikali zimeonekana, tumeshafanya upembuzi yakinifu na usanifu

wa kina. Pia ili kuhakikisha kwamba barabara hii inatumika tumeshaanza kujenga madaraja ambayo mara nyingi yanafanya barabara hii isipitike.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine wa barabara hii tayari tumeshaanza kujenga kilometra tano upande wa Kahama, ambayo ni barabara hiyo hiyo. Kwa hiyo Serikali ina nia njema na mara fedha itakapopatikana yote barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami kama ahadi za viongozi wa kitaifa walivyoahidi. Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, nisaidie kuangalia Wabunge hawa waliosimama na kila mtu hapo ana barabara anayotaka kuiulizia swali. Mheshimiwa Oran Manase Njeza, swali la nyongeza.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Kwa kuwa ni ahadi ya muda mrefu ya viongozi kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Mbalizi - Shigamba. Je, ni lini barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oran Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara imeahidiwa na viongozi mbalimbali wametoa ahadi.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara hii ipo kwenye mipango ya kuanza kufanyiwa usanifu wa kina kama maandalizi ya kuanza kujenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

MHE. ALLY M. KASSINGE: Mheshimiwa Spika, nikushuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Tatu wa Bunge lako hili niliulizia kuhusiana na Barabara ya kutoka Kiranjeranje, Nanjilinji mpaka Ruangwa kujengwa kwa kiwango cha lami na majibu ya Serikali ilikuwa kwamba itajengwa mara tu fedha zitakapopatikana.

Mheshimiwa Spika, sasa je, Serikali iko tayari kwa mwaka ujao wa 2022/2023 kutenga fedha kwa ajili ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami, ambayo iko kwenye llani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Kassinge, Mbunge wa Kilwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kiranjeranje hadi Ruangwa ambayo Mheshimiwa Mbunge ameisema, ni kweli ipo kwenye llani. Hata hivyo, kama nilivyosema, ni kipindi hiki tunachoendelea na bajeti, barabara hii pengine mwaka huu itakuwepo kwenye mpango kwa ajili ya kuanza maandalizi ya kufanya usanifu wa kina. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Changamoto ambayo inawakumba watumiaji wa Bandari ya Kabwe ni barabara inayotoka Lyazumbi kwenda Kabwe na ni agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu. Napenda kujua, ni lini agizo hilo litatekelezeka kwa kuanza kujenga hiyo barabara ili tufikie malengo ya bandari yetu waliyowekeza fedha nyingi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalı la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Nkasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara aliyoisema ya Lyazumbi hadi Kabwe inakwenda kwene bandari ambayo Serikali imewekeza kwa kiasi kikubwa sana kwa ajili ya biashara kati ya Tanzania na *DRCongo*. Naomba nimhakikishie Mbunge kwamba ziko jitihada zinafanyika za kujenga kwa kiwango cha lami, lakini mpango uliopo sasa hivi ni kipanua ile barabara na kujenga madaraja makubwa na kuiweka kwa kiwango cha changarawe ili magari makubwa yawezee kupita wakati Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya mpango wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Bryceson Magessa Tumaini, Mbunge wa Busanda sasa aulize swalı lake.

Na. 76

Ujenzi wa Barabara ya Geita – Nyarugusu – Kahama kwa Kiwango cha Lami

MHE. TUMAINI B. MAGESSA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Geita kuititia Nyarugusu kwenda Bukoli hadi Kahama ambapo upembuzi yakinifu ulishafanyika?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Bryceson Magesa Tumaini, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kuandaa nyaraka za zabuni kwa barabara ya Geita – Nyarugusu – Kahama yenyе urefu wa kilometa 133.9 imekamilika mwaka 2017. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Aidha, mwaka 2021, Kampuni ya Uchimbaji Madini ya *Barrick* ilionesa nia ya kufadhili ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Kwa sasa, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Wizara ya Madini na Wizara ya Fedha na Mipango zinaendelea na mazungumzo na Kampuni ya *Barrick* kuhusu utaratibu wa ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, wakati ujenzi kwa kiwango cha lami ukisubiri upatikanaji wa fedha, Serikali kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*), inaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya shilingi milioni 838.97 zilitengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali katika barabara hii. Aidha, Wakala wa Barabara nchini (*TANROADS*) Shinyanga kwa kutumia fedha za maendeleo inakamilisha ujenzi wa mita 600 kwa kiwango cha lami katika barabara hii kuanzia eneo la Busoka katika Manispaa ya Kahama. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Bryceson Magessa Tumaini, swali la nyongeza.

MHE. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu yale yale ambayo alinipatia mwaka 2021 leo yamejirudia tena. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza kwenye swali hili. Kwa vile mazungumzo ya ahadi yaliyotolewa na Barrick yamechukua muda sasa na hayana mafanikio: Nini kauli ya Serikali kwa ujenzi wa barabara hii bila kuhusisha Barrick ili iweze kufanyika? Kwa sababu wale waliota ahadi wanaonekana kama hawapo tayari kutekeleza ahadi hiyo?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili. Kwa vile upembuzi yakinifu wa barabara hii umeshafanyika toka mwaka 2017, lakini nasikitika kwamba nyumba zilizoko barabarani zote hazina alama:-

Je, nini mpango wa Serikali kuonyesha wananchi kwamba nyumba hizi zitabomolewa kama barabara itajengwa hivi karibuni?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Magessa, Mbunge wa Busanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, bado mazungumzo yanaendelea na yako kwenye hatua nzuri. Kama yangetuwa yamekwama, tungeacha na kutafuta utaratibu mwingine. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mazungumzo yanaendelea kati ya *Barrick* na hizo Wizara ambazo nimezitaja.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; tunapoweka alama za kuanza kubomoa, ni pale ambapo taratibu zote za kuanza ujenzi zimeanza na fedha ya kutoa fidia imeshapatikana. Tukishafikia hatua hiyo, basi tutaanza kuweka alama kuonesha wananchi ambao watapisha barabara hiyo. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, swalii la nyongeza.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza swalii la nyongeza. Barabara ya Ngongo - Ilola na Michiga yenye urefu wa...

SPIKA: Mheshimiwa simamisha hicho kisemeo.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza kuhusu barabara ya Ngongo - Milola na Michiga. Hii barabara ina urefu wa kilomita 82. Tuliambiwa itajengwa kwa kiwango cha lami, lakini mpaka leo bado hatujaiona hiyo lami. Kibaya zaidi kwenye barabara hii, sasa hivi mvua hizi zinazonyesha, hii barabaraba imekatika yote na wakaweka mchepuko, *diversion* ya pili; na hata ile *diversion* ya pili nayo imekatika; na barabara hii ni kiungo muhimu baina ya Majimbo matatu; Jimbo la Lindi, Jimbo la Mchinga na Jimbo la Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof/Kicheko*)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, tunaomba kauli ya Serikali, lini barabara hii itarekebishwa? Kama siyo kurekebishwa ina maana kwamba Majimbo haya yote yatakuwa yamejifunga. Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI – (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Salma Kikwete, Mbunge wa Mchinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Salma kwa jinsi ambavyo anafuatilia hii barabara ya Ngongo - Milola - Michiga yenye kilometra 82. Barabara hii inapita kwenye miinuko mikali; na kama alivyosema pia kuna maporomoko mengi ya maji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara hii imekatika, naomba kutumia nafasi hii kumwangiza Meneja wa *TANROAD* ahakikishe kwamba kesho anafika maeneo yote na kuhakikisha kwamba anapeleka Wakandarasi kwa ajili ya kurekebisha hii barabara na nipate taarifa kuanzia kesho ambapo pia atawasiliana na Mheshimiwa Mbunge kuona

kwamba hili suala linafanyika ili kuhakikisha kwamba barabara hii inapitika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi kwa kiwango cha lami, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ina azma ya kujenga na fedha bado zinaendelea kutafutwa. Basi zikipatikana, tunaanza kujenga hii barabara kwa kiwango cha lami. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ungetusaidia kutoa hilo agizo kwa Mameneja wa Mikoa yote ili Wabunge humu ndani wajue kwamba barabara zilizokatika kwenye maeneo yao ambako hakuna mawasiliano, basi wajue kila mahali kazi itafanyika. Vinginevyo, utaona Wabunge bado wamesimama wengi hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kuwaelekeza Mameneja wote wa *TANROADS* katika mikoa yote, wahakikishe kwamba barabara zote ambazo zimepata changamoto wanakwenda haraka na kama wanahitaji msaada wa Makao Makuu, basi waweze kuwasiliana na Wizara moja kwa moja ama *TANROADS* Makao Makuu ili barabara hizi ziendelee kupitika. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa namtafuta hapa Waziri wa TAMISEMI ili aseme jambo na ye ye kuhusu *TARURA*, pengine na yenyewe ingejaribu kusaidia hapa. Sijui, Naibu Waziri amekwenda kwenye kikao ama vipi, lakini *TARURA* tungesikia neno kutoka kwenu pia ingetusaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Halima James Mdee, swalii la nyongeza, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta swalii la nyongeza.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, nipo hapa. Nipo.

SPIKA: Mheshimiwa Halima kwa sababu Mheshimiwa Margaret Sitta ameshaanza kuongea, utapewa nafasi baada ya yeye kumaliza.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imefanya kazi kubwa sana ya kujenga barabara nzuri kutoka Ndondo mpaka Kigoma. Tatizo kubwa linalotukabili sisi Urambo ni kwamba kona ya kuingilia Urambo Mjini inasababisha ajali kubwa sana. Sasa kwa kuwa nilishaomba Serikalini kujengewa *round about* na Serikali imeshafanya utafiti wake, imeshapata na garama: Je, Serikali iko tayari sasa kujenga hiyo *round about*. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Sitta, Mbunge wa Urambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama alivyosema kwamba kama tathmini ilishafanyika, maana yake ni kwamba Serikali ina dhamira ya kuijenga. Naomba baada ya hapa, nimwombe Mheshimiwa Margaret Sitta tuweze kuona ni wapi tumekwama ili tuweze kuamua, kwa sababu kama kazi imeshafanyika, maana yake ni kwamba Serikali imeshaona kuna umuhimu wa kujenga.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Halima James Mdee, swali la nyongeza.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Miradi mingi ya Serikali ya barabara ina mwaka kati ya mmoja, kumi na mingine hadi 15 na changamoto kubwa ni kwa sababu tunaahidi barabara nyingi, lakini tuna fedha kidogo, hali inayosababisha tunagawana kilometra moja moja, matokeo yake barabara hazikamiliki, lakini tunatumia fedha nyingi sana kulipa *interest* kwa wakandarasi kwa sababu hatulipi fedha zote kwa wakati. Sasa Kamati ya bajeti ilishauri kwamba kwa nini Serikali isianze kumaliza barabara zote ambazo ziko kwenye mpango, kisha ndiyo tuanze upya?

Je, wazo hili la Kamati ya Bajeti ambalo Bunge limeridhia kwamba tumalize viporo vyote vikamilike, barabara ikamilike; Serikali imelipuuza ama inalifanyia kazi? (*Makof*)

SPIKA: Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haiwezi kupuuza ushauri wa Kamati ya Bajeti. Pia nataka nimhakikishie Mheshimiwa Halima Mdee kwamba tunaendelea kuufanya kazi ushauri wa Kamati ya Bajeti na tutakuja kulileta kama Serikali, tuone namna tutakavyofanya kuhusu kuhamua ni barabara zipo zijengwe na kwa wakati upi?

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa John Constantine Kanyasu, swali la nyongeza.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo yamekuwa ni yale yale kila mwaka, lakini mwaka wa fedha ulioisha, barabara ya Geita - Kahama ilitengewa shilingi bilioni tatu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa nini Wizara isitangaze kumpata mkandarasi na kuanza na fedha hizo zilizotengwa ili kipande hicho kitakachoanza kujengwa kianze kuanza kazi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, fedha iliyotengwa hii ni pamoja na fedha tunayotegemea kuipata kama mazungumzo yatakamilika na wenzetu wa *Barrick*. Kwa hiyo, mara fedha itakapopatikana, basi kazi hizo zitaanza kwa pamoja. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba, sasa aulize swali lake.

Na. 77

Barabara ya Ifakara – Kihansi – Madeke

MHE. GODWIN E. KUNAMBI aliuliza:-

Je, ni lini Ujenzi wa Barabara ya Ifakara – Kihansi – Madeke utaanza?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Ifakara – Kihansi hadi Madeke yenye kilometra 220.22 ni sehemu ya barabara ya Ifakara – Mlimba – Taweta – Madeke – Lupembe hadi Kibena

Mkoa wa Njombe ambayo ni barabara ya mkoa inayounganisha mikoa ya Morogoro na Njombe katika Kijiji cha Madeke.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kuandaa nyaraka za zabuni kwa sehemu ya Ifakara hadi Kihansi yeny urefu wa kilometra 126. Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) imeanza maandalizi ya kutangaza zabuni kwa ajili ya kupata Mkandarasi wa ujenzi wa kilometra 50 kati ya Ifakara hadi Mlimba kwa kiwango cha lami ndani ya mwaka wa fedha wa 2021/2022. Aidha, kipande cha barabara katika Kihansi na Mlimba chenye urefu wa kilometra 24.26 kimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, sehemu iliyobaki itaendelea kujengwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha hadi barabara yote ikamili kwa kiwango cha lami. Pamoja na juhudhi hizi, Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, inaendelea kuifanya matengenezo mbalimbali ili kuhakikisha inapitika majira yote ya mwaka ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya shilingi bilioni 2.729 zimetengwa. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Godwin Kunambi, swali la nyongeza.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Naomba niulize kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii inaunganisha mikoa ya nyanda za juu kusini; Mkoa wa Morogoro, Mkoa wa Njombe, Mkoa wa Ruvuma, Mkoa wa Mbeya mpaka Rukwa na inatoa *alternative route* ya barabara ya Iringa - Morogoro yaani kupitia Kitonga. Sasa katika majibu ya Serikali, ameeleza kwa habari ya kipande cha kutoka Ifakara mpaka Kihansi, kuna kipande cha kutoka Kihansi kwenda Masagati - Madeke mpaka *Kibena Junction*; kipande hiki, zabuni ya kumtafuta Mkandarasi wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu

wa kina ilitangazwa mwaka wa fedha uliopita, hadi sasa hajapati kana.

Mheshimiwa Spika, swali langu sasa:-

(a) Ni lini sasa Serikali inakwenda kukamilisha kazi hii ya kumpata Mkandarasi huyo?

Mheshimiwa Spika, (b)...

SPIKA: Tafadhalii uliza swali hilo moja kwa moja.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa...

SPIKA: Uliza swali tu, mwanzoni umetoa maelezo mrefu sana Mheshimiwa.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa za nchi yetu, Mikoa mingi haijaunganishwa kwa lami; swali langu lingine ni kwamba:-

(b) Ni lini Serikali inakwenda kuunganisha mikoa hii michache ambayo haijaunganishwa kwa lami, ukiwemo Mikoa wa Morogoro?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kunambi Mbunge wa Mlimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema, ni lini tunakwenda kuunganisha mikoa yote? Ndiyo kazi inayoendelea. Hata katika jibu la msingi, ndiyo maana hata hii barabara tunaiunganisha kati ya Morogoro na Njombe.

Kwa hiyo, tunaendelea na ni kipaumbele kikubwa sana kwa Serikali kuhakikisha kwamba mikoa hii inaunganishwa kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, Mbunge jitihada unaziona, tayari tunatangaza *tender* katika kuhakikisha kwamba hizi barabara zinaunganishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mkandarasi upande pili wa kutoka Lupembe - Madeke kuja Taveta, *tenderinatangazwa* tena baada ya kukosa Mhandisi Mshauri. Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba taratibu zinaendelea na Mkandarasi na Mshauri atakapopatikana, ataanza kufanya kazi ya kufanya ufanifu wa barabara hiyo. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa barabara ya kutoka Korandoto kuelekea Meatu iko kwenye llani: Je, ni lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Midimu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ya Kolandoto ambayo inapita Sibiti kwenda Karatu – Haydom – Mbulu, barabara hii ni ndefu na tuko kwenye mpango wa kuanza kujenga kipande cha Mbulu kuja Haydom kilomita 50. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge na kipande cha Sibiti tayari daraja limeshajengwa na tutategemea katika bajeti ya mwaka huu na ambayo tunaendelea nayo kuwa na barabara za maingilio zisizopungua kilomita 20 pande zote mbili. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari

tumeshaanza kutekeleza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Neema Mgaya, swali la nyongeza.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwanza, naipongeza Serikali kwa kutujengea daraja nzuri linalotuunganisha Wilaya ya Ludewa pamoja na Mkoa wa Ruvuma. Serikali imefanya kazi kubwa sana:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya Njombe – Ludewa – Manda – Itoni?

Mheshimiwa Spika, barabara hii ikikamilika itakuwa na umuhimu mkubwa sana wa kuunganisha Ludewa pamoja na Ruvuma, lakini vile vile watu wa Ruvuma watapita *shortcut* baada ya kuzunguka...

SPIKA: Mheshimiwa, swali la nyongeza hilo.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Spika, vile vile barabarabara hii itawezesha mradi wa Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Njombe – Ludewa – Manda ni barabara ambayo tayari Serikali imeanza kuijenga. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Tanzania tuna barabara hii tu kilometra 50 ambayo

mkandarasi yuko *site* tunajenga kilometra 50 barabara nzima kwa kiwango cha zuge ambayo inakwenda kuunganisha na hilo daraja, hatuna barabara nyingine Tanzania kama hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nataka nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kuanzia *junction* pale inapotoka barabara kwenda Songea hapa Itoni kwenda Lusitu, hii barabara tayari tunatangaza zabuni kilometra 50 kwenda kuunganisha pale ambapo tumeanza kujenga barabara ya zuge ili hatimaye tuweze kukamilisha barabara yote kwa kiwango cha lami. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tukiwa hapo kwenye Ujenzi na Uchukuzi, nilikuwa nimesema habari ya *TARURA*, naona Naibu Mawaziri wameshaingia humu ndani, Naibu Waziri anayehusika na *TARURA* aseme jambo kwa sababu huko tunapigiliwa sana simu barabara zimekatika kwenye majimbo.

Sasa kila Mbunge hapa hawezi kupata nafasi ya kueleza, sasa toeni maelekezo ya jumla kwa *TARURA* nchi nzima ili barabara zinazosimamiwa na *TARURA* ambazo zimekatika na hazipitiki wao waende wakazitazame ili wananchi waweze kupata huduma ya barabara. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu mwongozo ama maelekezo ambayo Ofisi yako imeyatoa kwetu Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nimelipata suala hili vizuri, nawaagiza Mameneja wote wa Mikoa wa *TARURA* pamoja na halmashauri zote nchini kuanzia siku ya kesho waende katika maeneo yote nchi nzima kwenda kufanya tathmini haraka iwezekanavyo na kutupatia Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuititia kitengo chetu cha *TARURA* ili angalau tuweze kutoa fedha katika zile fedha zetu za dharura. Katika yale maeneo ambayo bajeti yake ipo maana yake

tutapeleka zile fedha kuhakikisha zinakwenda kufanya hiyo kazi ambayo imekusudiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie tu kabisa hili agizo ambalo tumelitoa litatekelezeka na hiyo taarifa ikishafika tutaitleta katika Bunge lako Tukufu kabla ya Bunge hili kwisha. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa maelekezo hayo kwa TARURA.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii; Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalı lake.

Na. 78

**Makongamano ya Kimataifa Kukuza Utalii wa
Mlima Kilimanjaro**

MHE. ESTHER E. MALLEKO aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha makongamano ya Kimataifa ili kukuza utalii wa Mlima Kilimanjaro?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, lakini kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuendelea kutuamini mimi na Mheshimiwa Waziri kuendelea kuhudumu Wizara hii ya Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Spika, kipekee nikupongeze wewe binafsi kwa kuteuliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; tunakupongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau imekuwa ikiendelea kuutangaza Mlima Kilimanjaro kwa kutumia mbinu mbalimbali zikiwemo: -

- (a) Onesho la Utalii la Kimataifa la *Kilifair linalofanyika* Mjini Moshi Mwezi Juni kila mwaka;
- (b) Mbio za Kilimanjaro (*Kilimanjaro Marathon*) zinazofanyika Mkoani Kilimanjaro mwezi Februari kila mwaka;
- (c) Kushiriki makongamano mbalimbali ya kimataifa ikiwemo *WTM* – London, *ITB* - Ujeruman, *Fitur-Hispania* na *Expo - 2020 Dubai*;
- (d) Kushiriki makongamano ya kimataifa yanayolenga kuimarisha uhifadhi na kutangaza utalii wa Mlima Kilimanjaro likiwemo Kongamano la Milima Mirefu Duniani (*International Mountains Alliance - ITA*);
- (e) Mlima Kilimanjaro ni moja ya eneo la urithi wa dunia ambapo kupitia mikutano mbalimbali ya *UNESCO* Mlima huo hutangazwa;
- (f) Kuwatumia watalii wanaofika Tanzania kama mabalozi wa kuutangaza Mlima Kilimanjaro;
- (g) Kuendelea kutumia matukio muhimu ya Kitaifa kama sherehe za Uhuru kuhamasisha jamii kupanda Mlima Kilimanjaro; na
- (h) Kuandaa na kushiriki katika Onesho la Kwanza la Kimataifa la Utalii la Jumuiya ya Afrika Mashariki lilo fanyika Jijini Arusha ili kutangaza vivutio vya utalii ikiwemo Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kubuni mikakati zaidi ya kuutangaza Mlima Kilimanjaro kwa maslahi mapana ya nchi. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, swalii la nyongeza.

MHE. ESTHER E. MALLEKO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Wizara lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; je, Wizara ina mkakati gani kuongeza watalii kwa sababu kutoptera na UVIKO-19, idadi ya watalii wanaopanda Mlima Kilimanjaro imepungua sana kutoka 50,000 mpaka 12,000 kwa mwaka 2020. Je, Serikali sasa ina mkakati gani wa kuweza kuongeza watalii na kusaidia ajira kwa vijana wanaotegemea mlima huo?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; akinamama wajasiriamali wa Kilimanjaro wanaojishughulisha na shughuli za utalii tunaomba na wao waweze kupatiwa mikopo ili waweze kutangaza zaidi mlima wetu, mbuga zetu na utalii kwa ujumla. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu kwa swalii la kwanza, swalii la pili nadhani ni la Wizara nyingine. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum Kilimanjaro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Esther kwa juhudini nzuri anazozifanya za kuendelea kutangaza vivutio vya utalii ukiwemo Mlima Kilimanjaro. Nampongeza sana kwa sababu amekuwa ni balozi mzuri wa kuhakikisha eneo hili linaendelea kuvutia watalii wengi.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo ameuliza kwamba tuna mkakati gani wa kuendelea kuongeza watalii na kuongeza ajira kwa vijana. Eneo hili Wizara imekuwa ikibuni mbinu mbalimbali zikiwemo kuanzisha *marathons* mbalimbali katika maeneo mbalimbali ya hifadhi, lakini lengo ni kuhakikisha kwamba watalii wengi wanakwenda kuviona vivutio lakini pia kuwa mabalozi wa kuendelea kuvitangaza.

Mheshimiwa Spika, hili ni shahidi hata Watanzania wa leo wamekuwa wazalendo na killa mtu sasa hivi anamhabarisha mwenzake kuhakikisha kwamba wanafika kwenye vile vivutio, lakini siyo kufika tu, kuisemea Tanzania ndani ya nchi na maeneo mengine ya nje ya nchi na lengo ni kukuza utalii na kuongeza pato la Taifa. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Judith Kapinga, swali la nyongeza.

MHE. JUDITH S. KAPINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na kuutangaza Mlima Kilimanjaro ningependa kufahamu, je, Serikali ina mkakati gani wa kutangaza vivutio vidogovidogo ambavyo vipo katika mikoa hasa Mkao wa Ruvuma, Wilaya ya Mbanga, yenye vivutio vidogo vingi vya kihistoria vyenye kuvutia ili kupata watalii na kuongeza mapato ya ndani?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kapinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa na vivutio vidogovidogo ambavyo kwa nia moja au nyingine Serikali ilichelewa kuviiuba, lakini Wizara ina mkakati wa kuhakikisha inaibia na kuvitangaza vivutio hivi katika kila mkoa, wilaya na kata.

Mheshimiwa Spika, vivutio vingi vidogovidogo havina *GN*, hivyo tumeendelea kuelimisha wananchi, kuelimisha Serikali za Vijiji, kata na halmashauri kuhakikisha kwamba yale maeneo ambayo yanasmamiwa na halmashauri ama vijiji wayaibue na Serikali kuitia Wizara ya Maliasili na Utalii itatoa wataalam wa kuweza kushauri na kutoa usaidizi wa kuhakikisha kwamba haya maeneo yanapata *GN* na kuyatangaza na wale watalii waweze kufika katika maeneo hayo. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, sasa aulize swali lake.

Na. 79

Vitambulisho vya Taifa kwa Watu Wenye Haki ya Uraia

MHE. FLORENT L. KYOMBO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawatambua watu wenye haki ya Uraia ili wapate Vitambulisho vya Taifa pamoja na kuwapa Uraia watu ambao siyo raia lakini wameishi nchini kwa zaidi ya miaka kumi na tano?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI
aliibu: -

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kuwa na afya na leo kushiriki kwenye kikao cha Bunge.

Mheshimiwa Spika, pia nimshukuru Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuniamini kuwa mmoja wa wasaidizi wake katika nafasi ya Naibu Uwaziri. Ahadi yangu kwake ni kutekeleza majukumu haya kwa uadilifu, uaminifu na bidli kubwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, nikupongeze kwa kuchaguliwa kwa kura zote kuwa kiongozi wetu wa Bunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo sasa, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na zoezi la kuwatambua na kuwapatia vitambulisho wale wote wanaostahili. Aidha, zoezi hili ni endelevu kwa kuwa kila mwaka idadi ya watu wanaofikisha umri na vigezo vyta kutambuliwa na kusajiliwa inaongezeka. Aidha, idadi ya wagensi wakazi na wakimbizi wanaoingia nchini imekuwa ikiongezeka na hivyo kuhitaji kusajiliwa na kutambuliwa ili kuimarisha ullanzi na usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utaratibu wa kuwapatia uraia wa Tanzania (Tajnisi) wagensi ambao wanaomba uraia wa Tanzania ikiwa wamekidhi sifa na vigezo vyta kutajnisiwa uraia kwa mujibu wa Sheria ya Uraia Sura ya 357, Toleo la Mwaka 2002 na Kanuni zake. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Florent Kyombo, swali la nyongeza.

MHE. FLORENT L. KYOMBO: Mheshimiwa Spika, nikushukuru tena kwa nafasi. Ni mara ya pili nauliza swali kama hili katika Bunge lako Tukufu, lakini kwa imani kubwa niliyonayo kwa Waziri wa Mambo ya Ndani, ndugu yangu, Mheshimiwa *Engineer Masauni* na Mheshimiwa Sagini, naamini sasa hili suala litakwenda kutafutiwa ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Nkenge, Wilaya ya Misenyi, hasa Kata za Mutukura, Kakunyu, Minziro na maeneo mengine wamekuwa na mila na desturi zinazofanana kabisa na Nchi ya Uganda. Sisi tunaongea Ruganda lakini majina unayoyakuta upande wa Tanzania ni sawasawa na unayoyakuta upande wa Uganda. Wataalam

wetu wa Uhamiaji wamekuwa wanatumia kigezo hicho kuwa-judge kwamba siyo raia kwa sababu ya lugha na majina yale.

Mheshimiwa Spika, swali langu; je, ni lini Serikali itatambua hayo mahusiano ya ukaribu ya mila na desturi wananchi wakapewa haki yao ya uraia na waweze kupata pia vitambulisho vya *NIDA?* (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa kuwa sheria, kama alioitaja Naibu Waziri ya mwaka 1995 ya Uraia inaruhusu mwananchi ambaye amekaa katika nchi yetu kwa muda wa takribani miaka saba hadi kumi kwa tabia njema aweze kupata uraia wa Tajnisi. Sasa Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri, hamuoni ni muda muafaka twende wote katika kata hizo tukae na wananchi tuwaongoze wajaze fomu waweze kupata uraia na kuishi kwa amani katika nchi yao? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:
Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Kyombo kwa namna anavyofuatilia kwa karibu maslahi ya wananchi wake, hususan anaona wanakosa uraia amba wanastahili.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema, bahati nzuri vigezo anavifahamu, ametaja uraia mwema lakini viko vigezo vingine ambavyo viro kwa mujibu wa sheria, kwa haraka nitaje vichache: -

Mheshimiwa Spika, tunasema kabla ya tarehe ya kuwasilisha maombi yake ya uraia awe alikuwepo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miezi 12 mfululizo; kwamba katika kipindi cha miaka kumi kabla ya muda wa miezi 12 awe ameishi ndani ya Jamhuri ya Muungano kwa kipindi kisichopungua miaka saba; awe na ufahamu wa kutosha wa Lugha za Kiswahili na Kiingereza au Kiingereza; awe mwenye tabia njema. Hiyo ni moja, lakini mbili za mwisho,

awe amechangia au ameshiriki katika kukuza uchumi wa Taifa na mwisho aahidi kwamba akipata uraia anayo nia ya kuendelea kuishi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo ikiwa amekidhi vigezo hivi kwa kweli ana haki ya kupewa uraia.

Mheshimiwa Spika, ombi lake la pili, mimi na Waziri wangu, tuko tayari kuongozana naye na wataalam wetu ili kuona changamoto ambayo wanakabiliana nayo wananchi hawa walioko mpakani. Kuzungumza lugha ya nchi jirani hakiwezi kuwa kigezo cha kumnyima mtu uraia kwa sababu hali ya mipakani iko hivyo katika maeneo yote. Nashukuru.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Rehema Migilla, swali la nyongeza.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi nami niulize swali dogo la nyongeza. Mwaka 2014 raia kutoka Burundi waliweza kupatiwa uraia na sasa hivi wana vitambulisho vya *NIDA* kama raia wengine wa Tanzania. Hata hivyo, katika mchakato huo raia wapatao 6,000 waliwasilisha maombi ya kuweza kupatiwa uraia ili wawe raia wa Tanzania, lakini tangu mwaka huo waliojaza hizo fomu mpaka leo hii hawajaweza kupatiwa uraia.

Je, ni lini sasa mchakato wa kuwapatia uraia hawa raia wangu 6,000 walibakia utakamilika ili na wao waweze kupata uraia Tajnisi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, swali hilo liko mahususi kwa ajili ya hao wananchi 6,000, kama unayo majibu mahususi unaweza kumjibu Mheshimiwa Mbunge, kama huna majibu mahususi Mbunge anayo nafasi ya kuleta swali la msingi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nakubaliana na ushauri wako; alete swali mahususi ili tuweze kuandaa majibu yake kwa ufasaha. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Shangai, swali la nyongeza.

MHE. EMMANUEL L. SHANGAI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Wananchi wangu wa Kata ya Nguserosambu, Soitsambu na Ololosokwan wanakuwa na shida ya kunyimwa vitambulisho pamoja na vyeti vya kuzaliwa vya Tanzania kwa kisingizio kwamba, wao ni raia wa Kenya. Je, ni lini Serikali itawapatia wananchi wale fursa ya kupata vyeti vya kuzaliwa pamoja na namba za *NIDA*?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, swali hilo pia liko mahususi kwa kata alizozitaja Mheshimiwa Mbunge. Kama unayo majibu mahususi impatie Mheshimiwa Mbunge, kama huna swali hilo liweze kuja kama swali la msingi ili apate majibu mahususi kuhusu hoja yake.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshauri Mheshimiwa Mbunge alete swali mahususi ili tuweze kuanda majibu stahiki. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Haji Amour Haji, Mbunge wa Pangawe, sasa aulize swali lake.

Na. 80

Kuziwekea Utaratibu Maalum Kampuni Binafsi za Ulinzi

MHE. HAJI AMOUR HAJI aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kuwa na Chombo Maalum (*Agency*) kitakachosimamia shughuli zote za kampuni binafsi za ulinzi ili kuongeza wigo wa kiutendaji pamoja na kuwepo kwa sheria itakayosimamia kampuni hizo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haji Amour Haji, Mbunge wa Pangawe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali haioni sababu ya kuanzisha chombo maalumu (*Agency*) cha kusimamia makampuni binafsi ya ulinzi. Jeshi la Polisi linatosha kusimamia shughuli za makampuni hayo kama ilivyo sasa kwa sababu ndiyo taasisi iliopewa mamlaka kisheria ya kutoa leseni na hati za umiliki wa silaha hapa nchini ambazo pia humilikiye na makampuni hayo. Utaratibu huo hutoa urahisi wa kufuatilia mwenendo wa makampuni katika utunzaji na matumizi ya silaha hizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo kwa sheria itakayosimamia makampuni binafsi ya ulinzi. Tayari mapendelekezo ya kutungwa kwa sheria hiyo yapo kwenye hatua zaa awali za mawasiliano baina ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Baada ya maridhiano kati ya Serikali zetu mbili kufikiwa, maandalizi ya sheria hiyo yataendelea kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo.

SPIKA: Mheshimiwa Haji Amour Haji, swali la nyongeza.

MHE. HAJI AMOUR HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa vile Serikali inatambua umuhimu wa kuwepo kwa sheria ya makampuni ya ulinzi binafsi, swali langu ni hilli; je, sheria gani kwa sasa hivi inayotumika kuwapatia vibali hayo makampuni binafsi ya ulinzi?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa sasa hakuna sheria mahususi kwa ajili ya kazi hiyo, badala yake inatumika miongozo inayotolewa na Mkuu wa Polisi Nchini (*IGP*).

SPIKA: Mheshimiwa muuliza swali, naona ultaka kusimama tena, ama sijakuona vizuri. Ahsante sana.

Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

SPIKA: Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Je, Serikali imejipangaje kurudisha imani inayopotea kwa wananchi kwa Jeshi la Polisi kutokana na tuhuma mbalimbali zinazoendelea zinazowahusu Polisi?

SPIKA: Tafadhali peleka swali la msingi Mheshimiwa Jesca Msambatavangu. Kwa sababu ukiuliza kwa ujumla namna hiyo, tutakuwa hatuelewi ujibewe vipi na Serikali.

Mheshimiwa Amina Daud Hassan, swali la nyongeza.

MHE. AMINA DAUD HASSAN: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa tunayo makampuni mengi ya binafsi katika nchi yetu:-

Je, ni lini Serikali italeta Muswada wa kuwa na Sheria ya Makampuni Binafsi ya ulinzi? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI, WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi ni kwamba mashauriano yanaendelea baina ya Serikali zetu mbili; Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili turidhiane. Kwa sababu suala hili linagusa Muungano, hatuvezi kulifanya upande mmoja wa Muungano tukasema tumekamilisha.

Mara taratibu hizo zitakapokamilika, *then* tutapeleka Muswada kwa ajili ya kupitiwa na kuridhiwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Almas Maige, swalil la nyongeza.

MHE. ATHUMAN A. MAIGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Jibu la Mheshimiwa Waziri limeniridhisha. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha Maswali kutoka kwa Wabunge na Majibu kutoka upande wa Serikali. Sasa nilete matangazo niliyonayo hapa mbele.

Tangazo la kwanza ni la wageni waliopo Bungeni siku ya leo. Kwanza ni wageni waliopo Jukwaa la Spika; na hawa ni wageni wangu 10 ambaao ni Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Mipango kutoka Bunge la Uganda, pamoja na Maafisa wa Bunge hilo, wakiambatana na Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Uganda. (*Makofi*)

Kwanza ni Dkt. Kayefa Kiwanuka ambaao wao wanaita Chiwanuka; huyu ni Mwenyekiti wa hii Kamati na ndiye anayeongoza msafara. Ameongozana pia na Mheshimiwa Aval Jane Pakuto ambaye ni Makamu Mwenyekiti. Karibu sana. Yupo pia Mheshimiwa Maximus Ochai, yeye ni Mjumbe; yupo Mheshimiwa Hanifa Nabukehela, naye ni Mjumbe; yupo pia Mheshimiwa Ennos Asiimwe naye ni Mjumbe; yupo pia Mheshimiwa Karim Masaba, naye ni Mjumbe. (*Makofi*)

Kama nilivyosema, wameongozana na Maafisa; yupo Ndugu Stephen Sunday ambaye ni Naibu Mkaguzi Mkuu, karibu sana; yupo pia Ndugu Caroline Bonabana ambaye ni Afisa wa Bunge, karibu sana; yupo Ndugu, nadhani huyu ni Mkurugenzi wa Sheria ya Bunge la Uganga; yupo Ndugu Samuel Musana ambaye pia ni Afisa wa Bunge, karibu sana;

yupo pia Ndugu Maureen Muhumuza, naye pia ni Afisa wa Bunge. Karibuni sana sana wageni wetu kutoka Uganda. (*Makofi*)

Wageni hawa wameongozana na wenyeji wao ambao ni Ndugu Charles Kichele ambaye ni *Controller and Auditor General* wa Tanzania. Ahsante sana kwa kuwakarimu au kuwakirimu wageni. Ndugu Edwin Rweyemamu yeye anatoka Ofisi ya CAG pia; yupo pia Ndugu Gabriel Ntego, karibu sana; yupo pia Ndugu Eveline Thomas, karibuni sana. (*Makofi*)

Sasa Waheshimiwa Wabunge hawa wageni wetu wanatoka Uganda lakini wamepata fursa ya kuonana na Kamati zetu na kufanya nao mukutano ambazo ni za usimamizi kwa maana ya PAC, LAAC, PIC na Kamati ya Bajeti. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Sasa sintazungumza Kiingereza, nao wamesema sasa hivi Kiswahili Uganda kipo vizuri. Kwa hiyo, wameelewa kabisa yanayoendelea humu ndani, kwa hiyo, sitazungumza Kiingereza ili wanielewe. Wameshaelewa mambo yote. (*Makofi*)

Tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge; kwanza ni wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, ambaye ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni watoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. Watoto wake hawa wameongozwa na Ndugu Diana Mabula, ahsante sana. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu wote tumpongeze Mheshimiwa Angeline Mabula kwa hiyo nafasi alioipata na leo ameapishwa. (*Makofi*)

Haya ahsanteni sana. Mheshimiwa Mabula wakati Mawaziri na Naibu Mawaziri wenzake wakiapa yeye hakupata hiyo fursa, kwa hiyo, ameipata leo. Karibu sana Mheshimiwa Mabula uungane nasi kwenye kazi na

tunakutakia kila la heri katika majukumu yaliyo mbele yako. (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Florent Kyombo ambaye ni Ndugu Simon Fidelis Kibarabara ambaye ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Wilaya kutoka Misenyi, Mkoa wa Kagera. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunao wageni 16 wa Mheshimiwa Shally Raymond ambaao ni watumishi wa Kituo cha Haki za Binadamu wakiongozwa na Mkurugenzi, Ndugu Anna Henga. Karibuni sana viongozi na watumishi wa Kituo cha Haki za Binadamu. Wakati mwingine humu ndani nikisema umri umesonga watu huwa hawanielewii vizuri, lakini huyu Mkurugenzi jamani ni mwanafunzi wangu. Hebu simama kidogo! Mnaweza kupata picha, kama mtu niliyemfundisha amekuwa Mkurugenzi, basi mjue mambo yamesonga kidogo. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wa tatu wa Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo ambaao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni Arumeru Mashariki, Mkoa wa Arusha wakiongozwa na Ndugu Judith Mollel. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Ally Juma Makoa, ambaye ni rafiki yake kutoka Japan, Ndugu Jamila Songolo Nkya. Karibu sana. Karibu sana. Haya nilikuwa naangalia hili jina nikasema, mbona kama ametoka hapa hapa huyu! Karibu sana mgeni kutoka Japan. (*Makofi*)

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda ambaao ni uongozi wa CCM wa Kata kutoka Jimbo la Kigoma Mjini, Mkoa wa Kigoma wakiongozwa na Ndugu Edward Misigano Kilinzi. Karibuni sana. Mheshimiwa Ng'enda nilijua Kata zote zimeshajaa hapa, kumbe wamekuja kwa uwakilishi! Ahsante sana. (*Makofi*)

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Bonnah Kamoli ambaye ni rafiki yake kutoka Kyela. Huyu anaitwa Obert Benn Mwakifwange. Karibu sana. Eeh, jamani Mheshimiwa

Mbunge wa Segerea ana rafiki kutoka Kyela, mambo mazuri haya. (*Makofi/Kicheko*)

Mgeni wa Mheshimiwa Joseph Kakunda ambaye ni Kamishna wa Mikopo ya Elimu ya Juu (*TAHLISO*) kutoka Jijini Dar es Salaam na huyu ni Ndugu Emmanuel Martin. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wanane wa Mheshimiwa Emmanuel Shangai ambaa ni viongozi na wananchi kutoka Ngorongoro Mkoani Arusha wakiongozwa na Kiongozi wa Mila Ndugu Raphael Long'oi. Karibuni sana, sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wa walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi 90 na walimu 10 kutoka Shule ya Sekondari ya Wasichana Mtakatifu Monica ya Moshono Jijini Arusha. Karibuni sana, sana. Sijajua kama hii shule ni ya wasichana peke yao, lakini kama nimeona wasichana. Wapo wakaka hapo? Ni wasichana eh! Jamani tuwapigie makofi, Shule ya kutoka kwa Mheshimiwa Gambo hii. (*Makofi*)

Wageni wetu wote kwa ujumla wenu karibuni sana. Tunaamini mmepata fursa ya kujifunsa mawili matatu kutoka hapa Bungeni, lakini pia mmeona namna Wabunge wenu wanavyowawakilisha; na hapa mpo wageni wa Wabunge wengine ambaa hawajapata fursa ya kuzungumza leo, lakini mmewaona hapa wakitia bidii ya kusimama ili wapate nafasi. Wanawawakilisha vizuri sana Wabunge wenu, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Kampuni ya Simu ya *VODACOM* ipo kwenye viwanja vyta Bunge ili kutoa huduma mbalimbali zinazotolewa na kampuni hiyo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa. Sasa hapa wanaokaribishwa kwa mujibu wa hili tangazo ni Wabunge wote, siyo wale tu wanaotumia mtandao wa *VODACOM*. Wabunge wote mnakaribishwa ili mkajue huduma zinazotolewa na kampuni ya *VODACOM*.

Waheshimiwa Wabunge baada ya matangazo hayo, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu!

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI

HOJA ZA KAMATI

Taarifa za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii na Kamati ya Kudumu Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu shughuli za Kamati hizo kwa Mwaka 2021

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama ulivyo utaratibu wetu, nimwite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Ally Makoa, Mwenyekiti mpya kabisa wa Kamati hii, hongera sana Mwenyekiti, karibu uendelee na kazi. (*Makofi/Vigelegele*)

MHE. ALLY JUMA MAKOA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba taarifa hii yote iingizwe kwenye Taarifa Rasmi ya Bunge, *Hansard* kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kuisoma taarifa yangu, naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma ambaye ametujaalia sisi sote neema mbalimbali na kunifanya mimi leo kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kama Mwenyekiti Mpya wa Kamati. Pia nawashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati kwa kuniamini na kunichagua kuwa Mwenyekiti wao. Nawaahidi kazi itaendelea.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kuwalisilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge, Ardhi, Maliasili na Utalii kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza ni utangulizi. Kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa Kipindi cha kuanzia Januari, 2021 hadi Februari, 2022. Taarifa hii imejikita katika kuelezea shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii katika kipindi cha mwaka mmoja wakati ikitekeleza jukumu la kusimamia na kushauri Serikali ambayo ni jukumu lake la kikanuni.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha masharti ya Kifungu cha 7(1) cha nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge yanazingatiwa, Kamati ilipanga na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- (i) Uchambuzi wa Bajeti za Wizara zillizo chini ya Kamati;
- (ii) Ugaguzi wa Miradi ya Maendeleo; na
- (iii) Ziara za ufuatiliaji wa shughuli za Serikali, pamoja na uchambuzi wa Taarifa za utendaji.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu hii, Kamati ilijikita katika kuangalia mafanikio na changamoto kwa kila Sekta. Kamati ilibaini mafanikio na changamoto katika sekta ya ardhi kwa miradi na taasisi zifuatazo:-

- (i) Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi;
- (ii) Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya;
- (iii) Kupanga, kupima na kumilikisha ardhi nchini;
- (iv) Ukusanyaji kodi ya pango la ardhi;
- (v) Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipango Miji; na
- (vi) Bodi ya Usajili ya Wathamini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Miradi ya Upimaji Shirikishi, Urasimishaji wa Makazi Holela na Utatuzi wa Migogoro mbalimbali ya Ardhi katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma; baada ya kupitia taarifa hii ya mradi huu Kamati ilibaini kuwa kulikuwa na mafanikio yafuatayo:-

(i) Halmashauri iliweza kupima 80% ya eneo lote la Jiji na viwanja 335,566 vilipangwa na kupimwa kwa ukamilifu na umilikishaji ulikuwa ni viwanja 104,518; pia mradi uliwezesha Jiji kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mradi huu, Kamati ilibaini kuwa mradi umekumbana na changamoto kubwa ya kuwepo kwa malalamiko kwa baadhi ya wananchi ambapo walipimiwa mashamba yao na makampuni binafsi ambayo hadi sasa hayakuweza kukamilisha zoezi hilo. Pia Kamati iliangalia mafanikio na changamoto ya Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*).

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini mafanikio na changamoto katika sekta ya maliasili na utalii kwa miradi na taasisi zifuatazo: -

Mheshimiwa Spika, moja, ni miradi wa uendelezaji wa maeneo mapya ya kimkakati ya utalii ili kuongeza idadi ya watalii nchini. Zoezi hili limekuwa na manufaa makubwa sana na mafanikio haya ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 katika Ibara ya 66 - 71 iliyolenga kuimarisha utalii nchini ikiwa ni pamoja na kupanua wigo wa mazao ya utalii ili kufikia watalii milioni tano ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, pia Kamati iliangalia Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapor Tanzania (*Tanzania Wildlife Management Authority – TAWA*) na pia Kamati iliangalia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (*Tanzania Forest Services Agency – TFS*).

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana *TFS* yalikuwa ni pamoja na mapato kuongezeka kwa kipindi cha mwaka 2015/2016 hadi 2020/2021 na jumla ya shilingi bilioni 715 zilikusanywa na shilingi bilioni 123.82 ziliwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali na mafanikio mengine yalikuwa ni Wakala kutoa michango mbalimbali katika jamii yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 3.8.

Mheshimiwa Spika, *TFS* inakabiliwa na changamoto za uwanda mdogo wa kusimamia uhifadhi wa misitu Tanzania kwa kuwa *TFS* kisheria inasimamia misitu ya Serikali Kuu peke yake.

Mheshimiwa Spika, Kamati katika taarifa hii, ilibaini kuwa Hifadhi imefanikwa kama ifuatavyo:-

(i) Kuwa Hifadhi bora zaidi Barani Afrika na hifadhi ya pili kwa ubora duniani;

(ii) Kuwa hifadhi inayochangia kiasi kikubwa cha mapato katika Sekta ya Utalii. Kwa mfano, kwa miaka miwili mfululizo, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti imechangia asilimia 47 ya mapato yote yanayokusanywa na *TANAPA* kwenye hifadhi zake; na

(iii) Kupokea tuzo tatu kwa miaka mitatu mfululizo ya Urithi wa Dunia (*World Heritage Site*), na usitiri wa maisha (*Man and Biosphere Reserve - UNESCO*, 1981), Tuzo ya Maajabu Saba ya Asili ya Afrika na Dunia 2006, na Tuzo ya Hifadhi Bora Barani Afrika, 2019, 2020 na 2021.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa iliyoikabili hifadhi hii ni mlipuko wa UVIKO-19 ambao ulipunguza mapato yake kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia iliangalia Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (*TAWIRI*), pamoja na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19.

Mheshimiwa Spika, katika mpango huu, Wizara ya Maliasili na Utalii ilitengewa jumla ya shilingi billioni 90.2 sawa na asilimia 6.9 ya fedha zote kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Taasisi za Wizara *TANAPA*, *TAWA*, *NCAA*, *TFS* na *NTM* zilizothirika zaidi kutokana na mlipuko wa UVIKO, kuimarisha masoko ya utalii na kutangaza, kuimarisha mazingira ya biashara ya utalii kwa kuzingatia viwango vya afya na usalama wa Kitaifa na Kimataifa; kushiriki sekta binafsi kwa kuwajengea uwezo wa kukabiliana na janga la UVIKO-19 na kuimarisha mifumo yo kidijitali ya takwimu za utalii.

Mheshimiwa Spika, mpaka kufikia tarehe 24 Januari, 2022, Wizara ilipokea kiasi cha Shilingi bilioni 59.25, sawa na asilimia 66 ya fedha yote iliyotengwa kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu, ni Maoni na Mapendekezo ya Kamati. Yafuatayo ni maoni ya Kamati kuhusu shughuli zilizotekelizwa katika kipindi cha kuanzia Januari, 2021 hadi Februari, 2022, ambayo yalibainisha mtazamo wa kile kilichojiri wakati Kamati ikitimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mipango mizuri ya sekta bila utekelezaji haiwezi kuleta tija iliyokusudiwa. Kamati imeona bado kuna umuhimu wa Serikali kutenga bajeti ya kutosha kwa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, ili iweze kuratibu kazi ya upangaji na matumizi ya ardhi kote nchini na kutatua migogoro ya ardhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, muundo wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi haukidhi azma ya Serikali ya Awamu ya Sita, katika kuharakisha na kuhakikisha kuwa kila kipande cha ardhi kinapimwa.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa majengo ya watumishi wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya umeathiri uwezo wa kuanzisha mabaraza hayo. Kamati inaona kuna umuhimu kwa Serikali kuongeza majengo na watumishi wa Mabaraza ya Ardhi hususani Wenyevitii, Makatibu Mahsusii wa

kuchapa nakala za hukumu na watunza kumbukumbu, ili kuongeza idadi ya mashauri yanayosikilizwa na baraza.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inaona kuwa Wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi ya Kijiji na ya Kata, wanatakiwa kuwa na weledi wa masuala ya ardhi. Kiasi kidogo na kukosa mkakati wa kupanga, kupima na kusajili kila kipande cha ardhi ili kupunguza migogoro isiyo ya lazima, hususani katika vijiji miji na maeneo yanayokua kwa kasi (*Rapid Emerging Towns*). (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwitikio mdogo wa halmashauri nchini katika kutenga bajeti ili kusaidia zoezi la kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. Wananchi kuwa wazito kutoa maeneo yao wakati wa zoezi la kurasimisha makazi holela mjini, kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kijamii. Mfumo mbovu wa kuyasimamla makampuni binafsi, ambayo yanashirikishwa katika kupanga, kupima na kumilikisha, hali ambayo inapelekeea ucheleweshaji wa kutoa hati, utapeli wa baadhi ya makampuni na baadhi ya wananchi, wamedhulumiwa fedha zao. Kwa sababu, tangu walipe ni muda mrefu hawajaweza kupewa hati zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, zoezi la kupima na kumilikisha ardhi limekuwa likichukua muda mrefu sana kukamilika na wakati mwingine haijulikani muda muafaka wa kukamilika. Kukosekana kwa muda maalum (*time frame*) wa kukamilisha zoezi la kupima na kumilikisha ardhi katika maeneo tofauti, kunachangia migogoro ya ardhi na ujenzi holela wa makazi kunapelekeea kukosesha Serikali mapato. Ukosefu wa miundombinu ya uhakika ya TEHAMA unapunguza ufanisi katika kukusanya mapato ya sekta hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kasi ndogo ya utoaji elimu kwa umma kuitia vyombo vya habari na mikutano ya hadhara, kuhusu umuhimu wa wamiliki wa ardhi kulipa ankara zao kwa wakati, unaathiri utekelezaji wa zoezi la ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa sera ambazo zimepitwa na wakati mfano sera ya ardhi ya mwaka, 1995 na kutokuwepo kwa sera mbalimbali mfano sera ya nyumba (*housing policy*) kunaathiri ukuaji wa sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa mamlaka ya kusimamia sekta ya nyumba (*Real Estate Regulation and Control*) nchini, kumepelekea kuwepo kwa utitiri wa madalali wa nyumba, uholela wa bei za kupanga na hata kuikoseshwa Serikali mapato kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, uratibu usioridhisha wa upimaji wa ardhi katika Serikali za Mitaa unapelekea, uvamizi wa maeneo ya hifadhi za misitu na wanyamapori na kusababisha migogoro ya kisekta.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii; pamoja na Tanzania kubarikiwa na utajiri wa aina mbalimbali za vivutio vya utalii, bado Serikali haijaweka vya kutosha katika kuvitambua, kuviendeleza na kuvitangaza vivutio vyetu vya utalii.

Mheshimiwa Spika, mwenendo usioridhisha wa kuendelea kutegemea zaidi zao moja la utalii ambalo ni utalii wa wanyamapori unasababisha sekta hii, kukua kwa kasi ndogo na kutochangia kikamilifu katika uchumi wa nchi na ustawi wa wananchi wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa kuendeleza maliasili na kukuza utalii katika maeneo ya kipaumbele (*the silent natural resources management for tourism and growth*), unakumbana na changamoto ya kutengewa fedha lakini zinazotolewa kwa ajili ya utekelezaji ni kiasi kidogo ambacho hakiwezi kuleta ufanisi.

Mheshimiwa Spika, ubovu wa miundombinu na vitendea kazi vya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori unazorotesha na kuondoa, *morale* ya watumishi wa Taasisi na hivyo kupunguza kasi ya ufanisi wa tafiti zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mfumo wa matumizi ya ardhi ya Hifadhi ya Ngorongoro uliwekwa vizuri kisheria na kikanuni wakati wa uanzishwaji wake. Hata hivyo, usimamizi hafifu katika utekelezaji wa mfumo huo umeleta changamoto nyingi, ikiwa ni pamoja na uharibifu wa mazingira ya hifadhi. Hali inayotishia kupotea kwa sifa ya urithi wa dunia.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa sera ambazo zimepitwa na wakati mfano, Sera ya Utalii ya mwaka 1999, Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998, Sera ya Malikale ya mwaka 2008 na Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ya mwaka 1998, kunapelekea Wizara kushindwa kuendana na kasi ya mabadiliko ya kidunia.

Mheshimiwa Spika, tatizo la muundo la (*TFS*) kama Wakala wa Misitu limeifanya wakala ishindwe kusimamia sekta ya misitu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, uvamizi wa bonde la Kilombero kwa shughuli za kibinadamu litaendelea kutishia uhai wa uendelevu wa Mradi wa Kufua Umeme wa Mwalimu Nyerere iwapo Serikali haitachukua hatua ya haraka.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango wa maendeleo ya ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19, Kamati inaona kuna umuhimu wa Wizara kuongeza kasi ya utekelezaji ikiwa ni pamoja na kumalizia kusaini mikataba nane iliyosalia.

Mheshimiwa Spika, kuwasilisha maombi ya fedha zilizobaki kila mara baada ya kukamilishwa kwa mikataba, hata kama ni michache na kuendelea kusimamia kwa karibu na kufanya ufuatiliaji wa miradi ambayo imekwishaanza kutekelezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Kamati; kutungwa kwa Sheria ya Uendeshaji wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA):-

KWA KUWA Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania ilianzishwa kwa amri ya kisheria, (*Establishment Order*) na Waziri mwenye dhamana chini ya kifungu cha 8 cha Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na.5 ya mwaka, 2009. Ili kusimamia mapori ya akiba, mapori tengefu, jumuiya za hifadhi za wanyamapori na maeneo ya ardhi oevu ambayo mamlaka hii inasimamiwa na Bodi ya Ushauri badala ya Bodi ya Utendaji;

NA KWA KUWA hali hii inaathiri utendaji wa mamlaka kwa kuwa inakosa nguvu ya kisheria katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

KWA HIYO BASI Bunge linaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Wanyamapori, itakayoainisha bayana majukumu yake na kuanzisha Bodi ya Utendaji itakayoipa nguvu ya kisheria katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Rasilimali ya Misitu Nchini:-

KWA KUWA Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (*TFS*) wamekuwa wakifanya kazi nzuri ya udhibiti wa matumizi ya rasilimali za misitu ya Serikali Kuu peke yake na kuziacha rasilimali zingine za misitu zisizo za kisheria bila udhibiti madhubuti wa matumizi;

NA KWA KUWA changamoto ya udhibiti wa matumizi ya rasilimali za misitu isiyokuwa ya Serikali pamoja na kuleta mgongano, kwenye matumizi ya rasilimali hizo kunachangia kuleta uharibifu na kutishia uendelevu wa misitu yetu;

KWA HIYO BASI Bunge linaishauri Serikali kwamba kwa mara nyingine kuharakisha mchakato wa kuipandisha hadhi Wakala wa Misitu Tanzania (*TFS*) kuwa Mamlaka ya Misitu Tanzania ili kuipa nguvu ya kisheria ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya rasilimali za misitu yote nchini.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro:-

KWA KUWA Serikali imekuwa ikitumia mfumo wa matumizi mseto ya ardhi (*Multiple Land Use System*). Katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa mujibu wa sheria ambao umeiletea sifa Tanzania na kuifanya hifadhi hii kuwa sehemu ya urithi wa dunia;

NA KWA KUWA mfumo huo pamoja na manufaa iliyoiletea nchi, bado umeleta changamoto nyingi, ikiwemo ongezeko la watu na mifugo pamoja na shughuli nyingi za kibinadamu katika hifadhi. Hali hii imesababisha kuongezeka kwa gharama za kuwahudumia wananchi, pamoja na kuwepo kwa uharibifu wa mazingira. Hali inayotishia kupoteza hadhi ya hifadhi hiyo kama eneo la urithi wa dunia; (*Makofii*)

KWA HIYO BASI Bunge linaishauri Serikali kutekeleza mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, moja, Serikali kuharakisha mchakato wa kufanya tathmini ya kina kuhusu mfumo wa matumizi ya ardhi katika eneo hilo, ili kusaidia kufanya marekebisho ya sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ili kuendana na hali halisi iliyopo sasa;

Mheshimiwa Spika, mbili, Serikali itafute namna bora ya kushughulikia changamoto, ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro juu ya wananchi na mifugo ndani ya eneo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazokabili bonde la Kilombero:

KWA KUWA bonde hili limebainika kuwa linakabiliwa na changamoto kadhaa zinazotokana na matumizi mabaya ya ardhi ya bonde kama vile, uvamizi wa shughuli za kibinadamu zisizoendelevu kama vile uvuvi, kilimo, ufugaji pamoja na uanzishwaji wa makazi holela au yaliyorasimishwa isivyo halali;

NA KWA KUWA hali hiyo imeathiri kwa kiwango kikubwa uhifadhi wa bonde na kutishia kupoteza sifa ya kuendelea kuwa moja ya maeneo manne yallyotambuliwa kama yenye ardhi oevu (*RAMSAR site*) kupungua kwa mtiririko wa maji kuelekea Bwawa la Nyerere na hivyo kutishia uendelevu wa mradi wa kufua umeme na mradi wa *SGR* unaotegemea umeme kutoka Bwawa la Nyerere kutoweka au kupungua kwa bioanuai za wanyamapor, misitu na samaki.

KWA HIYO BASI Bunge linaishauri Serikali kutekeleza mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, moja, bonde la Kilombero lipandishwe hadhi kuwa Hifadhi ya Taifa ili liwezeshe eneo hili, kuhifadhiwa vyema na kulinda mazingira yasiendelee kuharibiwa na shughuli za kijamili na kiuchumi zinazoendelea;

Mheshimiwa Spika, mbili, kuimarisha ulinzi wa bonde kwa kutumia Jeshi Usu pamoja na kuwashirikisha wananchi katika shughuli za uhifadhi, wa bonde na kuwaelimisha wananchi wanaozunguka hifadhi ya bonde kuhusu umuhimu wa kulinda na kuhifadhi bonde hilo;

Mheshimiwa Spika, tatu, wananchi wote wanaofanya shughuli za kibinadamu zinazoleta athari, kwenye bonde la Kilombero waondolewe ili kunusuru na kuhifadhi bonde hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulijengea uwezo Shirika la Hifadhi ya Taifa (*TANAPA*):-

KWA KUWA idadi ya Hifadhi za Taifa zimeongezeka kutoka hifadhi 16 hadi 22 ambapo hata kabla ya kuanzishwa kwa hifadhi mpya sita, hifadhi tano kati ya 16 zilikuwa zina uwezo wa kujientesha zenyewe na kuzalisha ziada iliyosaidia kuendesha hifadhi zingine 11;

NA KWA KUWA Shirika linalipa kodi zote stahiki ikiwa ni pamoja na gawio kwa Serikali ambapo fedha hizo zingeweza

kutumika kuzilea na kuzikuza hifadhi ambazo hazijaweza kujitegemea.

KWA HIYO BASI Bunge linaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kulipunguzia au kuliondolea baadhi ya tozo kwa muda maalum ili kuliongezea Shirika nguvu ya kuweza kuhudumia Hifadhi za Taifa kwa ufanisi na kuziwezesha hifadhi zote kuijendesha kwa mapato yake.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa ya *Morocco Square, Seven Eleven* Kawe, *Golden Premier Residents* – Kawe na *Plot 300 Regent Estate* - Mikocheni iliyopo Dar es Salaam:-

KWA KUWA kwa muda mrefu sana miradi tajwa hapo juu imesimama tangu ujenzi wake ulipoanza mwaka, 2012 na 2013 kwa fedha za mkopo ambapo miradi hiyo illitarajiwa kukamilika mwaka 2015 na 2016;

NA KWA KUWA kutokamilika kwa miradi hiyo kwa wakati kumeongeza gharama za ujenzi, ongezeko la riba na Serikali kupata hasara kubwa, ambapo inasababisha kutopatikana kwa thamani halisi ya fedha iliyowekezwa;

KWA HIYO BASI Bunge linaishauri Serikali kuchukua hatua stahiki na kwa wakati, ili kuwezesha *National Housing Corporation* kukamilisha miradi hiyo ili tija ya uwekezaji huo ionekane. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mkakati endelevu wa upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi nchini:-

KWA KUWA programu ya upimaji, upangaji na umilikishaji wa ardhi ulikuwa unatekelezwa kwa majaribio katika Wilaya ya Kilombero, Malinyi na Ulanga kwa kutumia fedha za wafadhili, imekamilika kwa mafanikio makubwa ambapo illitarajiwa kusambazwa katika wilaya nyingine za Mkoa wa Morogoro na nchi kwa ujumla;

NA KWA KUWA Serikali haijatenga fedha ya kutosha za ndani kwa ajili ya kuendeleza *program* hiyo ambayo imeonyesha muelekeo wa kufanikisha, kupunguza kwa kiasi kikubwa migogoro ya ardhi nchini, kutotenga fedha za kutosha kunaathiri ufanisi wa *program* hii;

KWA HIYO BASI Bunge linaishauri Serikali kuhakikisha inatenga fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya kuendeleza *program* hii na *program* nyininge ambazo zinaonyesha mafanikio makubwa katika kuondoa migogoro ya ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, changamoto za upangaji, upimaji na umilikaji ardhi Dodoma:-

KWA KUWA zoezi la upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi katika Jiji la Dodoma limekumbana na changamoto kadhaa za malalamiko ya ukosefu wa maadili kutoka kwa watumishi wa halmashauri, kuwepo kwa makampuni ya kupima yenye utapeli, ukosefu wa elimu kwa wananchi na mgongano wa kimaslahi;

NA KWA KUWA changamoto hizo zimekuwa zikikwamisha na kupunguza kasi ya upimaji wa ardhi, ambapo unaikosesha Serikali mapato yatokanayo na gharama za upimaji na kuwanyima wananchi wa makundi tofauti haki za kumiliki ardhi kisheria;

KWA HIYO BASI Bunge linaishauri Serikali kutekeleza mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, moja, Bodi ya Mabaraza yanayoshughulika na usajili na nidhamu za watumishi wa sekta ya ardhi, ijielekeze zaidi katika kudhibiti maadili ili kurejesha imani kwa wananchi na taasisi zinazohudumiwa na wataalam hawa;

Mheshimiwa Spika, mbili, kuweka mkakati wa kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi kabla ya kipindi cha zoezi la

upimaji na umilikishaji ili kuondokana na migogoro isiyokuwa ya lazima;

Mheshimiwa Spika, tatu, Makampuni yote ambayo yalipewa kazi ya kurasi misha makazi katika Jiji la Dodoma na hayajakamilisha, kazi hiyo kwa zaidi ya mwaka mmoja yatimize wajibu wao kisheria.

Mheshimiwa Spika, kuhuisha sera mbalimbali zilizopitwa na wakati:-

KWA KUWA sera nyingi katika sekta ya ardhi na ile ya maliasili na utalii zimepitwa na wakati. Kwa mfano, sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999, Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ya mwaka 1998;

NA KWA KUWA kupitwa huko na wakati kunasababisha ugumu katika kutekeleza baadhi ya mambo ambayo yanatekelezwa kulingana na mabadiliko ya wakati na mazingira. Sera ya Malikale ya mwaka 2008, sera ya Taifa ya ufugaji nyuki na sera ya ardhi ya mwaka 1995;

KWA HIYO BASI Bunge linaishauri Serikali kuhakikisha mchakato wa kuzihuisha sera zilizopitwa na wakati, ili kuwezesha utekelezaji wake kuwa na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kuanzisha Mfuko wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha:-

KWA KUWA *program* ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi nchini imeonyesha mafanikio makubwa, baada ya kufanikiwa kukamilisha vipande vingi vya ardhi nchini na kupelekea kuondoa migogoro ya ardhi kwenye maeneo yaliyomilikishwa;

NA KWA KUWA bado kuna maeneo mengi nchini yanayohitaji kufikiwa na *program* hii, ili kumaliza kabisa changamoto zilizotokana na vipande vya ardhi ambavyo havijapimwa nchini;

KWA HIYO BASI Bunge linaishauri Serikali kuanzisha Mfuko wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha kama ulivyo Mfuko wa Maji ambapo, Mfuko huu utatumika kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kusimamia Sekta ya Nyumba nchini *Real Estate Regulatory Authority (RERA)*:-

KWA KUWA nchi yetu haina mamlaka inayosimamia sekta ya nyumba limekuwa ni tatizo la muda mrefu;

NA KWA KUWA, kukosekana kwa Mamlaka ya kusimamia Sekta ya Nyumba (*Real Estate Regulation and Control*) nchini, kumepelekea kuwepo kwa utitiri wa madalali wa nyumba, uholela wa bei za kupanga na hata kuikosesha mapato Serikali kwa kiasi kikubwa;

KWA HIYO BASI, Bunge linashauri kwamba, Serikali iharakishe mchakato wa kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Sekta ya Nyumba ili kuwepo na chombo madhubuti kinachosimamia sekta ya nyumba nchini.

Mheshimiwa Spika, hitimisho na kufunga hoja; mafanikio ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii katika kutekeleza shughuli zake kwa kipindi cha Februari, 2021 hadi Januari, 2022 yametokana na juhud, weledi pamoja na umahiri mkubwa wa Wajumbe katika kushiriki na kutoa maoni yenye tija wakati wote ambapo Kamati imekuwa ikiisimamia Serikali.

Mheshimwia Spika, ni wazi kwamba, ufanisi wa utendaji wa Kamati hii unatokana zaidi na Ofisi yako kuwajengea uwezo Wabunge na kuwapa msaada stahiki wa kitaalam na kiushauri wakati wote.

Kwa heshima kubwa, napenda kuwataja majina yao. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda, naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuipatia Wizara ya Maliasili na Utalii Shilingi Bilioni 90.2 ambazo ni fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19 ambazo zinalenga kuchochaea ukuaji wa sekta ya utalii. Aidha, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua yake kama Mkuu wa Nchi kuwa mstari wa mbele kuhamasisha utalii kupitia *royal tour* ambayo imechangia kuongeza idadi ya watalii nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa namna ya kipekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru; Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Dkt. Angelina S. Mabula, Mbunge; na Naibu wake Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Mbunge; Waziri wa Maliasili na Utalii Mheshimiwa Dkt. Damas D. Ndumbaro, Mbunge; na Naibu Waziri, Mheshimiwa Mary F. Masanja, Mbunge; pamoja na watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote ambacho Kamati ilikuwa ikitekeleza majukumu yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, namshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, ndc., kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo wakati wote. Vilevile, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, akisaidiwa na Wakurugenzi Wasaidizi; Ndugu Dickson M. Bisile na Ndugu Gerald S. Magili, bila kuwasahau Makatibu walioandaa taarifa hii akiwemo, Ndugu Ramadhan Abdallah, Ndugu Monica Mwamunyange, Ndugu Elieka Saanya na Ndugu Rehema Kipera pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndugu Mwimbe John.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza shughuli zilizoteklezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji shughuli hizo na pia maoni na mapendekezo ya Kamati, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa

lipokee, kujadili na hatimaye kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU
YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII KWA KIPINDI
CHA JANUARI 2021 HADI FEBRUARI, 2022 SEHEMU
YA KWANZA – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 MAELEZO YA JUMLA
1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa Kipindi cha Kuanzia Januari, 2021 hadi Februari, 2022. Taarifa hii imejikita katika kuelezea shughuli mbalimbali zilizotekelawa na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii katika kipindi cha mwaka mmoja wakati ikitekeleza majukumu ya kuisimamia na kuishauri Serikali ambayo ni majukumu yake ya kikanuni.

1.2 Muundo wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, taarifa hii imeundwa na sehemu kuu nne kama ifuatavyo: -

- i) Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla ikiwemo msingi wa shughuli za Kamati, mbinu na njia zilizotumika pamoja na orodha ya shughuli zilizotekelawa kwa kipindi cha mwaka mmoja;
- ii) Sehemu ya pili inafafanua shughuli zilizotekelawa na uchambuzi wa yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto zilizojitokeza;
- iii) Sehemu ya tatu inatoa maoni ya jumla na mapendekezo ili kuliwezesha bunge kufanya maamuzi, na

iv) Sehemu ya nne inatoa hitimisho na hoja kwa ajili ya bunge kuweza kujadili na kufanya maamuzi.

1.3 Msingi wa Utekelezaji wa Shughuli za Kamati

Mheshimiwa Spika, msingi wa utekelezaji wa shughuli za Kamati unatokana na Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ambayo inaeleza kuwa lengo kuu la Serikali ni ustawi wa wananchi wake. Kamati imepewa jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ina wajibu wa kufanya masuala yafuatayo kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge:-

- a) Kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia;
- b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge ilio chini ya Wizara inazozisimamia;
- c) Kushughulikia taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na
- d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022, Kamati ilitekeleza shughuli zifuatazo: -

- i) Kujifunza muundo na majukumu ya Wizara inazozisimamia pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara hizo kwa lengo la kujelimisha na kupata uelewa wa majukumu yanayofanywa na Wizara husika;
- ii) Kujadili taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara inazozisimamia kwa kipindi cha nusu mwaka (Julai – Disemba, 2021) kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa bajeti;

- iii) Kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo chini ya Wizara inazozisimamia iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2020/2021; na
- iv) Kuchambua utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2020/2021 na makadirio ya Bajeti ya mwaka 2021/2022 za Wizara inazozisimamia

1.4 Njia na Mbinu Zilizotumika

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutekeleza majukumu ya Kamati kwa kiasi kikubwa umezingatia **Kanuni ya 136(3)(4) na (5)** ambazo kwa pamoja zinaweka masharti kwamba, Kamati itatekeleza majukumu yake kwa idhini ya Spika na kwa kuzingatia bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka husika. Aidha, **Kanuni ya 142** ya Kanuni za Bunge inataka kubainisha njia au mbinu zilizotumika. Njia kuu zilizotumika na Kamati katika kutekeleza majukumu yake ni zifuatazo: -

- i) Kufanya vikao na Wizara inazozisimamia kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo na taasisi zake;
- ii) Kufanya ziara kwa lengo la kujiona utekelezaji wa shughuli mbalimbali zinazotekelawa na Wizara na taasisi zake na kuzilinganisha na taarifa iliyochambuliwa na Kamati;
- iii) Kufanya uchambuzi wa taarifa mbalimbali, ikiwemo taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa Mwaka 2020/2021 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;
- iv) Kushiriki mafunzo, semina na warsha mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na Wizara, Mashirika ya Umma, Taasisi Binhafi, Asasi za Kiraia na wadau wengine katika Sekta zinazosimamiwa na Kamati hii; na
- v) Kufanya majumuisho ya mambo yaliyobainika kwenye vikao wakati wa majadiliano ili kuorodhesha mambo makuu ya kutolewa maoni na ushauri.

Mheshimiwa Spika, lengo la kutumia mbinu hizi tofauti ni kuwawezesha wajumbe wa Kamati kujielimisha kwa kiwango cha kutosha katika nyanja ambazo wanawajibika kuzisimamia na kuishauri serikali.

SEHEMU YA PILI

2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA UCHAMBUZI WA YALIYOBAINIKA

2.1 Maelezo ya Shughuli

Mheshimiwa Spika, Kamati hii inasimamia shughuli za Umma zinazotekelvezwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii ambapo inasimamia sekta kuu zifuatazo: -

(a) Sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

(b) Sekta ya Maliasili na Utalii

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha masharti ya Kifungu cha 7(1) cha nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge yanazingatiwa, Kamati ilipanga na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

2.1.1 Uchambuzi wa Bajeti za Wizara zilizo chini ya Kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitekeleza jukumu hili la kuchambua na kupitia bajeti za Wizara zote mbili na taasisi zake ambapo ni takwa la kikanuni na taarifa ya maoni na ushauri wa Kamati iliwasilishwa na kuridhiwa wakati wa vikao vya Mkutano wa Tatu wa Bunge. Aidha, kwa kuwa Bajeti za Wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 bado zipo kwenye mchakato wa utekelezaji wake, ni rai ya Kamati kuwa, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba bajeti iliyoidhinishwa na Bunge inapatikana na kutolewa kwa wakati.

2.1.2 **Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo**

Mheshimiwa Spika, Tarehe 12 - 17 Machi, 2021, Kamati ilitembelea na kukagua miradi iliyotekelizwa na wizara hizi pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Tolea la Juni, 2020. Miradi hiyo ni: -

- (i) Mradi wa REGROW katika Hifadhi ya Taifa Ruaha - **Mradi Na.5203**;
- (ii) Private Plantation and Value Chain -Mafinga - **Mradi Na. 4647**;
- (iii) Mradi wa Shamba la Miti Saohill;
- (iv) Kupanga, kupima na kumilikisha Ardhi Mbeya - **Mradi Na. 2326**;
- (v) Uimarishaji Mipaka ya kimataifa Tunduma - **Mradi Na 2324**; na
- (vi) Mradi wa NHC Momba.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kwamba ufanisi katika utekelezaji wa miradi hiyo utasaidia kuleta ustawi wa wananchi na kuboresha maisha ya Watanzania ambapo jambo hili linaendana na lengo kuu la Serikali la kustawisha maisha ya wananchi sawa na Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka, 1977. Kwa ujumla miradi hiyo ikitekelezwa kwa ufanisi: -

- (i) itaondoa au kupunguza kwa kiwango kikubwa migogoro ya ardhi inayotokana na sababu mbalimbali na kuwezesha makundi mbalimbali ya watumiaji wa ardhi kumiliki ardhi kihalali;
- (ii) Itaboresha ustawi wa wananchi kwa kuwamilikisha ardhi kihalali na kuongeza pato la serikali kuititia kodi za ardhi na majengo;

- (iii) itapunguza uharibifu na hasara zinazosababishwa na muingiliano wa wananchi na wanyamaporu katika maeneo ya hifadhi;
- (iv) itaboresha miundombinu ya utalii na kuvutia idadi kubwa ya watalii kuja nchini na kuongeza fedha za kigeni na ustawi wa wanachi;

2.1.3 Ziara za Ufuatiliaji wa Shughuli za Serikali

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 7(1) (d) pamoja na kifungu cha 6 (6) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea mikoa miwili Ambayo ni Morogoro na Arusha. Ziara hizo ziliwezesha Kamati kufanya ufuatiliaji wa mambo yafuatayo:

- (i) Hifadhi ya Ngorongoro - Arusha kufuatilia hali ya hifadhi na changamoto zinazotokana na shughuli za binadamu zinazoendelea ndani ya hifadhi;
- (ii) Uhifadhi wa Bonde la Kilombero - kuona maendeleo ya Bonde hili ambalo pia ni chanzo kikubwa cha maji ya kuzalisha umeme kwenye Mradi wa Umeme wa Mwalimu Nyerere pamoja na changamoto zitokanazo na shughuli za binadamu ndani ya Bonde; na
- (iii) Hifadhi ya Taifa ya Nyerere- kufuatilia vyanzo vya mito inayotiririsha maji kuelekea Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere.

2.1.4 Uchambuzi wa Taarifa za Utendaji

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Januari, 2021 hadi Februari, 2022, Kamati ilipokea na kujadili taarifa mbalimbali za taasisi 13 ambapo taasisi 5 ni za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na taasisi 8 ni za Wizara ya Maliasili na Utalii. Lengo la kupokea na kujadili Taarifa hizi ni kuiwezesha Kamati kulisaidia Bunge kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo imelipa Bunge mamlaka ya kuisimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sehemu hii ya Taarifa inalenga kuonesha uchambuzi wa kina wa yaliyojitokeza katika uchambuzi ambapo matokeo ya uchambuzi yanajumuisha mafanikio na changamoto kwa kila sekta kama ifuatavyo: -

2.1.4.1 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Ardhi

Mheshimiwa Spika, ardhi ni sekta muhimu katika kustawisha maisha ya wananchi ambapo ikiboreshwu itapunguza migogoro ya ardhi kwa kiasi kikubwa. Aidha, sekta inachochea ukuaji wa uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. Kamati imebaini mafanikio na changamoto katika sekta ya ardhi kwa miradi na taasisi zifuatazo: -

(i) Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa tume hii pamoja na mafanikio mengine, ilipata mafanikio makubwa yafuatayo:-

(i) Tume imewezesha upimaji na uandaaji wa Hati miliki za Kimila 21,790 katika vijiji 42 vilivypo Kondoa, Mvomero, Uvinza, urambo, Magu, Mkalamu, Nzega, Kibondo, Korogwe, Muheza, Monduli, Babati, Bunda na Tarime;

(ii) Katika kipindi cha miaka sita 2015-2021 Tume imewezesha utatuzi wa migogoro ya mipaka katika vijiji 124 vinavyopakana na hifadhi ya Serengeti pamoja na Hifadhi za Taifa za Misitu;

(iii) Imefanikiwa kupima maeneo mengi na kutatua migogoro mingi ya mipaka ya vijiji vinavyopakana na hifadhi za Taifa; na

(iv) Imewawezesha wananchi wengi kumiliki ardhi kihalali na kuongeza pato la serikali kuitia kodi za upimaji na umilikishaji ardhi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Kamati imebaini kuwa bado Tume inakumbana na changamoto zifuatazo: -

- (i) ufinyu wa bajeti na hivyo kushindwa kufika maeneo mengi ambayo bado yana migogoro ya ardhi, na
- (ii) Muundo wa Tume hauwezeshi kutekelezaji majukumu yake kwa ufanisi kwa kuwa ina Bodi ya Ushauri badala ya Bodi wa Wakurugenzi

(ii) Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Chombo hiki kinaanza katika Baraza la Ardhi la Kijiji, Kata na Wilaya. Kamati imebaini mafanikio yafuatayo kwenye chombo hiki: -

(i) Baada ya Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kuanza kutoa huduma, migogoro mingi imetatuliwa ambapo kati ya mwaka 2004 hadi Disemba, 2020 jumla ya **mashauri 188,470** yamefunguliwa na kati ya hayo mashauri **164,196** yameamuliwa

(ii) Wizara imeandaa Muongozo wa Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi na Kanuni za Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya zilizotafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na kusambazwa kwa lengo la kutoa elimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na kuanzishwa kwa mabaraza haya, mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya yanakumbana na changamoto zifuatazo: -

- (i) Uhaba wa majengo na watumishi (Wenyeviti wa Mabaraza, Makatibu Mahsusini wa kuchapa nakala za hukumu na Watunza Kumbukumbu). Hali hii inaathiri uwezo wa kuanzisha Baraza kila mwaka.
- (ii) Ongezeko la mashauri kutokana na wananchi kuelewa umuhimu wa rasilimali ardhi na hivyo kutokuwa tayari kupoteza ardhi zao ambapo mabaraza yaliyopo yanazidiwa na uwingi wa mashauri.

(iii) Mkanganyiko wa kimuundo wa mabaraza ya ardhi ya kijiji na kata ambayo yapo chini ya TAMISEMI hali inayopelekea kushindwa kupata usimamizi stahiki wa kisekta.

(iii) Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipojadili taarifa za utekelezaji wa programu hii ilibaini mafanikio yafuatayo: -

(i) Kupanga na kupima jumla ya vipande vya ardhi **87,636** katika Halmashauri **24** ambapo Magu DC (**4,017**), Misungwi DC (**408**), Sengerema DC (**2,869**), Morogoro Manispaa (**971**), Sumbawanga Manispaa (**2,722**), Shinyanga DC (**1,121**), Babati TC (**2,623**), Geita DC (**1,549**), Tunduma TC (**7,722**), Songwe DC (**652**), Masasi TC (**500**), Mtwara DC (**1,109**), Chamwino DC (**3,989**), Dodoma CC (**131**), Tabora Manispaa (**905**), Rufiji DC (**1,325**), Busega DC (**1,024**), Mbeya Jiji (**709**), Musoma Manispaa (**354**), Arusha Jiji (**19,990**), Jiji la Dar es Salaam (**30,140**), Lindi DC (**2,057**) na Mpanda Manispaa (**749**).

Mheshimiwa Spika, Katika utekelezaji wa Programu hii, Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali kama vile: -

(i) Baadhi ya wananchi kutokuwa tayari kuachia sehemu ya maeneo wanayomilliki kwa ajili ya miundombinu ya barabara na huduma nyingine za kijamii,

(ii) Mwamko mdogo wa wananchi kuchangia ghamrama za upangaji na upimaji ardhi, na

(iii) Baadhi ya halmashauri kutokutenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya kuwezesha shughuli za upangaji, upimaji na umilikishaji.

(iv) Ukusanyaji Kodi ya Pango la Ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya mradi huu, Kamati imebaini mafanikio yafuatayo: -

i. Juhudi za Wizara za kujivekea mikakati na kuisimamia kumeleta ufanisi na kuongeza makusanyo kutoka **shilingi bilion 17** mwaka wa fedha 2011/12 hadi **shilingi bilion 121** kwa mwaka 2020/21 na kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/22 **shilingi bilioni 35.3** zilikusanya.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza mafanikio haya na kuitaka serikali kuendelea kusimamia utekelezaji wa mikakati iliyojiwekea ili kuweza kufikia na hata kuvuka malengo iliyojiwekea.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, bado zipo changamoto zinazosababisha kutokufikiwa kwa malengo ya ukusanyaji maduhuli yanayohusiana na sekta ya ardhi ambapo Kamati ilibaini changamoto zifuatazo: -

(i) Baadhi ya Mashirika na Taasisi za Serikali kuwa na malimbikizo makubwa ya madeni ya kodi ya pango la ardhi,

(ii) Uhaba wa watumishi wa kada za ardhi katika baadhi ya Halmashauri pamoja na upungufu wa vitendea kazi kama vile magari kwa ajili ya kusaidia zoezi la ufuatiliaji wa walipa kodi.

(iii) Kuyumba kwa mawasiliano ya kimtandao (Internet) katika baadhi ya vituo vya makusanyo hususani Halmashauri,

(iv) Kasi ndogo ya wananchi kulipia ankara za umilikishwaji walizopatiwa baada ya maeneo yao kupimwa kuititia njia za urasimishaji au upimaji shirkishi,

(v) Baadhi ya Taasisi na Mashirika yasiyozaalisha faida kuacha kulipia maeneo yao yote bila ya kuzingatia taratibu za msamaha wa kodi uliotolewa kuititia Gazeti la Serikali (GN) 347 la mwaka 2019, na

(vi) Athari za UVICO 19 katika uchumi ambazo zimesababisha baadhi ya wamiliki wa ardhi wakiwemo wawekezaji kushindwa kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati.

(v) Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, katika kipindi cha Aprili 2016 hadi Oktoba 2021 Bodi imeonesha mafanikio yafuatayo: -

- i. Kusajili Wataalam wa Mipangomiji **178** na kufikisha jumla ya Wataalam **428** waliosajiliwa na Bodi, na
- ii. Kusajili kampuni za upangaji ardhi kutoka kampuni **tatu (3)** mwaka 2010 na kufikisha jumla ya kampuni **89** ambapo kati ya hizo kampuni zilizo hai ni kampuni **80**. Kiasi hiki ni sawa na **asilimia 171** ya lengo la usajili kwa Wataalam na **asilimia 178** kwa lengo la kampuni kwa mujibu wa Mpango Mkakati wa Bodi 2015/16 – 2019/20.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Bodi inakumbana na changamoto kadhaa katika utekelezaji wa majukumu yake ambapo: -

- i. Mgawanyo wa majukumu unaotumika ambao uliidhinishwa mwaka 2015, utekelezaji wake haujaanza kikamilifu kutokana na uhaba wa rasilimali watu katika Bodi;
- ii. Muundo wa Kiutumishi kupitwa na wakati kwa hivyo kutokidhi kada zote za kitaaluma ambapo Bodi imeshaufanya maboresho ambayo yameshawasilishwa kwa Msajili wa Hazina kwa hatua stahiki; na
- iii. Uhaba wa fedha hususani za kujenga mifumo ya kielektroniki ya usajili wa Maafisa Mipangomiji.

(vi) Bodi ya Usajili wa Wathamini.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Usajili wa Wathamini ni taasisi ya umma iliyoanzishwa mwaka 2018 kwa Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini ya Mwaka 2016 **Sura ya 138** kwa ajili ya kusajili wathamini na kudhibiti kazi za uthamini nchini. Majumuku ya Bodi ni usajili wa wathamini ambapo katika usajili Bodi inafanya aina nne za usajili, Usajili Kamili (*Fully*

Registration), Usajili wa muda (temporary Registration), Usajili wa awali (provisional Registration), Uorodhesaji na Utambuzi wa Wathamini wasaidizi (Technician Valuers), Usajili wa Kampuni za Uthamini (Valuation Consulting Firms) na kutoa Mafunzo endelevu kwa wathamini, usimamizi wa Nidhamu na Maadili kwa Wathamini na Upimaji wa elimu na uzoefu wa wathamini kwa ajili ya kuwasajili.

Mheshimiwa Spika, Kamati baada ya kupokea na kuchambua taarifa za Bodi hii ilibaini mafanikio yafuatayo: -

- i. kusajili Wathamini **117** kwa Usajili Kamili, kusajili Wathamini **725** kwa Usajili wa Awali;
- ii. Kuwatambua na kuorodhesha Wasajili Wasaidizi **45** na kusajili Kampuni za Uthamini **50**;
- iii. Kuandaa Viwango vya Kazi za Uthamini (*Valuation Standards*) na Mwongozo wa Uthamini (*Valuation Guideline*); na
- iv. Kukagua na kurekebisha mitaala ya Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo cha Ardhi Tabora, na Chuo cha Ardhi Morogoro kwa kushirikiana na Kamisheni ya Elimu ya Juu Tanzania (*Tanzania Commission for Universities*) na Baraza la Taifa la Ufundsi (National Council for Technical Education).

Mheshimiwa spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Bodi inakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo: -

- i. Uhaba wa watumishi na Uhaba wa rasilimali fedha kwa ajili ya ujenzi na usimikaji wa mifumo ya kielektroniki ya usajili wa wathamini nchini;
- ii. Bodi kutojielekeza katika kudhibiti wathamini na Kampuni za uthamini zinazokiuka maadili na hivyo kusababisha kulalamikiwa, na
- iii. Kasi ndogo ya kusajili wathamini kwenye kiwango cha Usajili Kamili (Fully Registration).

(vii) **Miradi ya Upimaji Shirikishi, Urasimishaji wa Makazi Holela na Utatuzi wa Migogoro mbalimbali ya Ardhi katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma.**

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwa pamoja na Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa ilipokea taarifa kuhusu utekelezaji wa miradi ya upimaji shirikishi, urasimishaji na utatuzi wa migogoro mbalimbali ya Ardhi iliyotekelze wa katika Halmashauri ya jiji la Dodoma. Yafuatayo ni mafanikio yaliyobainika: -

- (i) Halmashauri imefanikiwa kutekeleza upangaji na upimaji kwa **asilimia 80%** ya eneo lote la Jiji la Dodoma;
- (ii) Imeboresha makazi yaliyokuwa holela katika Jiji la Dodoma;
- (iii) Jumla ya **viwanja 335,566** vimepangwa na kupimwa na umilikishaji umekamilika kwa **viwanja 104,518** ambavyo vimechangia kuongeza pato la Halmashauri na Serikali Kuu kwa ujumla;
- (iv) Jiji la Dodoma limefanikiwa kushirikisha wananchi katika kuchangia utengaji wa maeneo ya huduma kama shule, barabara, hospital na maeneo ya wazi ambayo ni chachu ya maendeleo katika Mitaa yao;
- (v) Mapato ya Jiji yaliongezeka kutohana na makusanyo yatokanayo na kodi za upangaji, upimaji na umilikishaji; na

- (vi) Wananchi waliokuwa na kipato cha chini wamenufaika kwa ardhi yao kupangwa na kupimwa na kufanikiwa kuinuka kiuchumi kuititia kuuza sehemu ya viwanja walivyonufaika katika mradi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mradi huu, Kamati ilibaini kuwa Mradi umekumbana na changamoto zifuatazo: -

- i. Uelewa mdogo katika masuala ya ardhi ambao umepelekea baadhi ya wananchi kuhisi ukiukwaji wa makubaliano au kuhisi kupoteza haki zao, na hasa kwa wananchi ambao wananaunua maeneo wakati mradi wa upimaji umeshaanza bila kufahamu makubaliano yaliyokuwepo katika mradi kabla ya kuanza upimaji;
- ii. Baadhi ya wananchi wamekuwa wazito kutoa sehemu ya ardhi kwa ajili ya huduma za kijamii baada ya kutamani kumiliki viwanja vingi kwa lengo la kunufaika.
- iii. Kuwepo kwa malalamiko kwa baadhi ya wananchi ambao walipimiwa mashamba yako na Makampuni binafsi ambayo hadi sasa hayajaweza kukamilisha zoezi hili. Jambo hili limeleta hofu kwa wamiliki wa maeneo ambayo bado hayana hati miliki.

(vii) Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa linatekeleza majukumu yake kama yalivyoanishwa kwenye Mpango Mkakatati 2015/2025 kwa kusimamia milki, kufanya kazi za ukandarasi na kujenga majengo ya biashara na nyumba za makazi kwa ajili ya kuza na kupangisha kwa watanzania.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba limefanikiwa:

- i. Utekelezaji wa miradi ya Morocco Square, Seven Eleven – Kawe, Golden Premier Residents – Kawe na Plot 300 regent Estante Mikocheni iliyopo Dar Es salaam
- ii. kutengeneza jumla ya mapato ya **shilingi Bilioni 139.9**. kiwango hiki ni sawa na **asilimia 52** ya lengo la ongezeko la mapato kwa mujibu wa Mpango Mkakati wa Shirika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio ya Shirika hili, bado linakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

- i. Riba kubwa zinazotozwa na benki za biashara nchini, Madeni makubwa ambayo Shirika linadai watu binafsi na Serikali,

ii. Ukosefu wa vifaa vya ujenzi kwa gharama nafuu.

iii. Ucheleweshwaji wa malipo.

2.1.4.2 Mafanikio na Changamoto katika Sekta ya Maliasili na Utalii

Mheshimiwa Spika, Tanzania imekuwa na maendeleo ya hifadhi za wanyamapori, misitu na nyuki; na malikale yenyе mchango mkubwa katika uhifadhi wa mazingira, ustawi wa wananchi na ukuaji wa uchumi. Aidha, maliasili, utalii na maliakale zimeendelea kuchangia katika kuingiza fedha za kigeni na pato la Taifa. Kamati imebaini mafanikio na changamoto katika sekta ya maliasili na utalii kwa miradi na taasisi zifuatazo: -

a. Mradi wa Uendelezaji wa Maeneo Mapya ya Kimkakati ya Utalii ili Kuongeza Idadi ya Watalii Nchini

Mheshimiwa Spika, Mradi huu wa utalii umefanikiwa katika: -

i. Kuchangia **asilimia 25** ya mauzo yote ya nje na **asilimia 60** ya mapato yote yatokanayo na biashara za huduma;

ii. Utalii huzalisha ajira takriban **milioni 1.5** ikiwa ni ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja;

iii. Ukuaji wa sekta hii umekuwa endelevu ambapo takwimu zinaonesha kuwa idadi ya watalii wanaotembelea nchini imekuwa ikiongezeka kutoka watalii 1,137,182 kwa mwaka 2015 hadi kufikia watalii 1,527,230 kwa mwaka 2019;

iv. Mapato yatokanayo na sekta ya utalii yameongezeka kutoka Shilingi triliuni 3.8 (Dola za Marekani bilioni 1.9) mwaka 2015 hadi kufikia Shilingi triliuni 6.06 (Dola za Marekani Bilioni 2.6) mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya ni sehemu ya utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 katika **Ibara** ya 66 -71 inayolenga kuimarisha utalii nchini

ikiwa ni pamoja na kupanua wigo wa mazao ya utalii ili kufikia **watalii milioni 5** ifikapo mwaka 2025 kutoka watalii 1,527,230 mwaka 2019. Aidha, inalenga kuongeza mapato yatokanayo na utalii kutoka **Shilingi trillioni 6.06 (Dola za Marekani bilioni 2.6)** mwaka 2019 hadi Shilingi trillioni 13.58 (**Dola za Marekani bilioni 6.0**) ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, miradi pamoja sekta ndogo ya utalii kwa ujumla zimekumbwa na changamoto ziafuatzo:-

- i. Mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 uliotokea tangu mwishoni mwaka 2019 ambapo umeathiri kwa kiasi kikubwa maendeleo ya sekta ya utalii nchini baada ya nchi nydingi duniani kufunga mipaka yake na kuzuia safari; na
- ii. Sekta ya utalii nchini, inategemea zaidi utalii wa wanyamaporii ambapo idadi kubwa ya watalii wanaotembelea Tanzania huja kuona wanyamaporii.

b. Mradi wa kuendeleza Maliasili na kukuza Utalii katika Maeneo ya Kipaumbele - Tanzania - Resilient Natural Resource Management for Tourism and Growth (Regrow)

Mheshimiwa Spika, mradi huu umeonesha mafanikio yafuatayo:-

- i. kuongeza ubora wa vivutio vya utalii katika ukanda wa kusini mwa Tanzania;
- ii. Usimamizi wa maliasili;
- iii. Kuimarisha na kuendeleza utalii, na
- iv. Kuongeza fursa za kiuchumi kwa wananchi wanaozunguka hifadhi na kuongeza mchango wa sekta ya utalii katika maendeleo ya kiuchumi nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa mradi huu unakabiliwa na changamoto ya mtiririko wa utoaji wa fedha isiyoridhisha inayozorotesha uendelezaji na Usimamizi wa

Mradi huu. Kwa mfano: Jumla ya **Shilingi bilioni 30.6** Kwa mwaka 2018/2019 zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza mradi huu lakini kiasi kilichotolewa na kutumika ni **shilingi bilioni 1.6** sawa na **asilimi 5** tu ya fedha zote, mwaka 2019/2020 mradi ilitengewa kiasi cha **shilingi bilioni 31.2** na fedha zilizotolewa na kutumika ni **shilingi bilioni 3.1** sawa na **asilimia 12** ya fedha iliyotengwa, na mwaka 2020/2021 Mradi ilitengewa kiasi cha **shilingi bilioni 30.5** lakini kiasi kilichotolewa kwa ajili ya mradi ni **shilingi bilioni 4.6** sawa na **asilimia 15** ya fedha iliyotengwa.

c. Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (*Tanzania Wildlife Management Authority*) – TAWA

i. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania ilianzishwa kwa amri ya kisheria (*establishment order*) na Waziri mwenye dhamana chini ya Kifungu cha 8 cha sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009 na kuchukua baadhi ya majukumu ya kiutendaji ya idara ya wanyamapori ambayo ni usimamizi, uangalizi, na uendelezaji wa rasilimali za wanyamapori nje ya hifadhi za taifa na mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro. TAWA imeonesha mafanikio makubwa yafuatayo ambapo kabla ya mlipuko wa UVIKO 19: -

ii. Idadi ya watalii wanaotembelea vivutio vya utalii katika Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu ilikuwa ikiongezekwa kwa kasi kutoka watalii 35,479 kwa kipindi cha mwaka 2015/2016 na kufikia watalii 129,428 kwa kipindi cha mwaka 2018/2019 sawa na **234.7%**. Ongezeko hili la watalii lilitokana na juhudzi za maksudi za serikali kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi; na

iii. Maboresho ya huduma hususani matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika kukusanya maduhuli.

Mheshimiwa Spika, TAWA inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

i. Kutoptaka na athari za mlipuko wa UVIKO 19, idadi ya watalii imepungua kwa **asilimia 62** kufikia watalii 37,684 mwaka 2020/

21 kwa kuwa vyanzo vikuu vya mapato ya TAWA ni Uwindaji wa kitalii na Utalii wa Picha;

ii. Mapato ya Mamlaka yalianza kushuka na kufikia **shilingi bilioni 43.74** na **shilingi bilioni 25.75** Mwaka 2019/20 na 2020/21 mtawalia; na

iii. Muingiliano kati ya wananchi na wanyamapori ambapo kumekuwa na matukio ya wanyama wakali na waharibifu kufanya uharibifu na kuua wananchi ambapo Kati ya mwaka 2016/17-2020/21 kulikuwa na matukio 6,472 ya wanyama wakali na waharibifu katika Wilaya 85 nchini.

d. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania - Tanzania Forest Services Agency (TFS)

Mheshimiwa Spika, Mafanikio yaliyopatikana kwa kuwepo Mamlaka ya Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ni kama ifuatavyo:-

i. Kusimamia, kutunza na kukusanya maduhuli kutoka vyanzo mbalimbali vitokanavyo na mazao ya misitu ambapo mapato ya Wakala yamekuwa yakiongezaka kila mwaka. Katika kipindi cha 2015/16 hadi 2020/21 jumla ya **shilingi bilioni 713** zilikusanywa na **shilingi bilioni 123.82** ziliwasilishwa katika **mfuko Mkuu wa Serikali**;

ii. Kuhamasisha ushiriki wa jamii kwenye shughuli za uhifadhi;

iii. Uzalishaji, usambazaji na upandaji wa miche ya miti; na

iv. Wakala umetoa michango mbalimbali kwa jamii yenye thamani ya zaidi ya **Shilingi bilioni 3.18 ambayo** ilielekezwa katika shughuli mbalimbali za kijamii ikiwemo ujenzi wa shule na mabweni, Ujenzi wa kompyuta maabara na ujenzi wa viwanja vya michezo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio makubwa ambayo TFS imeyapata, bado inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. Uhitaji mkubwa wa mazao ya misitu. Kwa mfano: Utigemezi mkubwa wa misitu kwa ajili ya nishati ya kupikia hususani mkaa na kuni umesababisha uvunaji holela na kwa kiasi kikubwa wa misitu unaozorotesha juhudzi za Wakala, uvunaji wa mbao kwa ajili ya ujenzi wa ndani na biashara ya nje ya nchi, pamoja na kuvamiwa kwa misitu kwa shughuli za kilimo, ufgaji, makazi na uchimbaji haramu wa madini; na

ii. Uwanda mdogo wa kusimamia uhifadhi wa misitu Tanzania kwa kuwa TFS kisheria inasimamia misitu ya Serikali tu.

e. Hifadhi ya Taifa Serengeti kuwa Hifadhi bora Barani Afrika

Mheshimiwa Spika, Kamati katika taarifa hii, ilibani kuwa Hifadhi imefanikwa:-

i. Kuwa Hifadhi bora Zaidi Barani Afrika na hifadhi ya pili kwa Ubora Duniani;

ii. Kuwa hifadhi inayochangia kiasi kikubwa cha mapato katika Sekata ya Utalii. Kwa mfano, kwa miaka 2 mfululizo, Hifadhi ya Taifa Serengeti imechangia **asilimia 47** ya mapato yote yanayokusanya na TANAPA kwenye hifadhi zake; na

iii. Kupokea tuzo tatu kwa miaka mitatu mfululizo ya Urithi wa Dunia (*World Heritage Site*), na Usitiri wa maisha (*Man and Biosphere Reserve*) – UNESCO, 1981, tuzo ya Maajabu 7 ya Asili ya Afrika na Dunia 2006, na tuzo ya Hifadhi Bora Barani Afrika 2019, 2020 na 2021 iliyotolewa na ‘World Travel Awards.

Mheshimiwa Spika, ni imani ya Kamati kuwa sababu zinazofanya Serengeti kuwa hifadhi bora zinaweza kutumika katika hifadhi zingine na kuleta matokea chanya katika kukuza sekta ya utalii wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa iliyoikabili hifadhi hii ni Mlipuko wa UVIKO 19 ambapo ulipunguza mapato yake kwa kiwango kikubwa.

f. Programu ya Kuongeza Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Misitu Kibiashara (Forestry Value Chains Development Programme)

Mheshimiwa Spika, programu ya Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Misitu (FORVAC) imepata mafanikio yafuatayo:-

i. Imeongeza faida za kiuchumi, kijamii na kimazingira kutokana na usimamizi wa misitu kwa kuongeza thamani ya mazao ya misitu na kuimarisha ustawi wa jamii kwa ujumla;

ii. Uandaaji wa Mipango 15 ya Matumizi Bora ya Ardhi katika eneo la Hekta 70,000, Mipango 26 ya Usimamizi wa Misitu imeandaliwa na kupitishwa kwenye ngazi zote;

iii. Utafiti wa aina za miti ambayo haijulikani kwa sasa umefanyika ambapo miti 14 imetambuliwa na kufanyiwa majaribio kwa ajili ya kuingizwa sokoni;

iv. Kuwajengea uwezo wadau na kuanzisha vikundi 51 vya kuweka na kukopa katika kongani za Tanga, Lindi na Ruvuma; na

v. Kuwajengea uwezo vikundi 15 vya ufugaji nyuki kwa mafunzo katika Kongani zote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyofikiwa, Programu hii imekabiliwa na changamoto zifuatazo:-

i. Elimu kuhusu umuhimu wa kupanda miti bado haijawafikia wanachi wengi na hivyo kutofikia lengo la kuongeza thamani ya zao la misitu na kuongeza uchumi wa nchi na ustawi wa wananchi; na

ii. Kasi ya upandaji miti katika miji inayokumbwa na ukame ikiwemo Dodoma, Singida na Shinyanga bado ni ndogo.

g. Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI)

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI) imeonesha mafanikio ya kiuhifadhi yafuatayo:-

- i. Kubainisha shoroba 61 za wanyamapori nchini ambazo inasaidia kupunguza migongano kati ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu. Kwa mfano; kwa mwaka 2021 katika mfumo ikolojia ya Ziwa Natron – West Kilimanjaro imeonekana kuna mwingiliano mkubwa wa mifugo na wanyamapori ambao umeathiri uwepo wa mbogo kwani kwa sasa eneo lina mbogo wasiozidi 50. Taasisi imeendelea kufuatilia mtawanyiko na idadi ya tembo ambapo idadi yake imefikia tembo elfu 52,273 mwaka 2020 pungufu ya tembo 56,756 (56%) toka tembo 109,029 mwaka 2009 nchi nzima. Nyumbu na Pundamilia wahamao kwenye mfumo ikolojia wa Serengeti, ambao kwa sasa wako kwenye eneo la ukomo wa ongezeko la idadi, ambapo nyumbu wahamao wako million 1 na laki 4
- ii. Kushughulikia magonjwa na tiba kwa wanyamapori;
- iii. Kudhibiti milipuko ya ugonjwa wa kimeta (anthrax) nchini, ugonjwa wa kutupa mimba au homa ya vipindi (brucellosis) , Kichaa cha mbwa (Rabies) na kichaa cha simba (Canine Distemper Virus) ni magojwa ya kipaumbele katika kutafiti na kuyadhibiti;
- iv. Ukamataji na uhamishaji wa wanyamapori kwa ajili ya uendelezaji na uanzishwaji wa mashamba ya wanyamapori yanayomilikiwa na serikali na watu binafsi (Game ranches, farms and zoos), kupandikiza katika hifadhi zinazohitaji na pia katika shughuli za utafiti na kukuza utalii nchini;
- v. Kurejesha wanyamapori kwenye maeneo yao ya asili. Ili kukuza na kuendeleza uhifadhi wa faru Weusi na Weupe nchini;
- vi. Kubainisha mbinu za kitaalamu ili kupunguza migongano baina ya binadamu na tembo ambapo hadi kufikia Septemba, 2021 Taasisi imefanya mafunzo kwenye wilaya 17 kati ya 53 zilizoathirika na jumla ya wananchi 400 wamefundishwa na kuwezeshwa vifaa tajwa ili kusambaza elimu hii kwa jamii zao; na

vii. Taasisi imeendelea kutoa ushauri kwa Serikali hasa katika utekelezaji wa miradi mikubwa inayogusa uhifadhi mfano ujenzi wa njia za umeme, Mabwawa ya umeme, Reli na pia ubadilishwaji hadhi na upandishwaji hadhi wa maeneo ya uhifadhi na vitalu nya uwindaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi kubwa inayofanywa na TAWIRI, bado inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- i. Ubovu wa jengo la ofisi za Makao makuu;
- ii. Ukosefu wa vifaa vya utafiti hasa Magari na vifaa vya maabara na ongezeko la hitaji la kufanya tafiti za matukio ya dharura yanayohusu migogoro kati ya wananchi na wanyamapori; na
- iii. Kutokuwa na Bodi ya Utendaji

h. Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya Uviko-19

Mheshimiwa Spika, katika mpango huu, Wizara ya Maliasili na Utalii ilitengewa jumla ya **Shilingi billioni 90.2** sawa na **aslimia 6.9** ya fedha yote kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maeneo makuu matano, ambayo ni kuziwezesha Taasisi za Wizara (TANAPA, TAWA, NCAA, TFS na NMT) zilizoathirika zaidi kutokana na mlipuko wa Uviko-19 kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Kuimarisha masoko na utangazaji utalii, kuimarisha mazingira ya biashara ya utalii kwa kuzingatia viwango vya afya na usalama vya kitaifa na kimataifa, kuimarisha sekta binafsi kwa kuwajengea uwezo wa kukabiliana na janga la UVIKO-19 na kuimarisha mifumo ya kidigitali ya takwimu za utalii. Mpaka kufikia tarehe 24 Januari 2022, Wizara ilipokea kiasi cha **Shilingi 59.25** sawa na **aslimia 66** ya fedha yote iliyoengwa kwa Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza Mpango huo Wizara imefanya Shughuli zifuatazo;

- i. Kuanza kwa kazi ya kihistoria ya Utafiti wa utalii wa ndani (Stand-Alone Domestic Tourism Survey) na Ukokotoaji mchango wa Sekta ya Utalii katika Pato la Taifa ambapo uzinduzi ulifanyika tarehe 15 Januari, 2022 ambao ulizinduliwa na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii;
- ii. Ujenzi na ukarabati wa kilomita 1,552 za barabara, malango matatu (3), viwanja vya ndege vitatu (3) na vituo vya kutua helikopta (Helpads) vitano (5), ununuzi wa mitambo na magari (maloni);
- iii. Ukarabati wa kilomita 263 kati ya kilomita 463 katika maeneo ya mapori ya akiba;
- iv. Ukarabati wa barabara katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro eneo la Golini hadi Njiapanda ya Seneto na Olduvai hadi Nasera Rock;
- v. Kuanza kwa ukarabati wa barabara na njia za kutembea kwa miguu katika maeneo ya misitu ya Magamba, Kalambo, Pugu-Kazi Mzumbwi, Rungwa na Amani;
- vi. Ukarabati wa maeneo na miundombinu ya malikale ya Mikindani, Tendaguru, Jengo la Kihistoria Lindi, magofu ya Kua, Kimbiji na Mbua Maji, makumbusho ya Nyumba ya Utamaduni, Kijiji cha Makumbusho, Azimio la Arusha, Elimu Viumbe, Majimaji na Mwl. Nyerere;
- vii. Mafunzo ya wadau wa utalii 150 kwa kila mkoa kwa mikoa 26 ya Tanzania Bara kuhusu miongozo ya kukabiliana na janga la UVIKO-19, ambapo mafunzo hayo yamezinduliwa rasmi tarehe 29 Januari, 2022 Jijini Dar es Salaam;
- viii. Ushiriki wa Onesho la Dubai Expo 2020 lilihofanyika Dubai na onesho la Fitur lilihofanyika nchini Hispania
- ix. Mafunzo ya kuwajengea uwezo waongoza Watalii 151 nchini yametolewa;

x. Kujenga mfumo wa kufanya Ufuatiliaji na Tathmini (M&E) wa utekelezaji wa Fedha za UVIKO-19 na mfumo wa kufanya tathmini ya huduma za malazi na kuzipanga katika madaraja ya ubora (AserT) pamoja na MNRT Portal umeboreshwa;

xi. Ununuzi wa magari ambapo hadi sasa utaratibu wa ununuzi wa magari 20 kupitia Wakala wa Manunuzi Serikalini (GSPA) unaendelea baada ya fedha za kununulia magari hayo kupelekwa kwenye taasisi husika.

xii. Jumla ya mikataba (120) inayohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa UVIKO - 19 imeandaliwa. Mikataba 112 ambayo ni asilimia 93.3 ya mikataba yote imesainiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na mpango huu, bado unakabiliwa na changamoto zifuatazo;

i. Kukamilisha mikataba kulingana na taratibu za manunuzi;

ii. Baadhi ya zabuni kurudiwa kutangazwa kutokana na ghamama za wazabuni kuwa kubwa kuliko fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi, mathalani jumla ya zabuni tano zimerudiwa kutoka taasisi za TANAPA, TAWA na NCAA; na

iii. Kukosekana kwa manunuzi ya Mitambo yakiwemo magreda, boti, na magari maalumu kutoka GPSA na hivyo kulazimu kuanza utaratibu wa manunuzi wa vifaa hivyo kutoka kwa watengenezaji (dealers).

2.1 Semina kwa Wajumbe wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka mmoja cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati, wajumbe walipata fursa ya kushiriki katika semina mbalimbali ambazo zililenga kuwajengea uwezo kama ifuatavyo: -

a) Semina Kuhusu Mapendekezo ya Kuanzishwa kwa Kanuni za Kuanzisha Mabucha ya Kuuza Nyamapori

Mheshimiwa Spika, Semina hii iliandaliwa na kutolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Kupitia semina hii wajumbe waliweza kupata uelewa wa kutosha kuhusu namna wizara inavyotunga sheria ndogo mamlaka iliyokasimiwa na Bunge lako tukufu kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa katika Katiba ya nchi. Kanuni hizo zinalenga kuweka masharti ambayo yatarahisisha upatikanaji wa nyamapori.

b) Semina kuhusu Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi

Mheshimiwa Spika, semina hii ilitolewa na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa lengo la kuwajengea wajumbe uwezo wa uelewa juu ya mipango ya Tume katika kupanga matumizi ya ardhi nchini. Mipango ya matumizi ya ardhi imeonekana kuwa ni suluhisho la migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali nchini hasa wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mpango huu mzuri na mikakati mingi iliyopo ya kuhakikisha kila kipande cha ardhi nchini kinapangiwa matumizi, kasi ya upangaji matumizi ya ardhi ni ndogo kwani hadi kufikia Mwezi Disemba 2019, takriban vijiji 2,300 katи ya vijiji 12,319 vilivyopo nchini ndivyo vilivyokuwa vimepangiwa matumizi ya ardhi. Kasi hii ni ndogo kulinganisha na ongezeko la migogoro ya ardhi na mahitaji ya watumiaji ardhi.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 Maoni ya Jumla

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni maoni ya Kamati kuhusu shughuli zilizotekelawa katika kipindi cha kuanzia Januari 2021 hadi Februari 2022 ambayo yanabainisha mtazamo wa kile kilichojirisha wakati Kamati ikitimiza majukumu yake. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

- i. Mipango mizuri ya sekta bila utekelezaji haiwezi kuleta tija iliyokusudiwa. Kamati inaona bado kuna umuhimu wa Serikali kutenga bajeti ya kutosha kwa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ili iweze kuratibu kazi ya upangaji wa matumizi ya ardhi kote nchini na kutatua migogoro ya ardhi;
- ii. Muundo wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi haukidhi azma ya serikali ya awamu ya Sita katika kuharakisha na kuhakikisha kuwa kila kipande cha ardhi kinapimwa;
- iii. Uhaba wa majengo na watumishi wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, umeathiri uwezo wa kuanzisha mabaraza hayo kila mwaka. Kamati inaona kuwa kuna umuhimu kwa Serikali kuongeza majengo na watumishi wa mabaraza ya ardhi hususan wenyeviti, makatibu Mahsuswi wa kuchapa nakala za hukumu na watunza kumbukumbu ili kuongeza idadi ya mashauri yanayosikilizwa na baraza. Aidha, Kamati inaona kuwa wajumbe wa mabaraza ya ardhi ya Kijiji na ya Kata wanatakiwa kuwa na weledi wa masuala ya ardhi;
- iv. Kasi ndogo na kukosa mkakati wa kupanga, kupima na kusajili kila kipande cha ardhi ili kupunguza migogoro isiyo ya lazima hususani katika vijiji-miji na maeneo yanayokua kwa kasi (*Rapid emerging Towns*);
- v. Mwitikio mdogo wa halmashauri nchini katika kutenga bajeti ili kusaidia zoezi la kupanga, kupima na kumilikisha
- vi. Wananchi kuwa wazito kutoa maeneo yao wakati wa zoezi la kurasimisha makazi holela mijini kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kijamii;
- vii. Mfumo mbovu wa kuyasimamia makampuni binafsi ambayo yanashirikishwa katika KKK. Hali ambayo imepeleka ucheleweshwaji wa kutoa hati, utapeli wa baadhi ya makampuni na baadhi ya wananchi wamedhulumiwa fedha

zao kwa sababu tangu walipe ni muda mrefu hawajaweza kupewa hati zao;

viii. Zoezi la kupima na Kumilikisha ardhi limekuwa likichukua muda mrefu Sana kukamilika na kuna wakati haijajulikani muda muafaka wa kukamilika. Kukosekana kwa Muda Maalumu (Time frame) wa kukamilisha zoezi la kupima na kumilikisha ardhi katika maeneo tofauti kunachangia migogoro ya ardhi na ujenzi holela wa makazi na kunapelelea kukosesha serikali mapato;

ix. Ukoefu wa miundombinu ya uhakika ya TEHAMA unapunguza ufanisi katika kukusanya mapato ya sekta hii;

x. Kasi ndogo ya utoaji elimu kwa umma kupertia vyombo vya habari na mikutano ya hadhara kuhusu umuhimu wa wamiliki wa ardhi kulipa ankara zao kwa wakati, unaathiri utekelezaji wa zoezi la ukusanyaji wa mapato;

xi. Uwepo wa sera ambazo zimepitwa na wakati mfano Sera ya Ardhi ya mwaka, 1995 na kutokuwepo kwa sera mbalimbali mfano Sera ya Nyumba (Housing Policy) kunaathiri ukuaji wa sekta ya ardhi;

xii. Kukosekana kwa Mamlaka ya kusimamia sekta ya Nyumba (Real Estate Regulation and Control) nchini kumepelekea kuwepo kwa utitiri wa madalali wa nyumba, uholela wa bei za kupanga na hata kuikosesha mapato serikali kwa kiasi kikubwa; na

xiii. Uratibu usioridhisha wa upimaji wa ardhi katika serikali za mitaa umepelekea uvamizi wa maeneo ya hifadhi za misitu na wanyamapor na kusababisha migogoro ya kisekta.

3.1.1 Wizara ya Maliasili na Utalii

i. Pamoja na Tanzania kubarikiwa na utajiri wa aina mbalimbali za vivutio vya utalii, bado serikali haijawekeza vya kutosha katika kuvitambua, kuviendeleza na kuvitangaza vivutio vyetu vya utalii;

- ii. Mwenendo usioridhisha wa kuendelea kutegemea zaidi zao moja la utalii ambalo ni Utalii wa Wanyama Pori kunasababisha sekta hii kukua kwa kasi ndogo na kutochangia kikamilifu katika uchumi wa nchi na ustawi wa wananchi wake;
- iii. Mradi wa kuendeleza Maliasili na kukuza Utalii katika Maeneo ya Kipaumbele (*Resilient Natural Resource Management for Tourism and Growth*) unakumbana na changamoto ya kutengewa fedha lakini zinazotolewa kwa ajili ya utekelezaji ni kiasi kidogo ambacho hakiwezi kuleta ufanisi;
- iv. Ubovu wa miundombinu na vitendea kazi vya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori unazorotesha na kuondoa morali za watumishi wa taasisi na hivyo kupunguza kasi na ufanisi wa tafiti hizo;
- v. Mfumo wa matumizi ya ardhi ya Hifadhi ya Ngorongoro uliwekwa vizuri kisheria na kikanuni wakati wa uanzishwaji wake. Hata hivyo, usimamizi hafifu katika utekelezaji wa mfumo huo umeleta changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na kuharibu mazingira ya hifadhi hali inayotishia kupotea kwa sifa ya urithi wa dunia;
- vi. Uwepo wa sera ambazo zimepitwa na wakati mfano Sera ya Utalii ya mwaka 1999, Sera ya Taifa ya Misitu ya Mwaka,1998, Sera ya Malikale ya Mwaka 2008 na Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ya Mwaka 1998 kunapelekea wizara kushindwa kuendana na kasi ya mabadiliko ya kidunia;
- vii. Tatizo la kimundo la TFS kama Wakala wa Misitu limeifanya Wakala ishindwe kusimamia sekta ya misitu kwa ufanisi;
- viii. Uvamizi wa bonde la Kilombero kwa shughuli za kibinadamu litaendelea kutishia uhai na uendelevu wa Mradi wa Kufua Umeme wa Mwalimu Nyerere iwapo Serikali haitachukua hatua za haraka; na

ix. Katika kutekeleza mpamgo wa maendeleo wa ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19, Kamati inaona kuna umhimu kwa Wizara kuongeza kasi ya utekelezaji ikiwa ni pamoa na kumalizia kusaini mikataba nane (8) iliyosalia, kuwasilisha maombi ya fedha zilizobaki kila mara baada ya kukamilishwa kwa mikataba hata kama ni michache na kuendelea kusimamia kwa karibu na kufanya ufuatilaji (M&E) wa miradi ambayo imekwishaanza kutekelezewa

3.2 MAPENDEKEZO

3.2.1 Kutungwa kwa Sheria ya Uendeshaji wa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA)

KWA KUWA, Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania ilianzishwa kwa amri ya kisheria (*establishment order*) na Waziri mwenye dhamana chini ya Kifungu cha 8 cha sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009 ili kusimamia mapori ya akiba, mapori tengefu, jumuiya za hifadhi ya wanyamapori na maeneo ya ardhi oevu ambapo mamlaka hii inasimamiwa na Bodi ya Ushauri badala ya Bodi ya Utendaji;

NA KWA KUWA, Hali hii inaathiri utendaji wa mamlaka kwa kuwa inakosa nguvu ya kisheria katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Wanyamapori itakayoainisha bayana majukumu yake na kuanzisha Bodi ya Utendaji itakayoipa nguvu ya kisheria katika kutekeleza majukumu yake.

3.2.2 Usimamizi wa Rasilimali za Misitu Nchini

KWA KUWA, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) wamekuwa wakifanya kazi nzuri ya udhibiti wa matumizi ya rasilimali za misitu ya Serikali Kuu peke yake na kuziacha rasilimali zingine za misitu zisizo za serikali bila udhibiti madhubuti wa matumizi;

NA KWA KUWA, changamoto ya udhibiti wa matumizi ya rasilimali za misitu isiyokuwa ya Serikali pamoja na kuleta mgongano kwenye matumizi ya rasilimali hizo, kunachangia kuleta uharibifu na kutishia uendelevu wa misitu yetu;

KWA HIYO BASI, Bunge linashauri kwamba, Serikali kwa mara nyingine, kuharakisha mchakato wa kuipandisha hadhi Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) kuwa Mamlaka ya Misitu Tanzania ili kuipa nguvu ya kisheria ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya rasilimali za misitu yote nchini.

3.2.3 Changamoto ya Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro

KWA KUWA, Serikali imekuwa ikitumia Mfumo wa Matumizi Mseto ya Ardhi (*Multiple Land Use System*) katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa mujibu wa Sheria ambao umeiletea sifa Tanzania na kuifanya hifadhi hii kuwa sehemu ya urithi wa dunia;

NA KWA KUWA, mfumo huo pamoja na manufaa uliyoiletea nchi, bado umeleta changamoto nyingi, ikiwemo ongezeko la watu na mifugo, pamoja na shughuli nyingine za binadamu katika Hifadhi, hali hii imesababisha kuongezeka kwa gharama za kuwashudumia wananchi, pamoja na kuwepo kwa uharibifu wa mazingira, hali inayotishia kupoteza hadhi ya Hifadhi hiyo kama eneo la urithi wa dunia;

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kutekeleza mambo yafuatayo:-

i. Kuharakisha mchakato wa kufanya tathmini ya kina kuhusu mfumo wa matumizi ya ardhi katika eneo hilo, ili kusaidia kufanya marekebisho ya Sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ili kuendana na hali halisi iliyopo sasa.

ii. Serikali itafute namna bora ya kushughulikia changamoto ya eneo la Hifadhi Ngorongoro juu ya wananchi na mifugo ndani ya eneo hilo.

3.2.4 Changamoto Zinazolikabili Bonde La Kilombero

KWA KUWA, bonde hili limebainika kuwa linakabiliwa na changamoto kadhaa zinazotokana na matumizi mabaya ya ardhi ya bonde kama vile uvamizi wa shughuli za kibinadamu zisizo endelevu kama vile uvuvi, kilimo, ufugaji pamoja na uanzishwaji wa makazi holela au yaliyorasimishwa isivyo halali,

NA KWA KUWA, hali hiyo imeathiri kwa kiwango kikubwa uhifadhi wa bonde na kutishia kupoteza sifa ya kuendelea kuwa moja ya maeneo 4 yaliyotambuliwa kama yenye ardhi oevu (RAMSAR site), kupungua kwa mtiririko wa maji kuelekea Bwawa la Nyerere na hivyo kutishia uendelevu wa mradi wa kufua umeme na mradi wa SGR unaotegemea umeme kutoka Bwawa la Nyerere, kutoweka au kupungua kwa bioanual za wanyamapor, misitu na samaki,

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kutekeleza mambo yafuatayo:-

- i. Bonde la Kilombero lipandishwe hadhi kuwa hifadhi ya Taifa ili kuliwezesha eneo hili kuhifadhiwa vyema na kulinda mazingira yasiendelee kuharibiwa na shughuli za kijamii na kiuchumi zinazoendelea;
- ii. Kuimarisha ulinzi wa Bonde kwa kutumia Jeshi Usu pamoja na kuwashirikisha wananchi katika shughuli za uhifadhi wa Bonde na kuwaelimisha wananchi wanaozunguka hifadhi ya Bonde kuhusu umuhimu wa kulinda na kulihihifadhi bonde; na
- iii. Wananchi wote wanaofanya shughuli za kibinadamu zinazoleta athari kwenye bonde la Kilombero waondolewe ili kunususu na kuhifadhi bonde hilo.

3.2.5 Kulijengea Uwezo Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA)

KWA KUWA, Idadi ya Hifadhi za Taifa imeongezeka kutoka hifadhi 16 hadi 22; ambapo hata kabla ya kuanzishwa kwa hifadhi mpya 6, ni hifadhi 5 katи ya 16 zilizokuwa zina uwezo

wa kuijendesha zenyewe na kuzalisha ziada iliyosaidia kuendesha Hifadhi za Taifa nyingine 11;

NA KWA KUWA, Shirika linalipa kodi zote stahiki ikiwa ni pamoja na gawio kwa Serikali ambapo fedha hizo zingeweza kutumika kuzilea na kuzikuza hifadhi ambazo hazijaweza kujitegemea;

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kuangalia uvezekano wa kulipunguzia, au kuliondolea baadhi ya tozo kwa muda maalum ili kuliongezea Shirika nguvu ya kuweza kuzihudumia Hifadhi za Taifa kwa ufanisi na kuziwezesha hifadhi zote kuijendesha kwa mapato yake.

3.2.6 Miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa ya Morocco Square, Seven Eleven - Kawe, Golden Premier Residence - Kawe na Plot 300 Regent Estate Mikocheni iliyopo Dar es Salaam

KWA KUWA, kwa muda mrefu sasa miradi tajwa hapo juu imesimama, tangu ujenzi wake ulipoanza mwaka 2012 na 2013 kwa fedha za mkopo ambapo miradi hiyoilitarajiwa kukamilika mwaka 2015 na 2016;

NA KWA KUWA, kutokamilika kwa miradi hiyo kwa wakati kumeongeza gharama za ujenzi, ongezeko la riba, na Serikali kupata hasara kubwa ambayo inasababisha kutopatikana kwa thamani halisi ya fedha iliyowekezwa;

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kuchukua hatua stahiki na kwa wakati, ili kuiwezesha NHC kukamilisha miradi hiyo ili tija ya uwekezaji huo ionekane.

3.2.7 Mkakati Endelevu wa Upangaji, Upimaji na Umilikishaji wa Ardhi nchini

KWA KUWA, programu ya upimaji, upangaji na umilikishaji wa ardhi iliyokuwa inatekelezwa kwa majaribio katika Wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga, kwa kutumia zaidi fedha za wafadhili imekamilika kwa mafaniko makubwa ambapo

ilitarajiwa kusambazwa katika Wilaya nyingine za Mkoa wa Morogoro na Nchi kwa ujumla kwa kutumia bajeti ya ndani;

NA KWA KUWA, Serikali haijatenga fedha za kutosha za ndani kwa ajili ya kuendeleza programu hiyo ambayo imeonesha muelekeo wakufanikiwa kupunguza kwa kiasi kikubwa migogoro ya ardhi nchini. Kutotenga fedha za kutosha kunaathiri ufanisi wa programu hii;

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kuhakikisha inatenga fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya kuendeleza programu hii na programu nyingine ambazo zimeonesha mafanikio makubwa katika kuondoa migogoro ya ardhi nchini.

3.2.8 Changamoto za Upangaji, Upimaji na Umilikishaji Ardhi Dodoma

KWA KUWA, zoezi la upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi katika Jiji la Dodoma limekumbana na changamoto kadhaa za malalamiko ya ukosefu wa maadili toka kwa watumishi wa Halmshauri, Kuwepo kwa Makampuni ya kupima yenye utapeli, ukosefu wa elimu kwa wanachi na mgongano wa kimaslahi;

NA KWA KUWA, changamoto hizo zimekuwa zikikwamisha na kupunguza kasi ya upimaji wa ardhi ambapo unaikosesha serikali mapato yatokanayo na gharama za upimaji na kuwanyima wananchi wa makundi tofauti haki ya kumiliki ardhi kisheria;

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kutekeleza mambo yafuatayo:-

- i. Bodi na Mabaraza yanayoshughulika na usajili na nidhamu za watumishi wa Sekta ya ardhi ijielekeze zaidi katika kudhibiti maadili ili kurejesha imani kwa wananchi na taasisi zinazohudumiwa na wataalamu hawa;

- ii. Kuweka mkakati wa kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi kabla na kipindi cha zoezi la upimaji na umilikishaji ili kuondokana na migogoro isiyo ya lazima; na
- iii. Makampuni yote ambayo yalipewa kazi ya kurasimisha makazi katika Jiji la Dodoma na hayajakamilisha kazi hiyo kwa zaidi ya mwaka mmoja yatimize wajibu wao wa kisheria.

3.2.9 Kuhuisha Sera Mbalimbali zilizopitwa na Wakati

KWA KUWA, Sera nyingi katika sekta ya Ardhi na ile ya Maliasili na Utalii zimepitwa na wakati, kwa mfano Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999, Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ya mwaka, 1998;

NA KWA KUWA, kupitwa huku na wakati kunasababisha ugumu katika kutekeleza baadhi ya mambo ambayo yanatekelezwa kulingana na mabadiliko ya wakati na mazingira, sera ya Malikale ya Mwaka, 2008, Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki, na Sera ya Ardhi ya Mwaka 1995;

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuzihuisha sera zilizopitwa na wakati ili kuwezesha utekelezaji wake kuwa na ufanisi.

3.2.10 Kuanzisha Mfuko wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha (KKK)

KWA KUWA, Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha (KKK) Ardhi nichini imeonesha mafanikio makubwa baada ya kufanikiwa kumilikisha vipande vingi vya ardhi nichini na kupelekea kuondoa migogoro ya ardhi kwenye maeneo yaliyomilikishwa;

NA KWA KUWA, bado kuna maeneo mengi nichini yanayohitaji kufikiwa na programu hii ili kumaliza kabisa changamoto zinazotokana na vipande vya ardhi ambavyo havijapimwa nichini;

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kuanzisha Mfuko wa KKK kama ulivyo Mfuko wa Maji ambapo mfuko huu utatumika kwa ajili ya Kupanga, Kupima na kumilikisha ardhi nchini hasa vijiji Miji (Growing towns) na kupunguza/ kuondoa kabisa makazi holela na kuongeza wigo wa walipa kodi.

3.2.11 Kuanzishwa kwa Mamlaka ya kusimamia Sekta ya Nyumba Nchini (Real Estate Regulatory Authority - RERA)

KWA KUWA, nchi yetu haina mamlaka inayosimamia sekta ya nyumba na limekuwa ni tatizo la muda mrefu,

NA KWA KUWA, Kukosekana kwa Mamlaka ya kusimamia sekta ya Nyumba (Real Estate Regulation and Control) nchini kumepelekea kuwepo kwa utitiri wa madalali wa nyumba, uholela wa bei za kupanga na hata kuikosesha mapato serikali kwa kiasi kikubwa,

KWA HIYO BASI, Bunge linashauri kwamba, Serikali iharakishe mchakato wa kuanzisha Mamlaka ya kusimamia Sekta ya Nyumba ili kuwepo na chombo madhubuti kinachosimamia sekta ya nyumba nchini.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO NA KUFUNGA HOJA

4.1 Hitimisho

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii katika kutekeleza Shughuli zake kwa kipindi cha Februari 2021 hadi Januari, 2022 yametokana na juhudi, weledi pamoja na umahiri mkubwa wa Wajumbe katika kushiriki na kutoa maoni yenye tija wakati wote ambapo Kamati imekuwa ikiisimamia Serikali. Ni wazi kwamba, ufanisi wa utendaji wa Kamati hii unatokana zaidi na Ofisi yako kuwajengea uwezo Wabunge na kuwapa msaada stahiki wa kitaalam, na kiushauri wakati wote. Kwa heshima kubwa ningependa kuwataja majina yao, hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina hayo ni haya yafuatayo: -

1. Mhe. Ally Juma Makoa, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Shabani Omary Shekilindi, Mb – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Jafari W. Chege, Mb Mjumbe
4. Mhe. Soud Mohamed Juma, Mb ‘
5. Mhe. Phillipo Augustino Mulugo, Mb “
6. Mhe. Khalifa Salum Suleiman, Mb “
7. Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo, Mb “
8. Mhe. Neema William Mgaya, Mb “
9. Mhe. Asya Mwadini Mohamed, Mb “
10. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb “
11. Mhe. Maida Hamadi Abdallah, Mb “
12. Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb “
13. Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb “
14. Mhe. Hassan Seleman Mtenga, Mb “
15. Mhe. Asia Abdulkarimu Halamga, Mb “
16. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb “
17. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb “
18. Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb “
19. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman, Mb “
20. Mhe. Munira Mustafa Khatibu, Mb “
21. Mhe. Dkt Florence G. Samizi, Mb “
22. Mhe. Agnes Mathew Marwa, Mb “
23. Mhe. Godwin Emmanuel Kunambi, Mb “
24. Mhe. Mwanakhamis Kassim Said, Mb “
25. Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb “
26. Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mb “

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mhe. Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuipatia Wizara ya Maliasili na Utalii **Shilingi Bilioni 90.2** ambazo ni fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19 ambazo zinalenga kuchocheara ukuaji wa sekta ya utalii. Aidha, tunapongeza hatua ya Rais kama mkuu wa nchi kuwa mstari wa mbele kuhamasisha utalii kupitia *royal tour* ambayo imechangia kuongeza idadi ya watalii nchini.

Aidha, kwa namna ya kipekee napenda kumpongeza Mhe. Dr Tulia Akson (Mb) kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Dkt. Angeline S. Mabula (Mb), na Naibu wake Mhe. Ridhiwani J. Kikwete, (Mb) Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Dkt. Damas D. Ndumbaro (Mb) na Naibu wake Mhe. Mary F. Masanja, (Mb) pamoja na watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nimshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi (*ndc*) kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo wakati wote. Vilevile, nimshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, akisaidiwa na Wakurugenzi Wasaidizi Ndg. Dickson M. Bisile na Ndg. Gerald S. Magili, Bila kuwasahau Makatibu walioandaa taarifa hii akiwemo, Ndg. Ramadhan Abdallah, Ndg. Monica Mwamunyange, Ndg. Elieka Saanya na Ndg. Rehema Kipera pamoja na Msaidizi wa Kamati Ndg. Mwimbe John.

4.2 HOJA

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza shughuli zilizotekelawa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji shughuli hizo, na pia maoni na mapendekezo ya Kamati, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa lipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Ally Juma Makoa, Mb
MWENYEKITI

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI,
MALIASILI NA UTALII**
Februari, 2022

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Utalii.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, nitoe tangazo. Wageni leo mmekuwa wengi sana kwa Waziri Mkuu, lakini pia mnatumia muda mrefu sana kukaa hapo. Yaani mtu anakaa dakika 15 hadi dakika 20. Sasa huyu mgeni aliyeo hapo kwa leo atakuwa wa mwisho kwa sababu hizi hoja za Kamati mwishoni tutakapohojiana ni maagizo kwa Serikali, naye ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Asipofahamu Wabunge tunaiagiza nini Serikali, tutabaki tena humu tunaulizana maswali, yale maagizo tuliyotoa ilikuwaje?

Kwa hiyo, huyu atakuwa mgeni wa mwisho kwa leo ili tumpe fursa Mheshimiwa Waziri Mkuu kusikiliza hoja za Wabunge zinazotoka kwenye Kamati zetu. Hapo baadaye naendelea kutafakari na nitashauriana na watalaam, tutaweka muda mahususi, yaani mtu akienda hapo akae muda gani? (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ninyi ni mashahidi, Mheshimiwa Waziri Mkuu huwa anasikiliza kila mtu, ofisi yake iko wazi muda wote. Kwa hiyo, anapokuja humu Bungeni ni kwa sababu yeye ni Mbunge, lakini pia ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Kwa hiyo, anataka kusikiliza pia Wabunge wanasmaje? Sasa tukifanya kiti chake kile ndiyo ofisi, humu ndani kile kiti chake siyo ofisi. Sawa Jamani eeh! (*Makof*)

Kwa hiyo, hapo baadaye nitatoa mwongozo wa muda gani mtu anaruhusiwa kwenda kukaa pale ili usiende pale unapiga *story*. Mheshimiwa Waziri Mkuu kaja ili awasilikize Wabunge wote wanasma nini? Kwa hiyo, huyo atakuwa mgeni wa mwisho kwa siku ya leo. Ahsante sana.

Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Vita Kawawa kwa niaba ya Mwenyekiti.

MHE. VITA R. KAWAWA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YAKUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba sasa nisome taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa Kipindi cha Januari, 2021 na Februari, 2022.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amirijeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuvisimamia na kuviimarisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama na kuhakikisha vinatekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Aidha, kwa namna ya pekee nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuimarisha hali ya mahusiano ya Kimataifa ambapo tangu aingie madarakani mwezi Machi, 2021 ameteua Mabalozi 28 kwa ajili ya uwakilishi katika nchi na maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tunakupongeza wewe kwa kuchaguliwa na Bunge letu Tukufu kuwa Spika wa Bunge hili. Kwa niaba ya Kamati, tunaahidi kushirikiana nawe katika kuhakikisha kuwa Bunge linatekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee, lijadili na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa Kipindi cha Kuanzia Januari, 2021 hadi Februari, 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane, Fasili ya (6) Kifungu cha 3, ikisomwa pamoja na fasili ya (7) Kifungu cha 1 na Kifungu cha 2 cha Kanuni ya Kudumu ya Bunge; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, ni moja kati ya Kamati tisa za Kudumu za Bunge za Kisekta. Kamati hii inasimamia Wizara tatu zifuatizo:-

- (1) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;
- (2) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; na
- (3) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati hii ni yameainishwa katika ukurasa wa nne hadi wa tano wa taarifa hii iliyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022 Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama imetekeleza shughuli mbalimbali masharti ya fasili ya 7(1) na Kifungu kidogo cha (2) cha Nyongeza ya Nne ya Kanuni ya Kudumu za Bunge. Shughuli hizo zimeainishwa katika ukurasa wa saba na ukurasa wa nane wa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ni uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, masuala yanayotolewa na taarifa hii ni yale ambayo Kamati imebaini kuwa changamoto zake zinahitaji kupewa umuhimu wa kipekee ili kuziwezesha Wizara pamoja na taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hivyo kuleta tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika matokeo ya uchambuzi wa Kamati, kuhusu kutokamilika kwa sera ya mambo ya nje: Sera ya Mambo ya Nje ilizinduliwa mwaka 2001 na Rais wa Serikali wa Awamu ya Tatu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Benjamin William Mkapa na hivyo kuifanya Sera hiyo kufikisha miaka 20 tangu kutungwa kwake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ukweli kwamba Sera hiyo ni ya muda mrefu na hivyo kuwepo kwa masuala mbalimbali yanayohitaji kufanyiwa mapitio, tangu Mwaka 2017 Kamati katika taarifa zake za mwaka za utekelezaji wa shughuli zake imekuwa ikiishauri Serikali kufanya mapitio ya marekebisho yake ili iendane na mabadiliko ya sasa ikiwemo ya kiuchumi, kisiasa, kiusalama, kijamii na kimazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha shughuli za Kamati za Mwezi Augosti, 2021 Kamati ilipokea taarifa kuhusu hatua za maandalizi ya kuandaa rasimu ya Sera ya Mambo ya Nje, kuelezwu kuwa Serikali inaendelea na zoezi la kuandaa rasimu ya sera.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudhi hizo zinazofanywa na Serikali katika kupata Sera mpya ya Mambo ya Nje, Kamati imebaini kuwa kasi ya mchakato huo hairidhishi ikilinganishwa na uhitaji wa sera hiyo kwa mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Spika, Balozi zetu nje ya nchi kwa muda mrefu zimekuwa zikikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo uhaba wa Watumishi, uhaba wa vyombo vyta usafiri pamoja uhaba wa uchakavu wa majengo. Katika kiindi kinachotolewa taarifa hii, Kamati imebaini kuwa Serikali imefanya kazi baadhi ya ushauri wa Kamati kuhusu namna ya kutatua changamoto hizo hususan katika eneo la watumishi na magari ya kutoa huduma katika Balozi zetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo zilizochukuliwa na Serikali, Kamati imebaini kuwa uchakavu na upungufu wa majengo Balozini bado ni changamoto kubwa. Hadi kufikia mwezi Januari, 2022 ni Balozi Nne tu kati ya 44 ndizo ambazo zinatumia majengo yake kwa ajili ya matumizi yote ya Ofisi na Makazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Serikali ilitoa maelezo kuwa Wizara inaendelea kutekeleza mpango wa ukarabati wa ujenzi wa majengo ya ofisi na makazi ya watumishi Balozini kwa lengo la kutatua changamoto ya

uchakavu na upungufu Balozini, Kamati inaona kuwa bado fedha zinazotengwa kwa ajili ya kutekeleza mpango huo hazitolewi kwa wakati na wakati mwingine hazitolewi kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu mtiririko usioridhisha wa fedha za maendeleo kwa Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Fungu 29 - Magereza. Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2021 na ilibaini kuwa mtiririko wa fedha za matumizi ya kawaida, yaani mishahara na mingineyo kwa mafungu yote ya Wizara hii ni mzuri.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa upande wa mtiririko wa fedha za maendeleo, Kamati ilibaini kuwa Fungu 28 Jeshi la Polisi na Fundu 93 Uhamiaji ndiyo iliyopokea fedha za maendeleo ambapo Idara ya Uhamiaji ilipokea asilimia 67.54 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge na Jeshi la Polisi limepokea asilimia 92.5 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa upande wa Fungu Na. 14 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji pamoja na Fungu 29 Jeshi la Magereza, Kamati ilibaini kuwa mafungu hayo bado hayajapokea fedha zozote za maendeleo ambazo ziliidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, tangu Bunge la Kumi na Moja, Kamati hii imekuwa ikiishauri Serikali pamoja na mambo mengine kuliwezesha Jeshi la Magereza kutekeleza mpango wa kujitosheleza kwa chakula. Hata hivyo, utekelezaji wa mpango huo umekuwa ukikabiliwa na changamoto za kibajeti kama Kamati ilivyobaini ambapo kwa kipindi cha Julai - Desemba, 2021 bado fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo shilingi bilioni sita bado hazijatolewa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa tija iliyokusudiwa na Bunge lilipoidhinishwa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa mafungu ya Wizara

ya Mambo ya Ndani, kutotolewa kwa fedha hizo kutaathiri mpango wa utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya kina kuhusu mtiririko usioridhisha wa fedha za maendeleo, Fungu Na. 14 na Fungu Na. 29 - Magereza inapatikana katika ukurasa wa 20 hadi 22 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji usioridhisha wa Vitambulisho vya Taifa; uchambuzi wa Kamati wa mwezi Novemba, 2021 kuhusu hali ya upatikanaji wa Vitambulisho vya Taifa ulibaini kuwa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *NIDA* ilisajili watu 22,682,414 hadi kufikia mwezi Novemba, 2021 ikiwa ni asilimia 90.6 ya lengo la watu 25,000,000 waliokusudiwa kusajiliwa katika awamu ya kwanza ya mradi mwaka 2013/2015.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati ilibaini kuwa kati ya idadi ya watu waliosajiliwa ni watu 19,131,466 ambao wamepata namba za utambulisho ikiwa ni sawa na asilimia 84.3 ya watu waliosajiliwa.

Aidha, Kamati ilihoji idadi ya vitambulisho vilivytotolewa kulingana na namba hizo za usajili tangu mradi huu ulipoanza mwaka 2013 na kubaini vitambulisho 10,124,722 vilizalishwa ikiwa ni sawa na asilimia 52.9 ya namba za usajili zillizopo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia uchambuzi wake wa kina, Kamati ilishauri Serikali kuhusu mikakati mbalimbali ya kutekelezwa na *NIDA*. Kwa kipindi cha Novemba, 2021 hadi Desemba, 2021 ili kufanikisha zoezi la upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa kwa wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge Iako Tukufu kuwa katika kipindi cha Februari, 2022 Wizara iliwasilisha taarifa ya *NIDA* ambayo ilieleza kuwa Serikali ilipokea ushauri wa Kamati ambapo imeanza kutekeleza mikakati hiyo ikiwa ni pamoja na kuomba fedha Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijiridhisha kuwa suala la upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Vitambulisho vya Taifa ni jambo linalotakiwa kupewa uzito wa kipekee ili kuwezesha mamlaka kutekeleza na kufikia malengo yake kwa kiwango stahiki. Taarifa ya kina kuhusu upatikanaji usioridhisha wa vitambulisho vya Taifa inapatikana katika ukurasa wa 23 hadi ukurasa wa 24 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kinachotolewa taarifa, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Taarifa ya Hali ya Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba, 2021 kwa kulinganisha na hali ya ulinzi na usalama katika kipindi kama hicho mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge Iako Tukufu kuwa, katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa wakati idadi ya makosa dhidi ya binadamu yamepungua kwa asilimia 6.1 ikilinganishwa na mwaka 2020, makosa ya usalama barabarani na makosa dhidi ya maadili ya Jamii yameongezeka.

Aidha, Kamati ilibaini kuwa bado kuna msongamano wa mahabusu na wafungwa Magerezani ambapo jumla ya mahabusu na wafungwa na Magerezani ni 32,010 ikiwa ni sawa na asilimia 107 zaidi ya uwezo wa Magereza yaliyopo kwa sasa wa kuwahifadhi wafungwa na mahabusu 29,902.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kuendelea kutumia adhabu mbadala kama vile Mpango wa *Parole* au kutumikia kifungo cha nje, bado wanufaika wa mpango huo ni wachache.

Mheshimiwa Spika, Kukosekana kwa Alama za Mipaka Nchini; Kamati ilipokea na kujadili taarifa kuhusu hali ya ulinzi na usalama wa mipaka nchini mwezi Februari, 2022, ilibaini kuendelea kuwepo na changamoto ya uharibifu wa alama za mipaka na hivyo kusababisha wafugaji kutoka katika baadhi ya nchi tunazopakana nazo kufanya shughuli za

ufugaji katika maeneo ya mipaka ambayo hayaruhusiwi kisheria.

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu zinaonesha kuwa changamoto hii ni ya muda mrefu na imekuwa ikiripotiwa Bungeni tangu Bunge la Nane. Ni wazi kuwa tatizo hili lisiposhughulikiwa litahatarisha usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Ubovu wa Barabara za Mipakani; ubovu wa barabara za usalama mipakani umeendelea kusababisha ugumu wa kufanya doria na kudhibiti mipaka yetu kwa nyakati tofauti. Bunge la Kumi na Bunge la Kumi na Moja, Kamati hii imekuwa ikiishauri Serikali kuhusu umuhimu wa kutatua changamoto hii, hata hivyo suala hili bado halijatekelezwa kwa ukamilifu wake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Masuala ya Umiliki wa Chuo Cha Diplomasia, Hali ya Mtangamano wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Mtangamano wa Afrika Mashariki, Utendaji wa Jeshi la Magereza, Maoni Kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mwaka 2021 na Matokeo ya Semina zilizofanyika yanapatikana katika ukurasa wa 13 mpaka 29 wa taarifa iliyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu; Maoni na Mapendekezo. Maoni; baada ya kuwasilisha matokeo ya uchambuzi wa Kamati katika Sehemu ya Pili, naomba sasa kuwasilisha Maoni ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; kutokana na kutokamilika Sera mpya ya Mambo ya Nje na kusababisha sera iliyopo kuendelea kutumika ilhali haiendani na kasi ya maendeleo ya kiuchumi duniani, kuendelea kutumia Sera ya Nje ya m waka 2001 kunaathiri utekelezaji wa masuala yanayohitaji muongozo wa kisera ambayo hayajatajwa kwenye sera ya sasa, kama vile masuala ya *diaspora* na mtangamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, tatu, changamoto ya umiliki wa chuo cha diplomasia imekuwa ya muda mrefu, jambo ambalo linasababisha Serikali ya Tanzania pekee kuendelea na jukumu la kukiendesha na kugharamia shughuli zote za chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, nne, ili kuwezesha wananchi wengi Zaidi kunufaika na fursa zitokanazo na mtangamano wa kikanda na mtangamano wa Afrika Mashariki, Serikali iendelee kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa zilizopo pamoja na vigezo vya bidhaa zinazohitajika katika masoko ya nje.

Mheshimiwa Spika, tano, kutokutolewa kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza mpango wa miaka 15 wa ukarabati na ujenzi wa majengo ya ofisi na makazi ya watumishi katika Balozi za Tanzania nje ya nchi kunakwamisha utekelezaji wa mpango huo.

Mheshimiwa Spika, sita, pamoja na nia ya dhati ya Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika Balozi za Tanzania nje ya nchi, kutotolewa kwa fedha za maendeleo kutoka Hazina kumeendelea kuwa changamoto ya muda mrefu inayoathiri utekelezaji miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, saba, kupeleka watumishi zaidi katika balosi zetu pamoja na kuongeza magari ya kutoa huduma katika balozi zetu kunaongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya balozi hizo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; kukosekana kwa alama za mipaka ya nchi kunachangia uvamizi wa shughuli za kibinadamu katika maeneo hayo, jambo ambalo si zuri kwa ulinzi na usalama wa nchi.

Mheshimiwa Spika, ubovu wa barabara za mipakani unasababisha ugumu wa kufanya doria na kudhibiti mipaka ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; uhaba wa maofisa wa ngazi za juu na askari wa Jeshi la Magereza unaathiri ufanisi wa Jeshi la Magereza katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, madeni ya taasisi za Serikali kwa Jeshi la Magereza yanakwamisha juhudzi za jeshi katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, ikiwemo kuboresha kilimo.

Mheshimiwa Spika, tatu, uhaba wa miundombinu ya umwagiliaji na vifaa vya kilimo, kama vile matrekta, unasabisha Jeshi la Magereza kushindwa kufanya kilimo cha biashara ambacho Kingechangia katika kukuza mapato yake na mapato ya Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya magereza pia, kutokuwa na hati za umiliki wa ardhi kunasababisha migogoro ya ardhi na wakati mwingine ardhi ya jeshi kutwaliwa na Serikali kwa ajili ya matumizi mengine.

Mheshimiwa Spika, kutotumika ipasavyo kwa mpango wa parole na matumizi hafifu ya sheria zinazoruhusu adhabu mbadala kwa wafungwa kunachangia kwa kiasi kikubwa msongamano magerezani.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa vifaa na vitendea kazi kwa jeshi la zimamoto na uokoaji unasababisha jeshi hilo kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji wa fedha za maendeleo kwa Fungu Namba 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Fungu 29 – Magereza, kunaathiri utekelezaji wa miradi muhimu ya majeshi hayo.

Mheshimiwa Spika, kutokuzalisha vitambulisho vya Taifa kulingana na malengo yaliyowekwa pamoja na kuzingatia uhalisia wa mahitaji yake kunaathiri tija iliyokusudiwa na uzalishaji wa vitambulisho hivyo.

Mheshimiwa Spika, mafunzo na semina kwa Kamati; upo umuhimu wa kutoa mafunzo kwa Kamati, hususan zile za kisekta, kuhusu usimamizi wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi ili kuwaelimisha na kuwakumbusha Wabunge kuhusu umuhimu wa kusimamia utekelezaji wa diplomasia ya uchumi kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo; baada ya kueleza maoni ya Kamati naomba sasa kutoa mapendekezo ya Kamati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Mpango wa Ukarabati na Ujenzi wa Majengo ya Ofisi na Makazi ya Watumishi wa Balozi:-

KWA KUWA balozi takribani 40 za Tanzania nje, zinazopanga majengo kwa ajili ya ofisi na makazi kutokana na kutokuwa na majengo. Aidha, majengo ya balozi hizo kuwa yamechakaa;

NA KWA KUWA fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza mpango wa miaka 15 wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi ya watumishi mabalozini hazitolewi kwa wakati na mara nyingine hazitolewi kabisa;

NA KWA KUWA kutokutolewa kwa fedha hizo kunasababisha Serikali kendelea kupoteza fedha nyingi kwa ajili ya kulipia pango;

KWA HIYO BASI Bunge linaishauri Serikali kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kila mwaka, ili kuwezesha utekelezaji wa mpango huo kwa maslahi mapana ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kutokamilika kwa Sera Mpya ya Mambo ya Nje:-

KWA KUWA kwa kipindi cha miaka mitano tangu mwaka 2017, Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kufanya marekebisho Sera ya Mambo ya Nje Mwaka 2001;

NA KWA KUWA msingi wa ushauri huo ulijikita katika ukweli kwamba, sera hiyo ni ya muda mrefu na hivyo, kuhitaji kufanyiwa mapitio ili iendane na mabadiliko mbalimbali ya kiuchumi, kijamii na kisiasa katika kipindi chote tangu itungwe;

NA KWA KUWA marekebisho yanayotarajiwa kufanyika ni pamoja na kuingiza masuala ya *diaspora* na mtangamano wa Afrika Mashariki ili yapate muongozo wa kisera;

KWA HIYO BASI Bunge linaishauri Serikali iongeze kasi ya maandalizi ya Sera ya Mambo ya Nje ili ianze kutumika rasmi mara moja.

Mheshimiwa Spika, Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii:-

KWA KUWA makosa dhidi ya maadili ya jamii ikiwemo matumizi ya dawa za kulevyia yameongezeka kwa 29.2% ikilinganishwa na mwaka 2022 katika kipindi cha Julai hadi Disemba;

NA KWA KUWA makosa haya yakiendelea kuongezeka na yatachangia pia, ongezeko la makosa dhidi ya binadamu ikiwemo mauaji, kubaka na kulawiti, hali ambayo sio nzuri kwa usalama wa raia;

KWA HIYO BASI Bunge linaishauri Serikali kuwa na mpango mkakati wa kupunguza makosa dhidi ya maadili ili kupunguza matukio ya makosa dhidi ya binadamu, ambayo yanaleta taharuki katika jamii na kuathiri usalama wa raia ambaao ndio nguzo muhimu ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Msongamano wa Mahabusu na Wafungwa:-

KWA KUWA uwezo wa magereza yaliyopo nchini kuhifadhi wafungwa 29,902 kwa siku na hadi kufikia mwezi Disemba, 2021 idadi ya wafungwa na mahabusu ilikuwa 32,010 ikiwa ni sawa na 107% zaidi ya uwezo wa magereza yaliyopo;

NA KWA KUWA tatizo la msongamano ni kubwa Zaidi katika magereza ya mahabusu ambao wanasubiri maamuzi ya kesi zao mbalimbali;

NA KWA KUWA kamati inatambua kuwa jukumu la kupunguza msongamano magerezani linajumuisha taasisi mbalimbali;

KWA HIYO BASI Bunge linaishauri Serikali iendelee kutenga na kutoa fedha kwa ajili ya kujenga magereza katika mikoa na wilaya zisizokwu na magereza pamoja na kukarabati mabweni yaliyochakaa na kuongeza mabweni katika magereza ambayo bado yana nafasi, ili kuhimili uhifadhi wa wafungwa na mahabusu;

Mheshimiwa Spika, pili, isimamie Kamati za Kusukuma Kesi kukutana mara kwa mara ili kumaliza changamoto ya ucheleweshaji wa kesi mahakamani;

Mheshimiwa Spika, tatu, ihakikishe upelelezi wa kesi, hususan, zile ambazo si za jnai hauchukui muda mrefu;

Mheshimiwa Spika, nne, iendelee kutumia mpango wa parole kwa wafungwa wengi wanaokidhi vigezo vya kutumikia vifungo vya nje chini ya mpango huo na kutoa adhabu mbadala kwa wafungwa wasiokuwa na tishio kwa usalama wa raia.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Upatikanaji wa Vitambulisho vya Taifa:-

KWA KUWA uzalishaji wa Vitambulisho vya Taifa umeendelea kuwa changamoto ya muda mrefu na hivyo kufanya upatikanaji wa vitambulisho hivyo kuwa chini ya lengo tangu kuanza kuzalishwa kwake mwaka 2013;

NA KWA KUWA, raia kutokuwa na vitambulisho vya Taifa kunaathiri upatikanaji wa huduma mbalimbali zinazohitaji raia kuwa na vitambulisho vya Taifa, kama vile kupata *passport* mpya na mambo mengineyo;

KWA HIYO BASI ili kuwezesha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa kuzalisha vitambulisho kwa wakati na kulingana na malengo yaliyowekwa pamoja na uhitaji halisi wa vitambulisho hivyo; Bunge linaishauri Serikali kutenga fedha za maendeleo kulingana na mahitaji halisi ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, ikiwa ni pamoja na kutengewa fedha za kutosha kwa ajili ya manunuzi ya kadi ghafi na ununuzi wa vyombo vya usafiri;

Mheshimiwa Spika, pili, kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati kwa ajili ya uzalishaji wa vitambulisho vya Taifa;

Mheshimiwa Spika, tatu, kuwa na mkakati wa kuboresha vitendea kazi vya teknolojia kama vile *computers* na *software(s)* mbalimbali ili kwenda sambamba na kasi inayokusudiwa na uzalishaji wa vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho; napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha kwa niaba ya Kamati, Taarifa ya Mwaka ya Kamati Kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa Kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022.

Mheshimiwa Spika, napenda pia, kuchukua nafasi hii kuwashukuru aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa George Simbachawene na Naibu wake Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis Chilo, kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati hii walipokuwa na dhamana ya Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, kipekee namshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani wa sasa, Mheshimiwa *Engineer*Hamad Masauni, pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Jumanne Sagini, kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kipindi kifupi ambacho Kamati imefanya kazi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile namshukuru Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Stegomena Taxi, na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Balozi Mbaruku Nassor Mbaruku, pamoja na watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano walioonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Ndugu Nenelwa Mwihambi, Katibu wa Bunge, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake.

Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Kamati ya Bunge, Ndugu Athumani Hussein; Mkurugenzi Msaidizi Gerald Magili; Makatibu wa Kamati Ndugu Ramadhan Abdallah, Bi. Grace Bidya na Bi. Victoria Mizengo, wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati kwa kipindi chote cha mwaka mzima na hata kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, hoja; baada ya kueleza shughuli zilizotekelizwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, maoni na mapendekezo, sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa lipokee, lijadili na hatimaye kuikubali taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU
YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KWA
KIPINDI CHA JANUARI, 2021- FEBRUARI, 2022 - KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

[Inatolewa Chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za
Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020]

SEHEMU YA KWANZA

MAELEZO YA JUMLA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuvisimamia na kuviiimarisha vyombo vyote vya ulinzi na usalama na kuhakikisha vinatekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Aidha, kwa namna ya pekee nampongeza Mhe. Rais kwa kuimarisha hali ya mahusiano ya Kimataifa ambapo tangu aingie madarakani mwezi Machi, 2021 ameteua Mabalozi ishirini na nane (28) kwa ajili ya uwakilishi katika Nchi na maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, tunakupongeza kwa kuchaguliwa na Bunge letu Tukufu kuwa Spika wa Bunge hili, kwa niaba ya Kamati tunaahidi kushirikiana nawe katika kuhakikisha kuwa Bunge linatekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee, lijadili

na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2021 hadi Februari, 2022.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii ya Mwaka ndio ya kwanza katika kipindi cha kwanza cha uhai wa Kamati katika Bunge la Kumi na Mbili. Kwa muktadha huu, naomba kukushukuru Mheshimiwa Spika kwa kuteuwa wajumbe Ishirini ili kuunda Kamati hii. Naomba niwashukuru wajumbe hao ambao kwa kipindi chote tangu kuundwa kwake, wametumia taaluma, uzoefu na sifa nyingine muhimu katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Wajumbe hao ni: -

1. Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Vincent Paul Mbogo, Mb. - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Bonnah Ladislaus Kamoli, Mb- Mjumbe
5. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Janeth Mauris Masaburi, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Cosato David Chumi, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Stela Alex Ikupa, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Zahor Mohammed Haji, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Alexander Pastory Mnyeti, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Felister Deogratius Njau, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Fakharia Shomar Khamis, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Vita Rashid Kawawa, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Muharami Shabani Mkenge, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Mwinyikondo Rajab Mustafa, Mb- Mjumbe
18. Mhe. Ali Juma Mohamed, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Abdi Hija Mkasha, Mb - Mjumbe; na
20. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inaelezea shughuli zilizotekeliza na Kamati kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2021 hadi Februari, 2022. Aidha, masuala yanayoainishwa kwenye Taarifa hii ni yale tu ambayo Kamati inaona kuwa utekelezaji wake unahitaji juhudii zaidi kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Taarifa inayowasilishwa imegawanyika katika Sehemu Kuu nne zifuatazo: -

- i) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuhusu majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelzwa;
- ii) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati;
- iii) Sehemu ya Tatu inabainisha maoni na mapendekezo ya Kamati; na
- iv) Sehemu ya Nne ni Hitimisho.

1.1 Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa lengo kuu la Serikali ni ustawi wa Wananchi na kwamba Serikali inawajibika kwa Wananchi kwa Mujibu wa Ibara ya 8 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Kamati hii inatekeleza majukumu yake kwa niaba ya Bunge ambalo, kwa niaba ya Wananchi, ndio linaisimamia na kuishauri Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake kama Ibara ya 63 (2) (3) inavyotaja.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane, Fasili ya 6, Kifungu cha 3 ikisomwa pamoja na Fasili ya 7, Kifungu cha (1) (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ni moja kati ya Kamati Tisa (9) za Kudumu za Bunge za Kisekta. Kamati hii inasimamia Wizara Tatu (3) zifuatazo:-

- i) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;
- ii) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; na
- iii) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, Majukumu ya Kamati hii ni:-

- i) Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia;
- ii) Kushughulikia Miswada na Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;
- iii) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na
- iv) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu ya kusimamia Wizara zilizoainishwa hapo juu, Kamati ina majukumu matano (5) ya nyongeza yaliyoainishwa kwenye Fasili ya 7, Kifungu cha 2, ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Majukumu hayo ni: -

- i) Kuimarisha ushirikiano kati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mabunge ya nchi nyingine;
- ii) Kufuatilia mwenendo na hali ya mtangamano wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika;
- iii) Kushughulikia taarifa za wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika;
- iv) Kushughulikia taarifa zote za wawakilishi katika Vyama mbalimbali vya Kibunge ambapo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwananchama; na
- v) Kushughulikia Taarifa za hali ya Ulinzi na Usalama wa Mipaka ya Nchi na Usalama wa Raia na Mali zao.

1.2 Njia na Mbinu zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati;

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kamati ilitumia njia na mbinu mbalimbali zilizoendana na matakwa ya Kanuni ya 136 (3) na (5) kuhusu kukutana na

kuzingatia bajeti ya Kamati iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2020/2021 na 2021/2022. Njia zilizotumika ni:-

- i) Vikao na Wizara kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji za Wizara hizo pamoja na Taasisi zake;
- ii) Ziara za kukagua utekelezaji wa masuala mbalimbali hususan Miradi ya Maendeleo ilio chini ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020;
- iii) Kuwasilisha kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti hoja mahsusizi zilizotokana na Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022;
- iv) Kutoa taarifa maalumu ya ushauri kwa Waziri mwenye dhamana juu ya masuala ya utekelezaji ambayo yanahitaji kurekeblishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 135 (17); na
- v) Kupata mafunzo mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na Serikali na Taasisi zake.

1.3 Shughuli zilizofanyika

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari 2021 – hadi Februari, 2022 Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama imetekeliza shughuli zifuatazo:-

1.3.1 Mafunzo na Semina mbalimbali

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa Kamati hii iliundwa Mwezi Januari, 2021, mafunzo yalitolewa katika kipindi kinachotolewa Taarifa ili kujenga uelewa wa Wajumbe wa Kamati katika maeneo mbalimbali hususan yale yanayohusu majukumu ya Kamati hii. Mafunzo na Semina zilizotolewa ni:-

- i) Mafunzo kuhusu Muundo na Majukumu ya Kamati ikiwa ni pamoja na umuhimu wa kuzingatia tahadhari zinazohusu Ulinzi, Usalama na Diplomasia katika shughuli za Kamati. Lengo lilikuwa kutoa uelewa kwa Wajumbe kuhusu mawanda

(scope) ya majukumu yao. Mafunzo haya yaliratibiwa na Bunge Mwezi Januari, 2021;

ii) Mafunzo kuhusu Muundo na Majukumu ya Wizara na Taasisi zinazosimamiwa na Kamati ili kuwapa uelewa mpana Wajumbe kuhusu Sekta zinazosimamiwa na Kamati hii. Mafunzo haya yalitolewa na Wizara husika Mwezi Januari, 2021;

iii) Mafunzo kuhusu matumizi ya Bunge Mtandao (e-Parliament) ili kuwawezesha Wajumbe kutumia mfumo wa Bunge Mtandao. Mafunzo haya yaliratibiwa na Ofisi ya Bunge Mwezi Januari, 2021;

iv) Mafunzo ya Stratejia yaliyoratibiwa na Chuo cha Ulinzi cha Taifa, Dar es Salaam, Mwezi Agosti, 2021 ili kupata uelewa mpana kuhusu dhana ya ulinzi na usalama wa taifa;

v) Mafunzo ya Diplomasia yaliyoratibiwa na Chuo cha Diplomasia, Dar es Salaam Mwezi Septemba, 2021 ili kupata uelewa mpana kuhusu masuala ya diplomasia hususan diplomasia uchumi na Itifaki ya viongozi; na

vi) Semina kuhusu Mbinu na Stadi za uchambuzi wa Miswada ya Sheria iliyoratibiwa na Bunge kuititia mradi wa Kulijengea Uwezo Bunge (Legislative Support Project-LSP) II, Mwezi Oktoba, 2021. Lengo lilikuwa kuwajengea uwezo Wajumbe katika kuchambua Miswada ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kuwa mafunzo na Semina hizo kwa kiasi kikubwa zimewajengea uwezo wajumbe wa Kamati katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi hususan katika masuala yahusuyo Stratejia, Diplomasia, na Uchambuzi wa Miswada ya Kisheria.

1.3.2 Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji za Wizara

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia masharti ya Nyongeza ya Nane, Fasili ya 7, Kifungu cha (1) (d) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilipokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa

majukumu ya Wizara inazozisimamia pamoja na Taasisi zake. Lengo la kupokea na kujadili taarifa hizo ilikuwa ni kutekeleza jukumu la Kibunge la kuisimamia Serikali kama inavyotajwa katika Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, baada ya kujadili taarifa hizo kwa kina, yapo masuala ambayo yalibainika na yanafafanuliwa katika Sehemu ya Pili ya taarifa hii.

1.3.3 Kutembelea na Kukagua Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kuhusu Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoishia, Kamati hili ilikagua Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa ambayo ilitengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Ziara hizo zilifanyika Mwezi Machi, 2021. Taarifa kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo ziliwasilishwa Bungeni Mwezi Aprili na Mei, 2021 kupitia Taarifa za Kamati kuhusu Utekelezaji wa Majukumu na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

1.3.4 Ziara za kukagua utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Masharti ya Fasili ya 7, Kifungu cha (1) (d) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, katika kipindi cha Mwezi Juni, 2021, Kamati ilitembelea nyumba 353 za Jeshi la Polisi zilizojengwa Kunduchi na Mikocheni Jijini Dar es Salaam kwa Ubia na Kampuni ya Mara World Tanzania Limited. Aidha, katika kipindi hicho cha Juni, 2021, Kamati ilitembelea miradi ya Jeshi la Magereza jijini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Maoni na ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa miradi iliyotembelewa yaliwasilishwa Serikalini

kupitia kwa Mheshimiwa Spika. Hata hivyo, masuala ambayo Kamati inaona yanahitaji utekelezaji zaidi, hususan kwa upande wa Jeshi la Magereza, yanatolewa Taarifa katika sehemu ya pili ya Taarifa hii.

1.3.5 Kuchambua Taarifa za Wizara kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; na makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2) ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 7(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazosimamia kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua kwa kina Bajeti za Wizara zote tatu (3) zinazosimamiwa na Kamati hii na kuwasilisha Bungeni Maoni na Ushauri wake Mwezi Aprili, na Mei 2021.

1.3.6 Kuchambua Miswada ya Sheria

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kinachotolewa Taarifa, Kamati ilishughulikia Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa Mwaka 2021 [*THE FIRE AND RESCUE FORCE (AMENDMENT) ACT, 2021*]. Kamati ilichambua kwa kina Muswada huu na kuwasilisha Bungeni Maoni na Ushauri wake¹

1.3.7 Mapitio ya Taarifa za Serikali kuhusu Mwenendo na Hali ya mtangamano wa Jumuiya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika;

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo awali, moja ya majukumu ya Kamati hii ni kushughulikia taarifa kuhusu Mwenendo wa hali ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa

Afrika. Jukumu hili limeainishwa katika Kifungu cha 7 (2) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kipindi cha Januari 2021- Februari, 2022, Kamati ilifanya mapitio ya taarifa za Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu hali ya Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika. Matokeo ya mapitio hayo yanaonekana katika sehemu ya Pili ya taarifa hii.

1.3.8 Majukumu mengine yaliyotekeliza kwa Agizo la Spika

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kinachotolewa Taarifa hii, Kamati ilielekezwa kushughulikia masuala mawili (2) kwa mujibu wa Kanuni ya 138 ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Masuala hayo ni kuhusu Uzalishaji usioridhisha wa Vitambulisho vya Taifa, na Tuhuma za Mauaji ya Wananchi watatu (3) na kupotea kwa Wananchi watatu (3) katika Kijiji cha Nyerege, Kata ya Rujewa, Wilayani Mbarali, Mbeya.

Kamati ilitekeleza shughuli hizo na kukabidhi Maoni na Ushauri wake kwa Mheshimiwa Spika.

SEHEMU YA PILI

UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

2.0 MAELEZO YA JUMLA

Mheshimiwa Spika, baada ya kuainisha majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekeliza kwa kipindi cha Januari 2021 hadi Februari, 2022, sasa naomba kutoa taarifa ya matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwenye masuala mbalimbali yaliyobainika wakati Kamati ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Kama ilivyoelezwa hapo awali, masuala yanayotolewa taarifa ni yale ambayo Kamati imebaini kuwa

changamoto zake zinahitaji kupewa umuhimu wa kipekee ili kuziwezesha Wizara pamoja na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hivyo kuleta tija kwa Taifa.

2.1 Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati

2.1.1 Umiliki wa Chuo cha Diplomasia

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Diplomasia kilichopo Kurasini Dar es Salaam kilianzishwa tarehe 13 Januari, 1978 kwa makubaliano ya nchi mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Msumbiji. Lengo kuu la kuanzishwa Chuo hiki lilikuwa ni kutoa mafunzo ya diplomasia na mahusiano ya Kimataifa kwa manufaa ya Serikali za Nchi hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipopokea Taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Chuo hiki, ilibaini kuwa kwa takribani miaka 39, Serikali ya Msumbiji imekuwa haichangii katika Bajeti ya Chuo na kushiriki katika shughuli za uendeshaji. Aidha, Nchi hiyo imesitisha kuleta wanafunzi katika Chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge la 11, Kamati hii ilishauri mara kwa mara kwamba, kwa kuwa shughuli zote za uendeshaji zinafanywa na Nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni vyema umiliki wa Chuo hicho uwe wa Tanzania pekee. Hata hivyo, umiliki wa Chuo umeendelea kuwa wa Nchi mbili.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipohoji, ilielezwa kuwa, Katiba ya Chuo cha Diplomasia imeanisha kwamba tofauti yoyote itakayotokana na Tafsiri ya Katiba au uendeshaji wa Shughuli za Chuo inapaswa kutatuliwa kwa makubaliano ya pamoja baina ya Serikali zote mbili au kupitia Tume ya Pamoja ya kudumu (JPC) ya ushirikiano ya nchi hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kamati imebaini kuwa suala hilo bado halijajadiliwa katika Tume ya pamoja ya kudumu na Wizara bado haijakutana na Serikali ya Msumbiji kujadili suala hilo.

2.1.2 Kutokukamilika kwa Sera Mpya ya Mambo ya Nje

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Hati Idhini ya Serikali (Government instruments) iliyotolewa tarehe 7 Mei, 2021, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ni mratibu mkuu wa utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 inayoweka msisitizo katika kukuza uchumi wa Nchi kuititia Diplomasia ya Uchumi.

Mheshimiwa Spika, Sera hiyo ilizinduliwa Mwaka 2001 na Rais wa Serikali ya Awamu ya Tatu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Benjamin W. Mkapa, na hivyo kuifanya Sera hiyo kufikisha miaka 20 tangu kutungwa kwake.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia ukweli kwamba Sera hiyo ni ya muda mrefu, na hivyo kuwepo kwa masuala mbalimbali yanayohitaji kufanyiwa mapitio, tangu Mwaka 2017, Kamati, katika taarifa zake za Mwaka za utekelezaji wa shughuli zake, imekuwa ikishauri Serikali kufanya mapitio na marekebisho ya Sera hiyo ili iendane na mabadiliko ya sasa yakiwemo ya kiuchumi, kisiasa, kiusalama, kijamii na kimazingira.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Shughuli za Kamati za Mwezi Agosti, 2021, Kamati ilipokea Taarifa kuhusu hatua za Maandalizi ya Sera Mpya ya Mambo ya Nje na kuelezwu kuwa Serikali inaendelea na zoezi la kuandaa Rasimu ya Sera hiyo pamoja na kueleza masuala mapya ambayo yatazingatiwa. Hata hivyo, hadi kufikia Mwezi Februari, 2022, Sera hiyo bado haijakamilika.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na juhudhi hizo zinazofanywa na Serikali katika kupata Sera Mpya ya Mambo ya Nje, Kamati imebaini kuwa kasi ya Mchakato huo hairidhishi ikilinganishwa na uhitaji wa Sera hiyo kwa mazingira ya sasa.

2.1.3 Uhaba na uchakavu wa majengo ya Balozi za Tanzania Nje ya Nchi

Mheshimiwa Spika, Balozi zetu nje ya nchi kwa muda mrefu zimekuwa zikikabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo

uhaba wa watumishi, uhaba wa vyombo za usafiri, pamoja na uhaba na uchakavu wa majengo.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi kinachotolewa Taarifa, Kamati imebaini kuwa Serikali imefanya kazi baadhi ya ushauri wa Kamati kuhusu namna ya kutatua changamoto hizo hususan katika eneo la Watumishi na Magari ya kutoa huduma katika Balozi².

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo zilizochukuliwa na Serikali, Kamati imebaini kuwa uchakavu na upungufu wa majengo Balozini bado ni changamoto kubwa. Hadi kufikia Mwezi Januari, 2022 ni Balozi nne³ (4) tu katи ya arobaini na nne (44) ambazo zina tumia majengo yake kwa ajili ya matumizi yote ya Ofisi na Makazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Serikali illoia maelezo kuwa Wizara inaendelea kutekeleza Mpango wa Ukarabati na Ujenzi wa Majengo ya Ofisi na Makazi ya Watumishi Balozini kwa lengo la kutatua changamoto ya uchakavu na upungufu wa majengo balozini, Kamati ilibaini kuwa bado fedha zinazotengwa kwa ajili ya kutekeleza Mpango huo hazitolewi kwa wakati na wakati mwingine hazitolewi kabisa.

2.1.4 Hali ya Mtangamano wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Mtangamano wa Afrika Mashariki

2.1.4.1 Hali ya Mtangamano wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipopokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu Hali ya Mtangamano wa SADC, pamoja na mambo mengine, ilibaini kuwa, Jumuiya inatekeleza hatua moja tu ya mtangamano ambayo ni eneo huru la biashara⁴.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Tanzania imeendelea kuaminika katika Jumuiya hii ya Kikanda, ambapo, pamoja na mambo mengine, Nchi yetu kupitia Bohari ya Madawa (MSD) imeteuliwa kununua dawa

za binadamu, vifaa tiba na vitendanishi kwa niaba ya Nchi wanachama baada ya kukidhi vigezo vytaalam katika Mnyonyoro wa ugavi wa dawa.

Aidha, Tanzania imenufaika katika kuuza bidhaa zake kwa nchi wanachama kwa urahisi kutokana na utaratibu wa kuondoleana ushuru.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kutumia fursa zilizopo hususan katika kusimamia vigezo vytaalam kwa bidhaa za mazao ili ziweze kuuzwa nje ya Nchi. Hii ni fursa muhimu katika kuuza uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto, kamati imebaini kuwa, pamoja na mambo mengine, kukosekana kwa miundombinu imara ya kufanikisha biashara kama vile reli na barabara kuna athiri uhusiano wa kibashara katika SADC. Kamati ilihoji mipango ya serikali ya Tanzania kuhusu kuboresha miundombinu ya Barabara na maji na kubaini kuwa Serikali tayari ipo katika mpango wa kuboresha miundombinu yake ili kurahisisha usafirishaji wa bidhaa nje ya Nchi. Kamati inapongeza jitihada hizo na kutoa rai kuwa Mpango huo upewe kipaumbele kutokana na umuhimu wake katika eneo la kuuza uchumi wa Nchi yetu.

2.1.4.2 Hali ya Mtangamano wa Afrika Mashariki

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipopokea Taarifa kuhusu hali ya Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Mwezi Februari, 2022 ilipitia hatua za Mtangamano za Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuona namna ambavyo Nchi wanachama hususan Tanzania zimenufaika katika hatua nne za mtangamano ambazo ni Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja, Umoja wa Fedha na Shirikisho la Kisiasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa katika kutekeleza hatua hizo, Tanzania imenufaika katika maeneo mbalimbali katika nyanja za kibashara, kuimarika kwa sekta za uchumi pamoja na kuimarika kwa uhusiano kati ya Tanzania na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ziara zake katika nchi za Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi ambazo zimewezesha Tanzania kufanikiwa kuondoa vikwazo nya muda mrefu na kuingia makubaliano katika Sekta mbalimbali kwa nia ya kunufaika na mtangamano huo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, Kamati ilibaini kuwa zipo changamoto za utekelezaji wa itifaki za hatua za mtangamano wa Afrika Mashariki. Changamoto hizo ni pamoja na Kasi ndogo ya Sekta binafsi kutumia fursa za biashara na uwekezaji zitokanazo na mtangamano wa Afrika Mashariki na masoko ya kimataifa.

2.1.5 Mtiririko usioridhisha wa fedha za maendeleo kwa Fungu 14 - Jeshi la Magereza Fungu 93

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipopokea Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kipindi cha Julai- Disemba, 2021 ilibaini kuwa mtiririko wa Fedha za Matumizi ya Kawaida (Mishahara na Mengineyo) kwa Mafungu⁵ yote ya Wizara hii ni mzuri. Hata hivyo, kwa upande wa mtiririko wa Fedha za Maendeleo, Kamati ilibaini kuwa Fungu 28- Jeshi la Polisi na Fungu 93- Uhamiaji, ndio yaliyopokea fedha za maendeleo ambapo Idara ya uhamiaji imepokea asilimia 67.54 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge na Jeshi la Polisi limepokea asilimia 92.5 ya fedha zizilizoishinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa, kati ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Fungu 93- Idara ya Uhamiaji, zinalenga kutekeleza miradi ambayo utekelezaji wake ulisimama kwa muda mrefu na Kamati imekuwa ikiisemea mara kwa mara tangu Bunge la kumi na moja (11). Miradi hiyo ni ya Ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Lindi, Mtwara na Geita.

Aidha, kwa Upande wa Fungu 28- Jeshi la Polisi, kamati ilibaini kuwa fedha zilizotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo,

pamoja na mambo mengine zinalenga kukarabati na kujenga vituo vya Polisi pamoja na nyumba za makazi ya askari.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kutoa fedha hizo hususan kwa ajili ya kujenga nyumba za makazi ya askari ambapo uhaba wa nyumba za makazi kwa ajili ya askari imekuwa ni changamoto ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa upande wa Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji pamoja na Fungu 29- Jeshi la Magereza, Kamati ilibaini kuwa Mafungu hayo bado hayajapelekewa fedha zozote za maendeleo ambazo ziliidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 kiasi cha Shilingi bilioni saba na milioni mia nane arobaini (7,840,000,000.00) kiliidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Jeshi la Magereza. Pamoja na mambo mengine, fedha hizo zimelelenga kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha samani Msalato, Utekelezaji wa Mpango wa kujitosheleza kwa Chakula, na ukarabati wa Mabweni ya Wafungwa.

Mheshimiwa Spika, tangu Bunge la Kumi na Moja, Kamati hii imekuwa ikiishauri Serikali, pamoja na mambo mengine, kuliwezesha Jeshi la Magereza kutekeleza mpango wa kujitosheleza kwa Chakula. Hata hivyo utekelezaji wa mpango huo umekuwa ukikabiliwa na changamoto za kibajeti kama Kamati ilivyobaini ambapo kwa kipindi cha Julai- Disemba, 2021 bado fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo (Shilingi bilioni sita) bado hazijatolewa.

Aidha kwa upande wa Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Shilingi bilioni tatu na milioni mia tano (3,500,000,000.00) ziliidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza miradi mitatu ya maendeleo. Miradi hiyo ni pamoja na Ukarabati wa Kituo cha zimamoto na uokoaji

kilichopo llala Jijini Dar es Salaam, kugharamia ununuzi wa magari mawili ya kuzimia moto kutoka Shirika la Nyumbu na Ununuzi wa vifaa vya kuzimia moto na maokozi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa tija iliyokusudiwa na Bunge ilipoidhinisha fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa Mafungu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kutokutolewa kwa fedha hizo kutaathiri mpango wa utekelezaji wa miradi hiyo.

2.1.6 Upatikanaji usioridhisha wa Vitambulisho vya Taifa

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati wa Mwezi Novemba, 2021 kuhusu hali ya upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa ulibaini kuwa, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) ilisajili watu milioni 22,682,414 hadi kufikia Mwezi Novemba, 2021 ikiwa ni asilimia 90.6 ya lengo la watu milioni 25,000,000 waliokusudiwa kusajiliwa katika awamu ya kwanza ya Mradi 2013-2015.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Kamati ilibaini kuwa kati ya idadi ya watu milioni 22,682,414 waliosajiliwa, ni watu milioni 19,131,466 ambao wamepata namba za utambulisho ikiwa ni sawa na asilimia 84.3 ya watu waliosajiliwa. Aidha, Kamati ilihoji idadi ya vitambulisho viliviyotolewa kulingana na Namba hizo za usajili tangu mradi huu ulipoanza mwaka 2013 na kubaini kuwa vitambulisho milioni 10,124,722 vilizalishwa ikiwa ni sawa na asilimia 52.9 ya Namba za Usajili zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia uchambuzi wake wa kina, Kamati iliishauri Serikali kuhusu Mikakati mbalimbali ya kutekelezwa na NIDA kwa kipindi cha Novemba 2021- Disemba 2021 ili kufanikisha zoezi la upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa kwa Wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kipindi cha Februari, 2022 Wizara iliwasilisha Taarifa ya NIDA ambayo ilieleza kuwa Serikali ilipokea ushauri wa Kamati ambapo imeanza kutekeleza mikakati hiyo ikiwa ni pamoja

na kuomba fedha Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya Utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mikakati ya Uzalishaji wa vitambulisho vya Taifa, Kamati ilibaini kuwa NIDA inatarajia kuzalisha vitambulisho milioni 7.96 hadi ifikapo mwezi Disemba 2022. Kati ya hivyo, vitambulisho milioni sita vitategemea upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, pamoja na jitihada mbalimbali zinazoendelea bado idadi ya vitambulisho vinavyokusudiwa ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji halisi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijiridhisha kuwa, pamoja na changamoto za kimkataba zinazochelewesha uzalishaji wa vitambulisho vya Taifa, bado upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Vitambulisho vya Taifa ni jambo linalotakiwa kupewa uzito wa kipekee. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Mamlaka iliomba kiasi cha Shilingi bilioni 79,757,213,204.00 na kutengewa Shilingi bilioni 11,203,453,000.00 tu. Ufinyu huu wa Bajeti umesababisha Mamlaka kushindwa kutekeleza na kufikia malengo yake kwa kiwango stahiki.

2.1.7 Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kinachotolewa Taarifa, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Taarifa ya Hali ya Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao katika kipindi cha Mwezi Julai hadi Disemba, 2021 kwa kulinganisha na hali ya ulinzi na usalama katika kipindi kama hicho Mwaka 2020. Taarifa hiyo pamoja na mambo mengine, ilibainisha hali ya uhalifu nchini na matukio yanayohatarisha hali ya usalama wa Raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa, katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa wakati idadi ya makosa dhidi ya binadamu yamepungua kwa asilimia 6.1

ikilinganishwa na Mwaka 2020, makosa ya usalama barabaran, makosa dhidi ya maadili ya Jamii yameongezeka.

Aidha, Kamati ilibaini kuwa bado kuna Msongamano wa Mahabusu na wafungwa Magerezani ambapo jumla ya mahabusu na wafungwa na magerezani ni elfu thelathini na mbili na kumi (32,010) ikiwa ni sawa na **asilimia 107 zaidi ya uwezo wa Magereza yaliyopo kwa sasa wa kuwahifadhi wafungwa na mahabusu elfu ishirini na tisa mia tisa na mbili** (29,902).

Mheshimiwa Spika, kamati ilibaini kuwa Pamoja na Serikali kuendelea kutumia adhabu mbadala kama vile mpango wa *Parole*, au kutumikia kifungo cha nje, bado wanufaika wa mpango huo ni wachache. Kwa mfano, kwa kipindi cha Julai-Disemba 2021, wafungwa 70 tu wallachiliwa huru ili kutumikia vifungo vyao chini ya mpango huo.

2.1.8 Utendaji wa Jeshi la Magereza

Mheshimiwa Spika, Mwezi Juni, 2021, Kamati ilifanya ziara katika Miradi ya Jeshi la Magereza katika Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Katika ziara hiyo, Kamati ilibaini uwepo wa Changamoto mbalimbali zinazolikabili Jeshi la Magereza na hivyo kuathiri utendaji wa Jeshi hilo. Changamoto hizo ni pamoja na:-

- i) Madeni yanayosababishwa na Taasisi za Serikali kutokulipia Huduma zinazotolewa kwao na Jeshi. Hadi kufikia mwezi Juni, 2021 Jeshi lilikuwa linadai zaidi ya Shilingi Billioni tisa (9);
- ii) Uhaba wa maafisa wa ngazi za juu pamoja na upungufu wa askari kutokana na kutokuwepo kwa ajira kwa muda mrefu;
- iii) Migogogoro ya ardhi na wakati mwingine ardhi ya Jeshi kutwaliwa na Serikali kutokana na Jeshi la Magereza kutokuwa na Hati ya Umiliki. Juhudi za upimaji zinakwama

kutokana na Jeshi kutokupatiwa fedha kwa ajili ya shughuli hiyo;

iv) Uhaba wa Magari hasa ya viongozi na ya kusafirishia mahabusu kwenda mahakamani;

v) Uhaba wa mitambo na vifaa vya kilimo kama vile matrektu na miundombinu ya umwagiliaji ili kuwezesha Jeshi hilo kuzalisha kwa ajili ya biashara.

2.1.9 Maoni kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ya Mwaka 2021;

Mheshimiwa Spika, Mwezi Agosti, 2021, Kamati ilichambua na kujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa Mwaka 2021 na kuwasilisha Bungeni maoni yake kuhusu Muswada huo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji yalilenga kuleta matokeo sita (6) yakiwemo yafuatayo:-

i) Kuimarika kwa utendaji na kuongeza ufanisi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na kutoa huduma bora kwa wananchi;

ii) Kuimarika kwa usalama wa maisha ya watu na mali zao dhidi ya moto na majanga mengine; na

iii) Kuboresha huduma za zimamoto na uokoaji zinazotolewa na Kampuni Binafsi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa matokeo yaliyokusudiwa yalilenga kuondoa mapungufu yaliyobainika wakati wa utekelezaji wa Sheria hiyo pamoja na kurekebisha Sheria nyingine ili ziendane na Marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibainisha kwamba Muswada huo ulikuwa ni wenye manufaa kwa Taifa.

Hata hivyo, ili kuwe na utekelezaji wenye tija wa Sheria hii ni muhimu Serikali ikaliwezesha Kibajeti Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kulingana na uhalisia wa mahitaji yake.

2.1.10 Kukosekana kwa Alama za Mipaka ya Nchi (Beacons);

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipopokea na kujadili taarifa kuhusu Hali ya Ulinzi na Usalama wa Mipaka ya Nchi Mwezi Februari, 2022, ilibaini kuendelea kuwepo kwa changamoto ya uharibifu wa alama za mipaka na hivyo kusababisha wafugaji kutoka katika baadhi ya nchi tunazopaka nazo kufanya shughuli za ufugaji katika maeneo ya Mipaka ambayo hayaruhusiwi kisheria.

Kumbukumbu zinaonesha kuwa changamoto hii ni ya muda mrefu na imekuwa ikiripotiwa Bungeni tangu Bunge la nane. Ni wazi kuwa tatizo hili lisiposhughulikiwa litahatarisha usalama wa Taifa.

2.1.11 Ubovu wa Barabara za Mipakani

Mheshimiwa Spika, Ubovu wa barabara za usalama mipakani umeendelea kusababisha ugumu wa kufanya doria na kudhibiti mipaka yetu kwa nyakati zote.

Mheshimiwa Spika, tangu Bunge la Kumi na Bunge la Kumi na Moja, Kamati hii imekuwa ikiishauri Serikali kuhusu umuhimu wa kutatua changamoto hii. Hata hivyo, suala hili bado halijatekelezwa kwa ukamilifu wake.

2.1.12 Matokeo ya Semina zilizofanyika

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishiriki semina na mafunzo mbalimbali katika kipindi cha Januari, Agosti, Septemba na Oktoba, 2021. Mafunzo na Semina hizo zilihusu Muundo na Majukumu ya Kamati, umuhimu wa kuzingatia tahadhari zinazohusu Ulinzi, Usalama na Diplomasia katika shughuli za Kamati, Muundo na Majukumu ya Wizara na Taasisi zinazosimamiwa na Kamati, matumizi ya Bunge Mtandao (e-

Parliament), Stratejia, Masuala ya Diplomasia na mafunzo kuhusu Mbinu na Stadi za uchambuzi wa Miswada ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, katika Semina hizo, pamoja na mambo mengine, wajumbe walijadili hatua na mbinu za kuchambua Miswada ya Sheria, na namna ambavyo Bunge linaweza kuhakikisha utekelezaji wa Diplomasia Uchumi kwa kutunga sheria rafiki kwa ukuaji wa Uchumi na kuitisha Bajeti yenye uhalisia katika kuimarishe Diplomasia uchumi.

Mheshimiwa Spika, katika semina na mafunzo hayo changamoto mbalimbali zilibainika kwenye baadhi ya maeneo na kuwasilishwa Serikalini kwa ajili ya kufanyiwa kazi. Hii ni pamoja na kuiwezesha zaidi kibajeti Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili iweze kuratibu vema masuala ya nje katika sekta mbalimbali zenyetija katika kukuza uchumi wa Taifa kama vile Sekta za kilimo, utalii, biashara na mengineyo.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 Maoni

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha matokeo ya uchambuzi wa Kamati katika Sehemu ya Pili, naomba sasa kuwasilisha maoni ya Kamati kama ifuatavyo:-

a) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;

- i) Kutokamilika kwa Sera Mpya ya Nje Mambo ya Nje kunasababisha Sera iliyopo kuendelea kutumika ilhali haiendani na kasi ya maendeleo ya kiuchumi Duniani;
- ii) Kuendelea kutumia Sera ya Nje ya Mwaka 2001 kunaathiri utekelezaji wa masuala yanayohitaji muongozo wa kisera ambayo hayajatajwa kwenye Sera ya sasa kama vile Masuala ya Diaspora na Mtangamano wa Afrika Mashariki;

- iii) Changamoto ya Umiliki wa chuo cha Diplomasia imekuwa ya muda mrefu jambo ambalo linasababisha Serikali ya Tanzania pekee kuendelea na Jukumu la kukiendesha na kugharamia shughuli zote za Chuo;
- iv) Ili kuwezesha wananchi wengi zaidi kunufaika na fursa zitokanazo na Mtangamano wa Kikanda na Mtangamano wa Afrika Mashariki, Serikali iendelee kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa zilizopo pamoja na vigezo vya bidhaa zinazohitajika katika masoko nje ya nchi;
- v) Kutokutolewa kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa miaka kumi na tano (15) wa Ukarabati na Ujenzi wa Majengo ya Ofisi na Makazi ya Watumishi katika Balozi za Tanzania nje ya Nchi kunakwamisha utekelezaji wa mpango huo;
- vi) Pamoja na nia ya dhati ya Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika Balozi za Tanzania nje ya nchi, kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kutoka Hazina kumeendelea kuwa changamoto ya muda mrefu inayoathiri utekelezaji wa miradi hiyo.

- vii) Kupeleka watumishi zaidi katika Balozi zetu, pamoja na kuongeza magari ya kutoa huduma katika Balozi zetu kunaongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Balozi hizo.

b) Wizara ya Ulinzi na JKT

- i) Kukosekana kwa alama za mipaka ya nchi (beacons) kunachangia uvamizi wa shughuli za binadamu katika maeneo hayo jambo ambalo si zuri kwa ulinzi na usalama wa nchi;
- ii) Ubovu wa barabara za mipakani unasababisha ugumu wa kufanya doria na kudhibiti mipaka ya nchi;

c) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

- i) Uhaba wa Maafisa wa ngazi za juu na Askari wa Jeshi la Magereza unaathiri ufanisi wa Jeshi la Magereza katika kutekeleza majukumu yake;
- ii) Madeni ya Taasisi za Serikali kwa Jeshi la Magereza yanakwamisha juhudzi za Jeshi katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwemo kuboresha kilimo;
- iii) Uhaba wa miundombinu ya umwagiliaji na vifaa vya kilimo kama vile matreksa, unasababisha Jeshi la Magereza kushindwa kufanya kilimo cha Biashara ambacho kingechangia katika kukuza mapato yake na mapato ya Serikali kwa ujumla;
- iv) Baadhi ya Magereza kutokuwa na Hati za Umiliki wa ardhi kunasababisha migogoro ya ardhi na wakati mwingine ardhi ya Jeshi kutwaliwa na Serikali kwa ajili ya matumizi mengine;
- v) Kutokutumika ipasavyo kwa mpango wa *Parole* na matumizi hafifu ya sheria zinazoruhusu adhabu mbadala kwa wafungwa kunachangia kwa kiasi kikubwa msongamano magerezani;
- vi) Uhaba wa vifaa na vitendea kazi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linasababisha Jeshi hilo kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;
- vii) Ucheleweshwaji wa fedha za Maendeleo kwa Fungu 14- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, na Fungu 29- Magereza kunaathiri utekelezaji wa miradi muhimu ya Majeshi hayo; na
- viii) Kutokuzalisha vitambulisho vya Taifa kulingana na malengo yaliyowekwa pamoja na kuzingatia uhalisia wa mahitaji yake kuna athiri tija iliyokusudiwa ya uzalishaji wa vitambulisho hivyo.

d) Mafunzo na Semina kwa Kamati

Upo umuhimu wa kutoa Mafunzo kwa Kamati hususan zile za Kisekta kuhusu usimamizi wa utekelezaji wa Diplomasia

Uchumi ili kuwaelimeisha na kuwakumbusha Wabunge kuhusu umuhimu wa kusimamia utekelezaji wa Diplomasia uchumi kwa maslahi mapana ya Nchi.

3.2 Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza maoni ya Kamati, naomba sasa kutoa mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo;-

3.2.1 Utekelezaji wa Mpango wa Ukarabati na Ujenzi wa Majengo ya Ofisi na Makazi ya Watumishi Balozini

Kwa kuwa Balozi takribani arobaini za Tanzania nje zinapanga majengo kwa ajili ya Ofisi na makazi kutokana na kutokuwa na majengo aidha majengo ya Balozi hizo kuwa yamechakaa;

Na kwa kuwa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa jili ya kutekeleza Mpango wa Miaka kumi na tano (15) wa ujenzi na ukarabari wa majengo ya ofisi na Makazi ya Watumishi Balozini hazitolewi kwa wakati na mara nydingine hazitolewi kabisa;

Na kwa kuwa kutokutolewa kwa fedha hizo kunasababisha Serikali kuendelea kupoteza fedha nydingi kwa ajili ya kulipia pango;

Hivyo basi, Bunge linaishauri Serikali kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kila mwaka ili kuwezesha utekelezaji wa Mpango huo kwa maslahi mapana ya Nchi.

3.2.2 Kutokukamilika kwa Sera Mpya ya Mambo ya Nje

Kwa kuwa, kwa kipindi cha miaka mitano tangu Mwaka 2017, Kamati imekuwa ikishauri Serikali kufanya Marekebisho Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001;

Na kwa kuwa, Msingi wa Ushauri huo ulijikita katika ukweli kwamba Sera hiyo ni ya muda mrefu na hivyo kuhitaji

kufanyiwa mapitio ili iendane na mabadiliko mbalimbali ya kiuchumi, kijamii na kisiasa katika kipindi chote tangi itungwe;

Na kwa kuwa, Marekebisho yanayotarajiwa kufanyika ni pamoja na kuingiza masuala ya Diaspora na Mtangamano wa Afrika Mashariki ili yapate muongozo wa Kisera;

Kwa hiyo basi, Bunge linaishauri Serikali iongeze kasi ya maandalizi ya Sera ya Mambo ya Nje ili ianze kutumika rasmi mara moja.

3.2.3 Makosa dhidi ya Maadili ya jamii

Kwa kuwa makosa dhidi ya maadili ya Jamii ikiwemo matumizi ya dawa za kulevyia yameongezeka kwa asilimia 29.2 ikilinganishwa na Mwaka 2020 kwa kipindi cha Julai- Disemba;

Na kwa kuwa makosa haya yakiendelea kuongezeka yanachangia pia ongezeko la makosa dhidi ya binadamu ikiwemo mauaji, kubaka, na kulawiti, hali ambayo si nzuri kwa usalama wa raia;

Hivyo basi, Bunge linaishauri Serikali kuwa na Mpango Mkakati wa kupunguza makosa dhidi ya maadili ili kupunguza matukio ya makosa dhidi ya binadamu ambayo yanaleta taruhuki katika jamii na kuathiri usalama wa raia ambao ndio nguzo muhimu ya maendeleo.

3.2.4 Hali ya msongamano wa Mahabusu na Wafungwa Gerezani

Kwa kuwa uwezo wa magereza yaliyopo nchini ni kuhifadhi wahalifu 29,902 kwa siku, na hadi kufikia Mwezi Disemba, 2021 idadi ya wafungwa na mahabusu ilikuwa ni 32,010 ikiwa ni sawa na asilimia 107 zaidi ya uwezo wa Magereza yaliyopo;

Na kwa kuwa tatizo la msongamano ni kubwa zaidi katika magereza ya mahabusu ambao wanasubiri maamuzi ya kesi zao mbalimbali;

Na kwa kuwa Kamati inatambua kuwa jukumu la kupunguza Msongamano Magerezani linajumuisha Taasisi mbalimbali;

Hivyo basi, Bunge linaishauri Serikali:-

- i) lendelee kutenga na kutoa fedha kwa ajili ya kujenga na Magereza katika Mikoa na Wilaya zisizokuwa na Magereza pamoja na kukarabati mabweni yaliyochakaa na kuongeza mabweni katika Magereza ambayo bado yana nafasi ili kuhimili uhifadhi wa wafungwa na mahabusu;
- ii) Isimamie Kamati za Kusukuma kesi kukutana mara kwa mara ili kumaliza changamoto ya ucheleweshwaji wa kesi mahakamani;
- iii) Ihakikishe upelelezi wa kesi hususan zile ambazo si za jinai, hauchukui muda mrefu;
- iv) lendelee kutumia Mpango wa *Parole* kwa Wafungwa wengi wanaokidhi vigezo vya kutumikia vifungo vya nje chini ya mpango huo; na
- v) Kutoa adhabu mbadala kwa wafungwa wasiokuwa tishio kwa usalama wa raia.

3.2.5 Hali ya upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa

Kwa kuwa uzalishaji wa vitambulisho vya Taifa umeendelea kuwa changamoto ya muda mrefu na hivyo kufanya upatikanaji wa vitambulisho hivyo kuwa chini ya lengo tangu kuanza kuzalishwa kwake Mwaka 2013;

Na kwa kuwa Raia kutokuwa na vitambulisho vya Taifa kunaathiri upatikanaji wa huduma mbalimbali zinazohitaji raia kuwa na vitambulisho vya Taifa kama vile kupata Passport mpya;

Hivyo basi, ili kuwezesha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa kuzalisha vitambulisho kwa wakati na kulingana na malengo

yaliyowekwa pamoja na uhitaji halisi wa vitambulisho hivyo, Bunge linaishauri Serikali:-

- i) Kutenga fedha za maendeleo kulingana na mahitaji halisi ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ikiwa ni pamoja na kutengewa fedha za kutosha kwa ajili ya manunuzi ya kadi ghafi na ununuzi wa vyombo vya usafiri;
- ii) Kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati kwa ajili ya uzalishaji wa vitambulisho vya Taifa;
- iii) Kuwa na Mkakati wa kuboresha vitendea kazi vya kiteknolojia kama vile *Computers* na *Software* mbalimbali ili kwenda sambamba na kasi inayokusudiwa ya uzalishaji wa vitambulisho vya taifa.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Shukrani

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati kuhusu utekelezaji wa shughuli zake kwa kipindi cha Januari, 2021 hadi Februari, 2022. Ni imani ya Kamati kuwa fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 136 (15), ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 itasaidia kuliwezesha Bunge lako Tukufu kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. George Simbachawene, (Mb), na Naibu Waziri wake Mhe. Khamis Hamza Khamis, (Mb) kwa ushirikiano waloutoa kwa Kamati hii walipokuwa na dhamana ya Wizara hii.

Aidha, kipekee namshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani wa sasa Mhe. Eng. Hamad Masauni, (Mb), pamoja na Naibu Waziri wake Mhe. Jumanne Sagini (Mb) kwa ushirikiano

walioutoa kwa Kamati katika kipindi kifupi ambacho Kamati imefanya kazi nao.

Vilevile, namshukuru Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mhe. Stergomena Tax, (Mb) na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Balozi Liberatha Mulamula, (Mb), na Naibu Waziri wake Mhe. Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk (Mb) pamoja na watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini si kwa umuhimu, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc*, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, *ndc* Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magilli, Makatibu wa Kamati Ndg. Ramadhan Abdallah, Bi. Grace Bidya na Bi. Victoria Mizengo wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vema shughuli za Kamati kwa kipindi chote cha Mwaka mzima na hata kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza shughuli zilizoteklezwa, Uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, Maoni na Mapendekezo sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee, kujadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

.....
Mussa Azzan Zungu, Mb

MWENYEKITI

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO
YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

Februari, 2022

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Vita Kawawa kwa kuwasilisha Taarifa hii muhimuya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuzisikiliza taarifa hizi mbili za Kamati, tutaanza mjadala utakaokuwa unahu Kamati zote mbili. Tutaanza na Mheshimiwa Cosato David Chumi, atafuatiwa na Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga ajiandae.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa hoja ambayo imewasilishwa mezani. Nitajielekeza kwenye hoja ya Kamati ya Ulinzi, Mambo ya Nje na Usalama.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanza napenda kutumia nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Mafinga Mjini, kukupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge letu. Mwenyezi Mungu akusimamie na kukuongoza; hizi ni salamu ambazo nimetumwa na Wanamafinga nizifikishe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya salamu hizo, kama mara zote ambavyo huwa nasema kwamba, Mheshimiwa Rais ndio mwanadiplomasia namba moja. Pale anapokuwa amefanya kazi ametimiza majukumu yake kama mwanadiplomasia namba moja, tunao wajibu wa kumpongeza na kumtia moyo. Mimi sitaishia tu kumpongeza na kumtia moyo, lakini nitafanya na takwimu kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na kazi nzuri ya diplomasia, kama mwanadiplomasia namba moja ambayo Mheshimiwa Rais anaifanya, nchi yetu imeendelea kupata

fursa mbalimbali za kibiashara, hasa katika eneo letu la afrika Mashariki, lakini na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, hapa unipe ruhusa nitoe takwimu kidogo tu; kutokana na kazi nzuri anayoifanya Mheshimiwa Rais, biashara kwa maana ya *trade balance* kati yetu sisi na Kenya, kwa mara ya kwanza tumefanya vizuri sana katika kipindi cha Januari mpaka Septemba, 2021. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwa takwimu kibiashara, mauzo yetu katika nchi Jirani ya Kenya, kama wenzetu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na hii naitoa kulingana na takwimu za ile *Kenya National Bureau of Statistics* kwamba, mauzo yetu yameongezeka kutoka dola za kimarekani milioni 347 sawasawa na bilioni za Kitanzania 802 mpaka dola za kimarekani milioni 396, sawasawa na fedha za Kitanzania bilioni 915.

Mheshimiwa Spika, hili ni ongezeko kubwa na ni ongezeko ambalo mara nyingi, *trade balance* kati yetu sisi na wenzetu, wenzetu wamekuwa wakituzidi, lakini kutokana na kazi nzuri ambayo Mheshimiwa Rais, kama mwanadiplomasia namba moja ameifanya, tunaona sasa kama Taifa letu na sisi *trade balance* kati yetu sisi na majirani zetu sasa inaendelea kukua. Kwa hiyo, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu, kama Kamati tulikuwa na kilio cha muda mrefu na kuishauri Serikali kupeleka maafisa katika balozi zetu, ili waendelee kutafuta fursa za kiuwekezaji, fursa za biashara na fursa mbalimbali za kiuchumi kwa ajili ya Taifa letu. Ninapozungumza hapa Wizara imefanikiwa kupeleka maafisa 137 katika balozi zetu 44 ambaao ni sawa na wastani wa asilimia 63% kati ya maafisa 215 wanaohitajika. Hii ni hatua kubwa ambayo itaenda kuongeza ufanisi katika balozi zetu, itaenda kuongeza utendaji na zaidi ya yote kung'amua zaidi fursa za kiuwekezaji na hivyo kuliongezea Taifa letu mapato zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, kama ambavyo tumesema katika Kamati yetu, bado kuna shida kubwa ya uchakavu wa majengo na uhaba wa majengo katika balozi zetu. Kama taarifa yetu ilivyojonesha ni Balozi nne tu za Cairo, Lusaka, Maputo na Harare ndizo ambazo maafisa wetu au Serikali yetu ina majengo kwa maana ya ofisi na ina majengo kwa maana ya makazi ya maafisa wetu wa ubalozi.

Mheshimiwa Spika, jambo hili linaifanya Serikali kubeba mzigo mkubwa sana wa kugharamia pango kwa ajili ya ofisi na pango kwa ajili ya makazi ya maafisa wetu na hivyo kuwa ni mzigo mzito sana kwa Serikali. Ndio maana Kamati yetu imekuwa ikishauri na inaendelea kushauri kwamba, Serikali kwa maana ya Hazina, waweze kutoa fedha ili ule mpango mkakati ambao Wizara ya Mambo ya Nje imejjjengea au imejjiwekea wa miaka 15 wa kuondokana na kupangisha na kukodi majengo ya ofisi na makazi ambayo hata kiusalama sio nzuri sana, basi uweze kutimia, lakini utatimia ikiwa tu wenzetu hawa watapatiwa fedha kama ambavyo Kamati imeelekeza.

Mheshimiwa Spika, hapa nitatoa mfano mdogo. Kwa mfano, katika Ubalozi wetu wa Marekani, pale Washington DC, tuna jengo ambalo ikiwa Serikali itatoa fedha kiasi cha bilioni 3.8 likakarabatiwa, maana yake ni kwamba, lile jengo ambalo tunalitumia sasa hivi tutahama na hivyo, lile jengo tunalolitumia sasa hivi tutalipangisha na kwa mwaka tutapata wastani wa bilioni 2.4. Kwa hiyo nitoe wito na ushauri kama Kamati ambavyo imesema tukitoa fedha hizi kwa Wizara tukakarabati majengo maana yake kwanza tutaokoa fedha ambazo tunapanga sasa, lakini pili, tutazalisha mapato zaidi kwa ajili ya kuendeshea shughuli zingine za Serikali.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano mdogo. Kwa mfano, katika Ubalozi wetu wa Marekani, pale *Washington DC*, tuna jengo ambalo, ikiwa Serikali itatoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 3.8 likakarabatiwa, maana yake ni kwamba, lile jengo ambalo tunalitumia sasa hivi tutahama na kulipangisha na kwa mwaka tutapata wastani wa shilingi bilioni 2.4.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo natoa wito na ushauri ushauri kama Kamati ambavyo imesema, tukitoa fedha hizi kwa Wizara, tukakarabati majengo, maana yake kwanza tutaokoa fedha ambazo tunapanga sasa, lakini pili, tutazalisha mapato zaidi kwa ajili ya kuendeshea shughuli nyingine za Serikali. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili katika Kamati yetu ambalo tumeliona, tulikuwa tumeshauri kwamba Magereza wajitosheleze kwa chakula. Tunapozungumza hivi sasa, Magereza kutoptaka na kazi nzuri wanayofanya, wameokoa takribani shilingi bilioni 11 ambazo zilitokana na kuwalipa wazabuni kwa ajili ya chakula kwa wafungwa na mahabusu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wetu kama Kamati na mimi kama Mjumbe wa Kamati, ninashauri ili Magereza iweze kujilisha na kuzalisha ziada, basi kile ambacho kinakuwa kimepangwa na Serikali katika bajeti, fedha zile ziende. Sambamba na kuwapa fedha ambazo zitawasaidia kuwa na uwezo katika kujenga miundombinu ya umwagiliaji, pia Jeshi la Magereza tunapozungumza hivi sasa ukiacha yule Mkuu wa Magereza (*Commissioner General of Prison*) ambaye kimuundo anatakiwa kuwa na wasaidizi wanne, hana hata msaidizi mmoja. Pia kimuundo kuna ma-*Deputy* ambao wanatakiwa kuwa kama 17, lakini yuko mmoja tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni wakati wa Serikali sasa kuliwezesha Jeshi la Magereza kifedha na nyenzo ili liweze kuzalisha kwa ajili ya kujilisha kama ambavyo wameokoa hizo shilingi bilioni 11, lakini pia waweze kuzalisha kwa ajili ya ziada. Haya yatawezekana ikiwa tu tutawapa fedha, na ile ikama yao kwa maana ya muundo wao yule Mkuu wa Magereza, apatiwe wasaidizi wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kutoptaka na muda, naomba kuwasilisha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Kamati. (*Makofij*)

SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa sijasema; wachangiaji kutoka Chama cha Mapinduzi wanachangia kwa dakika saba kwa kila Mbunge. Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendecka atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga na Mheshimiwa Emmanuel Lekishoni Shangai, ajiandae.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi ya kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nachukua nafasi hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Amiri Jeshi Mkuu na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, kwa jinsi anavyoliongoza Taifa letu kwa viwango ambavyo kila mtu anakiri na kazi yetu ni kuendelea kumwombea kwa Mwenyezi Mungu, ampe afya njema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwa kura zote na Bunge hili la Jamhuri ya Muungano kuwa Spika wa Bunge letu. Hakika Mbeya imetupa mtu, hakika Magufuli alimwona mtu makini, hakika aliyekuteua kuingia kwenye Bunge la Katiba aliona mbali na leo Watanzania watashuhudia uwezo wako katika kipindi cha uongozi wako. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, nisiwe mwizi wa fadhila, niwapongeze Wabunge ambaao wamepata dhamana ya kuaminipa na Rais kwa nafasi mbalimbali; nampongeza Mheshimiwa Shangai kwa kuchaguliwa na wananchi wa Ngorongoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu sasa kwanza kwa kuwashukuru waliowasilisha taarifa za Kamati zote mbili, lakini nianze na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Mtakumbuka tumekuwa na mgogoro wa muda mrefu kati ya wananchi au watumiaji wa ardhi na Hifadhi zetu za Taifa kwa muda mrefu; na Rais wa Awamu ya Tano aliunda Kamati ya Makatibu Wakuu na Mawaziri na baada ya kazi kukamilika, alisema maamuzi yatatolewa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alisema kazi inaendelea, alitekeleza uamuzi huo kwa kufanya uamuzi wa haraka na kwa muda mfupi sana aliweka historia ya kuwatuma Mawaziri wapatao nane kuzunguka nchi nzima kutoa maamuzi ya Serikali ya kilio cha muda mrefu cha wananchi wa maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri hawa wanane wakiongozwa na Mheshimiwa Lukuvi, wakati huo akiwa Waziri wa Ardhi, walifika Jimbo la Simanjiro kutokana na mgogoro uliokuwepo kati ya Kijiji cha Kimotoro kwa upande mmoja na Pori la *Mkungunero Game Reserve* kwa upande mwingine; na pia kushughulikia mgogoro uliokuwepo kwa Vijiji nya Wilaya ya Kiteto kwa maana ya *Erikiushi*, Bwawani na Katikati, lakini kushughulikia pia mgogoro ulioko kati ya Mkungunero na Jimbo la Kondoa Vijijini la Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji na maamuzi yale yalitangazwa na wananchi walipata faraja na hakika walimsifu sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kinachoshangaza mpaka sasa, baada ya maamuzi na maelekezo ya Rais ambayo yalikuja kutamkwa na Mawaziri, watendaji na wataalam walioambiwa wafanye kazi hiyo, mpaka sasa wameshindwa kukamilisha kazi hiyo kwa sababu wanazozijua wao wenyewe. Ombilangu kwa Waziri Mkuu na kwa Serikali, wale waliotumwa kufanya kazi hiyo wakamilishe haraka ili wananchi...

SPIKA: Mheshimiwa Ole-Sendeka, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Venant.

TAARIFA

MHE. VENANT D. PROTAS: Mheshimiwa Spika, mchangiaji anaongea vizuri sana juu ya Mawaziri hawa, lakini nataka nimpe taarifa kwamba kweli walitumia fedha nyingi kuzunguka kuja kutatua migogoro hii, lakini cha ajabu wataalam waliachiwa hili jukumu la kusaidia kutatua migogoro hii, wenyewe wanasema wanahitaji maelekezo kutoka kwa wahusika kwa barua. Kwa hiyo nampa taarifa

kuwa Serikali sasa ipeleke maelekezo kwa barua ili sasa migogoro hii iweze kwisha.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Christopher Ole-Sendecka.

MHE. CHRISTOPHER O. SENDEKA: Mheshimiwa Spika, napokea taarifa yake na ninaungana naye kuiomba Serikali ifuatilie kazi ambayo watendaji walipewa ya kuhakikisha kwamba wanamaliza mgogoro huu ili ahadi ya Rais iweze kuwa ni ya kweli kama alivyoahidi mwenyewe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, niende sasa katika suala ambalo ninaliomba Bunge hili lijipe muda wa kuungana na Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kupata muda wa kulitafakari, nalo ni suala la mgogoro uliopo katika maeneo mawili ya Wilaya ya Ngorongoro. Kwanza Tarafa ya Ngorongoro yenye kilometa za mraba 8,000 eneo ambalo kuna maisha mseto kati ya wanyamapori, binadamu na mifugo inayofugwa na binadamu ambayo imeanza mwaka 1959.

Mheshimiwa Spika, mgogoro mwingine ni katika eneo la kilometa 1,500 za Tarafa za Loliondo ambayo inatakiwa ifanywe kuwa ama *Game Reserve* au *Game Control Area*. Jambo hili ni vizuri sana Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania likaelewa, likapata muda wakati Serikali inafanya tathmini, Bunge lako likapeleka Kamati ya kuyajua mambo haya. Kwa sababu upotoshaji unaoendelea kufanywa na baadhi ya vyombo vya habari na upotoshaji unaofanywa na *social media* hakika hauwatendei haki wananchi wa Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba ninukuu maneno haya ya gazeti la Jamhuri la tarehe 1 mpaka 7 Februari, linasema hivi: "*Loliondo na Ngorongoro kwa ujumla wake ni za Watanzania. Hivyo sote tuna wajibu wa kuona ikiendelea kuwepo ili iwe na manufaa kwa Watanzania na walimwengu wote. Haiwezekani kabila moja katika nchi likatae kutii mipango ya Serikali hasa ikizingatiwa kuwa*

kinachofanywa na dola kina manufaa makubwa kwa Umma na kwa nchi.” (Narudia), “*haiwezekani kabilia moja likatae kutii.*” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, lugha hii siyo njema hata kidogo. Haiwezekani! Unaposema haiwezekani kabilia moja; wanaosemwa hapa, walioko Loliondo na Ngorongoro ni kabilia moja linaloitwa Wamasai. Wamasai hawa wamekuwa waungwana kwa uhifadhi. Kama kuna kabilia lililoonesha uhifadhi bora na kuweza kuishi na wanyama katika eneo moja bila kuwadhuru ni Tarafa ya Ngorongoro katika Wilaya ya Ngorongoro ambalo wengi wa wananchi wanaoishi hapo ni Wamasai.

Mheshimiwa Spika, wananchi hao hao walitoa ardhii yote ya Serengeti, Tarangire, Ngorongoro na *Lake Manyara*. Leo unapozungumza kilometra za mraba 1,500 ambayo Mheshimiwa Waziri Pinda aliundia Tume na baada ya Tume ye ye mwenyewe alikwenda; CCM iliunda Tume iliyoongozwa na Dkt. Mwigulu Nchemba, nami nilikuwa Mjumbe wake tukaleta taarifa. Waziri Mkuu wakati huo Mheshimiwa Mizengo Pinda akaenda Loliondo akatoa tamko la Serikali, juu ya msimamo wa Serikali kuhusu eneo la Loliondo na msimamo wa Serikali kuhusu eneo la Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, Wakati huo huo Rais wa Awamu ya Nne Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, baada ya kelele kuendelea alisema hivi akiwa kwenye matibabu; na haya ni maneno yake naomba ninukuu kwa ruhusa yako. Haya ilikuwa ni tarehe 23 Novemba, 2014.

Mheshimiwa Spika, nami naomba ninukuu kwa sababu aliandika kwenye *twitter* yake kwa Kiingereza: “*There has never been, nor will there ever be, any plan by the government of Tanzania to evict the Maasai people from their ancestral land.*” Mwisho wa kunukuu. Haya ni maneno ya Rais wa Awamu ya Nne. Baada ya kelele za waandishi wa habari kutumia *social media* na kutumia magazeti yao kutuma ujumbe usio mzuri kwenye ulimwengu mzima.

Mheshimiwa Spika, hata leo naungana na Kamati, wanaposema mfumo wa matumizi bora ya ardhi, usimamizi hafifu ndiyo unapelekea tishio hilli lilioko Ngorongoro. Nataka nikwambie, magazeti haya ambayo nilikuwa nakukuu ambayo ni mengi, ninayo hapa, yalikuwa ni matokeo ya semina iliyoanywa na Dkt. Fredy Manongi, Kamishna wa Uhifadhi wa Ngorongoro kwa kuwaita Wahariri wa Habari ili watoe picha wanayoitaka wao na huku wanasaahau kwamba hata *log* yao Mamlaka ya Ngorongoro ina kichwa cha Faru, ina picha ya ng'ombe hapa, kuonyesha kwamba Ngorongoro ni kwa ajili ya wafugaji wa uhifadhi. Hata hivyo, anasaahau *section 6* ya sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Ngorongoro inasema hivi, naomba ninukuu tena ili hawa wenzetu waelewe kwamba walioko Ngorongoro hawako kwa ajali. Inasema hivi:-

"The functions of the authority shall be to conserve and develop the natural resources of the conservation area;" ya pili, anazungumza: *"to promote the tourism; na ya tatu: "to safeguard and promote the interest of Maasai citizens of the United Republic."* Hayo ndiyo malengo makuu matatu.

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo kwa sababu ujumbe wenywewe umefika, lakini kwa kukuomba na wewe utupe muda, isaidie Kamati hiyo iende Ngorongoro, ikae na wananchi wa Loliondo na wananchi wa Tarafa ya Ngorongoro. Serikali nayo iunde Tume yake, tutekeleze maelekezo ya Mheshimiwa Rais, amewaambia wasaidizi wake, nendeni mkakae na viongozi wa mila...

SPIKA: Mheshimiwa Ole-Sendeka, dakika moja, malizia.

MHE. CHRISTOPHER O. SENDEKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa dakika moja.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo kwamba viongozi wa Serikali wakakae na viongozi wa Ngorongoro, wakae na viongozi wa mila wa Ngorongoro ili watafute ufumbuzi wa namna ya kuendelezwa kwa ufugaji

na uhifadhi katika eneo la Ngorongoro. Ninachoomba Serikali isimamie maelekezo ya Rais kama alivyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuichangia hoja hii. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, Mheshimiwa Hassan Selemani Mtenga ajiandae.

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye taarifa hizi za Kamati na niungane na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kwa kuanza kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita iliyo chini ya Mama Samia Suluhu Hassan, maana hata kule Jimboni kwangu Ludewa kila kona ambako wananchi wapo, kuna miradi ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, halikadhalika niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, naye nimkumbushe kwamba ana ahadi na wananchi wa Ludewa na wanamsubiri sana kule. Ziara yake ameshaahirisha mara nne, kwa hiyo, wananchi wameniomba sana niweze kumkumbusha, wana hamu naye sana, wanataka aende akashuhudie kazi nzuri ambazo Rais wetu amefanya ikiwemo daraja la Ruhuhu, barabara ya zege na mambo mengine lukuki. Nashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, halikadhalika nakupongeza kwa kuchaguliwa. Nami binafsi nikiri kwamba nakufahamu tokea *Law School* ukiwa mwalimu wangu *Cohort* ya 12. Kwa kweli Mwenyezi Mungu amekupa karama nyingi, naamini hata Bunge hili litaenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache nirudi sasa kwenye hoja mahususi ambapo ningependa kuanza kuchangia kwenye Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Nimemksiliza *RC* wangu wa zamani wa Mkoa wa Njombe, Mheshimiwa Ole-Sendeka, amezungumzia hoja ya Ngorongoro ambayo vilevile imekuwa ikijadiliwa sana kwenye

vyombo mbalimbali nya Habari. Wako ambao wanasema kwamba wananchi waendelee kuwepo vilevile kwa sababu ni aina ya pekee ya utalii; watu, mifugo na wanyama wa asili, lakini wapo ambao wanaona kwamba ongezeko la mifugo kama ng'ombe, kondoo, mbuzi na wanadamu inaharibu ekolojia ya eneo lile na wanyama wale walikwenda pale kwa sababu za kiasili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hata tukisoma maandiko matakatifu tutaona kwamba Mwenyezi Mungu baada ya kuumba mbingu, ardhi, wanyama, ndege ndiyo akamuumba mwanadamu. Kwa hiyo, tuna jukumu vile vile la kutunza hizi maliasili. Ila hoja ya mahususi na ya msingi ni kwamba tunavyoshughulikia mambo haya kama alivyoongea Mheshimiwa Ole-Sendeka, tuweze kuzingatia haki za binadamu, kwamba Serikali inavyotekeleza wajibu wake wa kulinda hifadhi ile ambayo iko kwenye urithi wa dunia, Hifadhi ya Ngorongoro, ni sharti na ni muhimu sana kuheshimu haki za binadamu. Tunapowahamisha wale watu, lazima tuangalie sheria zinasemaje kuhusu haki za binadamu? Zikoje? Vile vile kuwe na ushirikishwaji wa hali ya juu.

Nimemuona Mheshimiwa amesitisiza zaidi ushirikishwaji kwa hiyo hoja zote ni za msingi lakini ile Hifadhi ya Ngorongoro ambayo ina sheria yake, Sura ya 284 na Kifungu cha 6 kama alivyokinukuu, kinaelezea majukumu ya ile mamlaka ya uhifadhi wa Ngorongoro. Kwa hiyo, mamlaka ile ilikuwa na majukumu ambayo imepewa na sheria na ilikuwa na wajibu wa kuyasimamia. Kwa hiyo, watu walikuwa wanaongezeka tunaangalia, lakini sasa tunavyotaka kuilinda ile Hifadhi tuzingatie haki za binadamu, lakini hoja ya ile hifadhi kuendelea kuwepo ni muhimu sana ikapewa kipaumbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, halikadhalika kwenye Kamati yetu tuliona kwamba Serikali imewekeza fedha nyingi sana kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere na takribani shilingi trilioni 6.5 zimewekezwa pale na asilimia siyo chini ya 60 ya maji yanatokana na bonde la Mto Kilombero. Kwa hiyo, na kwenyewe ni muhimu sana Serikali ikachukua hatua za

haraka pasipo kuathiri haki za binadamu. Wale wananchi wote ambaao wanafanya shughuli zinazoathiri ustawi wa bonde hili la Mto Kilombero na kuathiri uwepo wa maji ya kutosha yatakayoenda kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, kwa kweli ni vizuri Serikali ikachukua hatua za haraka bila kuathiri haki za binadamu. Ninavyosema haki za binadamu, nafikiri ni neno ambalo ni pana kidogo.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika tukija kwenye masuala ya utalii, huku Nyanda za Juu Kusini kuna vivutio vingi sana nya utalii, kule Jimboni kwangu Ludewa, Ziwa Nyasa kuna samaki wa mapambo, kuna milima ya *Livingstone*, ingawa bahati mbaya kuna Kata nne pale haziflikiki kwa gari; Kata ya Lumbila, Kata ya Kilondo, Kata ya Makonde na Kata ya Lifuma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika zile safu za milima ya *Livingstone* kuna nyani wale wakubwa, wazuri, ni kivutio kizuri cha utalii. Pia kuna miamba ile ya Ziwa Nyasa na Kitulo kule kwa Mheshimiwa Festo Sanga, Makete. Kwa hiyo, vivutio ilikuwa ni vizuri vikatambulika na Wizara hii ya Maliasili na kuweza kukuza utalii wa Nyanda za Juu Kusini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, halikadhalika kuna ngoma za asili. Mheshimiwa Naibu Waziri tulimpelekea ngoma moja ya Mganda ya Boma la Mtumbati, kulikuwa na tukio la watu wa Makete. Alivutiwa sana na ile ngoma, mavazi yao wanavaa kaptura nyeupe na shati jeupe. Ngoma ile kwa kweli ni kivutio kizuri sana na muhimu cha utalii. Pia kuna ngoma nyingine kama Ngwaya, Matuli; hata vyakula nya asili. Kwa hiyo, ni vizuri Wizara hii ikitambua vitu vile na kuviingia kwenye mradi wa *regrow*, itasaidia sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikirejea kwenye Wizara ya Ardhi, Wizara hii inafanya kazi kubwa sana na sasa hivi wamewekeza sana kwenye mifumo ya kielektroniki; Teknolojia Habari na Mawasiliano kuna mfumo unaitwa *Landrent Management System*, kuna mfumo unaitwa *Molis* na mifumo mingine mingi. Mifumo hii kwa kweli inasaidia sana katika kuongeza ufanisi. Isipokuwa Wizara hii inakabiliwa na

upungufu mkubwa sana wa wafanyakazi. Takribani wafanyakazi 2,000 wanahitajika waongezeke. Kwa hiyo, Wizara hii langaliwe kwa jicho la karibu ili isaidie kupunguza migogoro.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai, atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga na Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba ajiandae.

MHE. EMMANUEL L. SHANGAI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na binafsi nikupongeze kwa sababu najua umechaguliwa siku ile nami nikaapishwa; kwa hiyo mimi ni Mbunge wako uliyemuapisha katika Wabunge wote waliopo kwenye Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, pia niipongeze Kamati kwa taarifa yao nzuri. Hata hivyo nitoe taarifa kwenye Bunge lako Tukufu kwamba eneo la Ngorongoro haliwezi kufa, kwa sababu wananchi walioko katika Eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ni wananchi ambao ni wahifadhi namba moja tofauti na wahifadhi wa vitabu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wananchi waliopo Tarafa ya Ngorongoro au Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ambayo inaongozwa kwa mfumo wa ardhi mseto ni wananchi ambao katika eneo hilo wameishi miaka 60 bila kula wanyama na bila kuwa wawindaji. Wananchi hao sasa hivi tukiona kwenye vyombo vyaya habari wako *very victimized*, wanaitwa ni majangili, ni watu maskini ndani ya Tanzania, *as if* kwamba kuna omboomba katika eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, kuna vyombo vyaya habari ambavyo sasa hivi kila siku ni kuandika kuhusiana na eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, kwamba wananchi sasa hivi ni tatizo. Nadhani Serikali kwanza ingewatambua wale wananchi kama wahifadhi waliohifadhi kwa niaba ya

wananchi wengine milioni 60 wa Tanzania, lakini si kuwaona kama tatizo.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa kwamba, kwenye eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro watoto wanakwenda shule, si kama inavyotangazwa kwenye vyombo vya habari vya akina Kitenge. Kule kwetu kuna shule za msingi 30 na watoto wanakwenda shule; kuna vituo vya afya, kuna zahanati, kuna maendeleo mengine ambayo Watananzia wengine wanayo. Kama imefika sehemu tunaona labda ni tatizo, mheshimiwa Rais tarehe 16 mwezi wa Kumi, akiwa Arusha alisema kwamba ni lazima tukae na wananchi ili tutafute suluhu ya changamoto zilizopo katika eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niishauri Kamati pamoja na Wizara, kwamba ni lazima kukaa na wale wananchi. Kwa hali ilivyo kwa sasa, kumekuwa na *enmity* kubwa sana kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na wananchi waliopo ndani ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro; huku tukijua kwamba wananchi hao wako kisheria, hawajavamia. Wale wananchi walikuwepo na waliingia mkataba na mkoloni mwaka 1959 wakati walipofanya makubaliano kutoka Moru – Serengeti kutoka mwaka 1918 mpaka mwaka 1948, ndipo wananchi wale wakaamua kuhama kutoka Serengeti na kuja katika maeneo ya *higher land* ambayo ni Ngorongoro ya sasa (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunawaona wale wananchi kama ni wananchi ambao ni wavamiaji. Hao waandishi wa habari wa mitaani, anatoka mtu anasema nimesafiri kilometra 400 kumtafuta tembo Ngorongoro, hiyo si kweli. Ngorongoro tembo wako njiani kwa wale waliokwenda na ni wapi katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro unaweza ukasafiri kilometra 400 katika eneo la *square kilometer* 8,100? Hakuna. Sehemu ya mbali ni Nayobi ambayo ni kilometra 80 na sehemu nyingine ni Kakensiya ambayo ni kilometra 75, hakuna sehemu unayoweza ukatembea hivyo. Kwa hiyo, niombe, kwanza, Serikali iingilie kati utumiaji wa vyombo vya

habari kwa ajili ya kuwaonesha wananchi wale kama hawafai.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ole-Sendeka amesoma lile gazeti. Ukitosha kama mwananchi uliye Ngorongoro, ukaona jinsi unavyoandikwa, unaishi na wanyama, unaishi na pofu, unaishi na wanyama wote na pundamilia, wanalala mpaka bomani, lakini unaonekana kama mtu ambaye hufai. That is totally haihitajiki katika maisha haya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi ni...

TAARIFA

SPIKA: Mheshimiwa Olelekaita

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge wa Ngorongoro kwamba sheria nchi hii hairuhusu kabisa aina ya *reporting* iliyofanyika na magazeti hayo na kwamba kuna *regulation* inaitwa *The Electronic and Postal communication (online contempt regulation, 2018)* inakataza aina ya *publication* inayo-cause public disorder, bad language, discouraging, abuse na calculated words to offend a particular group ya watu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo sheria za nchi zinakataza na ni suala tu la Mheshimiwa *Attorney General* na Serikali kuliangalia hilli ili haya yasitokee. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Emmanuel Shangai.

MHE. EMMANUEL L. SHANGAI: Mheshimiwa Spika, kuhusiana na eneo la Pori Tengefu la Loliondo; najua pori hilo lilitangazwa pamoja na mapori mengine 49 mwaka 1974 kwa G/N 459, lakini ukijaribu kuangalia, baada ya kutangazwa mwaka 1974 Waziri alitakiwa kutangaza ndani ya miezi 12, lakini hayakufanyika hivyo.

Mheshimiwa Spika, eneo la pori tengefu tunaloliongelea watu wengine huku nje tunaona kama vile ni ardhi ambayo haina watu. Ardhi ile inakaliwa na wananchi zaidi ya 80,000, kuna vijiji zaidi ya 23, kuna kata nane. Sasa leo hii ukisema uchukue kilometra 1,500 wale wananchi hawana sehemu nyingine ya kwenda na wala hawana sehemu ya malisho kwa ajili ya mifugo yao na huku tukijua kwamba Wilaya yetu ya Ngorongoro asilimia 95 ni wafugaji, wanategemea mifugo.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya Mkuu wa Mkoa alikwenda Loliondo, amekwenda kutoa matamko ambayo yameleta taharuki ndani ya Wilaya ya Ngorongoro. Kwa sasa hivi wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro na niiombe Serikali kutafuta namna ya kutuliza hali ile ambayo inatumika na magazeti na baadhi ya watu ambao hawana nia na wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, niiombe tu Serikali, kama ina nia njema ya kutatua matatizo ya Wilaya ya Ngorongoro ni lazima ikae na wananchi meza moja na kutafuta njia ya kutatua changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeweka vizuri, kwamba tutafute namna bora ya kutatua matatizo yale. Kwa sababu wananchi wetu wanategemea kwamba Serikali yao itawasaidia, itawasililiza na kuwaletaa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe tu, hoja zilizo mbele yetu ni hoja zetu sisi Wabunge kwa Serikali. Kwa hiyo hoja za hawa Wenyeviti unapomaliza kuchangia, labda kama una jambo mahsus ambalo unataka tutoke nje ya hiso taarifa, lakini Mbunge ukichangia hizi ni taarifa zetu sisi kwa Serikali. Kwa hiyo ni muhimu sana kukumbuka kuunga mkono hoja za Kamati zetu.

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Hassan Selemani Mtenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Wycliffe

Makamba na Mheshimiwa Elibariki Emmanuel Kingu ajiandae.

MHE. HASSAN S. MTENGA: Mheshimiwa Spika, nami nitangulize kutoa shukrani za dhati kwako kwa kuchaguliwa kwa kura nydingi sana kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu kwa kazi nydingi anazozifanya. Niwapongeze na Mawaziri ambao wamepata uteuzi hivi karibuni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie suala la Hifadhi ya Ngorongoro. Hifadhi yetu ya Ngorongoro ilianza rasmi mwaka 1954. Hifadhi hii wakati inaanizishwa kulikuwa na takriban watu kama 8,000. Watu 8,000 kwa wakati huo walikuwa ni wachache sana, lakini leo tunapozungumza hapa Bungeni kuna watu takriban 110,000. Sasa ni nini nataka nizungumze. Kama tunakwenda kuwa na hifadhi ina watu zaidi ya 110,000, hatuwezi kuiita hifadhi kwa kweli, tusidanganyane kwenye Bunge hili. Lakini hii ni rasilimali ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia rekodi za mapato ya makusanyo ya fedha wenye Hifadhi yetu ya Ngorongoro; mwaka 2018 tulikusanya bilioni 143.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Simwoni anayeomba taarifa, ni nani!

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, niko hapa.

SPIKA: Nimekuona tayari, Mheshimiwa Jafari Chege.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, sina budi na wala sina namna ya kumwondoa mchangiaji kwenye hoja yake ya msingi, naaka tu nimpe taarifa kwamba nje ya watu zaidi ya 100,000 wanaopatikana pale tunachozungumza ni pamoja na aina ya shughuli zinazofanyika kwenye ile hifadhi ya Ngorongoro. Mojawapo ikiwa ni kwamba miaka hiyo

ambayo watu walikuwa ni zaidi ya 8,000 ng'ombe waliokuwa kwenye hifadhi walikadiriwa kuwa 12,000. Leo tunavyozungumza kuna ng'ombe zaidi ya laki moja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka nimpe taarifa ili aende akijua kwamba hayo yote yanafanyika kwenye Hifadhi ya Ngorongoro.

SPIKA: Sasa kabla sijakuuliza Mheshimiwa Mtenga uendelee na mchango wako, nilikuwa najizuia kidogo kusema kanuni zetu, maana nachukua muda wenu kidogo, nilikusudia kuwakumbusha baadaye. Kwa sababu usipomsikiliza Mbunge mwenzako kumaliza hoja yake, huenda hilo jambo, yaani unatakiwa umuingizie taarifa akiwa amemaliza kile anachokisema ili ujue kuwa kuna jambo amelisahau. kwa sababu pungufu ya hapo maana yake wewe unamuingizia taarifa yako, sasa haelewi kama mtiririko wake aendelee nao ama vipi.

Kwa hiyo tuwe wavumilivu kidogo. Leo taarifa zinaruhusiwa kabisa, wala msiwe na wasiwasi, lakini mwache yule mwenye hoja amalize ile hoja, anapokwenda kwenye hoja nytingine unagundua kwamba amesahau hii sasa ngoja nimuongeze, ndilo lengo hasa la hiyo kanuni yetu ya Taarifa.

Mheshimiwa Mtenga.

MHE. HASSAN S. MTENGA: Mheshimiwa Spika, kwanza niipokee taarifa, lakini nilikuwa nazungumzia mwaka 1820 mapato ya Ngorongoro yalikuwa bilioni 143. Tulipoingia 20...

SPIKA: Samahani, ulikusudia kusema 1820 au 2018.

MHE. HASSAN S. MTENGA: Mheshimiwa Spika, ni mwaka 2018, Mheshimiwa Chege alinitoa kidogo kwenye mstari.

Mheshimiwa Spika, tulipoingia mwaka 2019 tukakuta tuna fedha ambazo tulizikusanya bilioni 124, lakini 2020 tukakusanya fedha bilioni 31.

Mheshimiwa Spika, sasa naziweka hizi *record* ili tuone jinsi hifadhi yetu inavyokwenda kuteketea na masuala ya mifugo pamoja na kaya ambazo zipo kwenye hifadhi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwenye hifadhi hii kuna kaya zaidi ya 22, lakini leo tunapotaka kuzungumzia watalii wanaoingia Ngorongoro imekuwa ni hali ya hatari. Watalii wanapoingia Ngorongoro kwanza lazima wakutane na ng'ombe, mbuzi pamoja na kondoo ndipo waingie huko ndani.

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi kuna vitu vinafichwa kwenye Ngorongoro. Leo kuna watu wanauawa na simba, wanazikwa usiku, haya hayazungumzwi. Wanafika mahali kuwazika watu hawa usiku Serikali isije ikaelewa na ikatambua kwamba wananchi wao wanauawa mbugani.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe ushauri na ushauri wangu, pale tunapozungumza kwamba tunataka hifadhi iwepo lazima tufike mahali tukubaliane kwamba hifadhi hii iwepo. Kwa sababu kwa mujibu wa sheria, kama hawa watu walikuwa 8,000, leo wako 110,000, wametokea wapi zaidi ya 102,000? Kwa mkataba upi unaozungumzwa? Lazima vitu hivi tuviangalie.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe angalizo moja. Kwetu kule Mtwara kulikuwa na mradi wa gesi. Mradi ule wa gesi ukazua mambo mengi sana, lakini kwenye Bunge hili ikasemwa kwamba mradi ule ni wa kitaifa na Serikali ikachukua maamuzi na gesi ile ikatoka Mtwara ikaja Kinyerezi – Dar es Salaam na sasa ndiyo imekuwa sehemu ya msaada wa umeme wa gesi ya Mtwara. Hakuna sehemu tulipozungumza kwamba sasa katika hii rasilimali tugawane mbavu, hakuna. Hata hivyo, huku tunapoelekea kwenye suala la Ngorongoro, leo kuna wafugaji wako mle ndani, twendeni kwa wale wafugaji wakaombe mifugo waliyokuwa nayo halafu wataowaona watu walio nyuma ya mifugo ile.

Mheshimiwa Spika, wale waliopo ndani ya Ngorongoro si wenye mifugo yao; na hili lipo, si kwamba ni jambo ambalo tunalizungumza tu hapa. Sasa kama kuna

matajiri wako nje, wanafanya kazi wao kugeuka kuwa *NGOs* na *NGOs* sasa hivi ziko kule zinaelimisha watu jinsi ya kutohama.

Mheshimiwa Spika, kwa suala la Ngorongoro tufike mahali kama Bunge tuchukue hatua. Hali ya Ngorongoro ni mbaya. Naishauri Serikali, hizi kaya 22 twendeni tuwatafutie makazi au tuwalipe fidia, hawa watu tuwaondoe kwa utaratibu.

Mheshimiwa Spika, kuna kitu ambacho kipo ndani ya pazia; leo tunazungumza wenzetu wapo mle ndani, wanafuga; si wao tu, kuna wenzetu wa nchi Jirani wanafanya kila njia Ngorongoro ife na sisi tumejifungia humu Bungeni. Pia wako wenzetu wanatumika. Huko nje kuna matajiri, kwenye hoteli kuna matajiri kutoka Ngorongoro. Lazima tuelezane humu ndani. Wamekuja kufuata nini matajiri? Mbona hatujawaona Wamasai wamekuja na lubega wanasema mimi ndiye mwenye ng'ombe 200? Wanakuja matajiri hapa wanakaa Arusha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii inaumiza sana. Nimezungumza kwa uchungu kwa sababu Jimbo langu mimi la Mtwara MJini ni Jimbo ambalo ni masikini, na ndiyo maana leo ninazungumza kwa ukali sana. Hata tukiangalia kwenye bajeti, mimi nimetoa gesi kuileta huku, kwenye bajeti, tuiangalie Arusha, sisi tunapata sawa na Arusha? Arusha sawa na Mtwara? Si vitu viwili tofauti? Mtwara haiwezi kuingia Arusha hata kwa mara 200 wala kwa mara 100, haiwezi kuingia Arusha, lakini tunapoingia kwenye kutafuta rasilimali ya Taifa, keki tunagawana sawasawa. Kuna haja gani sasa ya wenzetu kuzuia hiyo keki wao wanataka kuihujumu hiyo keki? Hili halikubaliki kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pale kuna Baraza la Wafugaji. Baraza lile la Wafugaji ndicho chanzo chote mnachoona kwenye mgogoro huu tulikuwa nao. Ngorongoro wenyewe walikuwa wanawapa hela zaidi ya bilioni tatu kwa mwaka kuendesha shughuli zao. Zile bilioni tatu sasa ndizo zimegeuka

kuwa chungu kwa Serikali. Tunapigwa na fedha zile ambazo tulikuwa tunawapa Baraza la Wafugaji.

Mheshimiwa Spika, kanuni sizijui sana, lakini kuna maneno ningesema hapa, naogopa sana unaweza ukani fikuza kutoka nje, ila nikuombe, kama walipeleka Mtwara kule vifaru, ma-*bulldozer* pamoja na vitu vingine...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. HASSAN S. MTENGA: ...kwamba rasilimali ile ya taifa iwe keki ya Taifa, tunaogopa nini? Au kwa sababu kuna matajiri?

Mheshimiwa Spika, ni vyema sasa, kama waling'ata jongoo Mtwara wang'ate hao jongoo na sehemu nyingine. Tukiacha Ngorongoro kesho tutakwenda Mfinga Iringa, kesho kutwa watahamia Serengeti na mwaka ujao watakuja pale Mbeya; halafu tunakaa humu tunajifungia, tunaona ni vitu vya kawaida tu?

Mheshimiwa Spika, tufike mahali...

SPIKA: Dakika moja, malizia Mheshimiwa.

MHE. HASSAN S. MTENGA: Mheshimiwa Spika, ahsante nakushukuru sana. Zingekuwa mbili ningekushukuru zaidi. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna moja au nyingine mgogoro ule hauwezi kwisha kwa mazungumzo kama wanavyodai, kwa sababu wenzetu wanatoka wanakwenda kule wanashawishi watu, leo hii wameshajipanga, wanasema njia zote tu-*block*, tuanze Maandamano pamoja na vitu vingine.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Taarifa Mheshimiwa Spika.

MHE. HASSAN S. MTENGA: Sasa hawa ni wenzetu wanafanya vitu hivi. Huo mgogoro wanakwambia wewe uende ukazungumza, ukazungumze na nani? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ole-Sendeka naona amekaa kabla ya taarifa, kwa hiyo...

MHE. CHRISTOPHER O. SENDEKA: Mheshimiwa Spika nilitaka kumpa...

NAIBU SPIKA: Hataweza kuipokea sasa kwa mujibu wa kanuni zetu kwa sababu ilibidi awe anazungumza ili ndipo nimpe sasa nafasi ya kuipokea taarifa yako.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikae.

SPIKA: Haya, ahsante sana.

Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Elibariki Emmanuel Kingu na Mheshimiwa Muhamari Shabani Mkenge ajiandae.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hoja hizi mbili za Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba ni-*declare*kwamba mimi ni mdau mkubwa sana wa mazingira; lakini ukiacha hivyo, hapa Bungeni mimi ni mdau mkubwa sana wa meno ya tembo, ninayetetea tembo wasing'olewe meno.

Mheshimiwa Spika, nimeguswa sana na mjadala unaoendelea nchini juu ya hili suala la Ngorongoro. Labda nishauri kabla sijaendelea, ipo haja kubwa ya Wabunge kutembelea hifadhi zetu. Mimi ni mdau mkubwa sana. Ipo haja kubwa ya kuzitembelea ili tuone tunapokuwa tunazungumzia tunamaanisha nini? Najua hilo unaliweza, utupeleke tukazitembelee hizo hifadhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 1979 Hifadhi ya Serengeti na Hifadhi ya Ngorongoro zilipewa hadhi ya Urithi wa Dunia; siyo wa Tanzania, ni Urithi wa Dunia. Mwaka 2018 UNESCO illipa hadhi Ngorongoro kuwa ni moja kati ya Eneo la Utalii wa Miamba (*Global Geopark*), Aprili, 2018.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, hadhi hii haitolewi ovyo ovyo. Afrika hadhi hii ya *Geopark* iko kwenye nchi mbili tu; ipo kwenye nchi ya Tanzania na Morocco. Ni nchi mbili tu kwa Afrika. Yaani duniani ziko nchi tano tu zenye hadhi hii; zinaongezeka Brazil hapo na nchi nyingine. Kwa hiyo, ni nchi tano tu zina hadhi ya kuwa na utalii wa miamba, moja kati ya nchi hizo ni Tanzania kupitia *Ngorongoro Park*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tangu tumepewaa hadhi hiyo mwaka 2018, ndiyo ile aliyokuwa anasema kaka yangu pale, ndiyo kwa mara ya kwanza Tanzania tuliweza kuingiza mapato ya nchi shilingi bilioni 148 kwenda shilingi bilioni 150 baada ya kupewaa hadhi hiyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa kupanga ni kuchagua. Tanzania ni nchi kubwa sana, tuchague lile eneo liwe la makazi ya watu au liwe moja kati ya Urithi wa Dunia, Utalii wa Miamba na chanzo cha tatu cha mapato kwenye nchi hii? Kupanga ni kuchagua. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mimi nimekwenda Ngorongoro hivi karibuni. Nimefika pale, hilo eneo ambalo wanasesma ndugu zangu wanaishi Wamasai, hali ni mbaya. Wale watu pale wamesema ng'ombe ziko laki moja, siyo kweli, kuna mifugo zaidi ya laki nane iko mle ndani, lakini mifugo inayomilikiwa na wazawa wa pale, wale Wamasai ni asilimia tatu tu. Sasa swalii tuijulize, ile mifugo mingine inamilikiwa na nani? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mkitaka tuweze, Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa, toa tangazo kesho kwamba wale wananchi ng'ombe wanazomiliki zote ziwe za kwao, utaona anapigwa mwingine, analia mwingine. Utaona! Zile ng'ombe siyo zote ni za wale Wamasai. Vyombo vyaa dola si vipo! Au

kazi yake ni kutumwagia sisi maji ya washawasha! Si waende wakafanye *research* pale! Wamasai wale hawamiliki zile ng'ombe wala kondoo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye haya mambo ya uhifadhi, haya mambo kidogo ni ya kitaalam, kibaya kuliko vyote, wale ndugu zetu siku hizi hawafugi ng'ombe, wanafuga kondoo; na kazi ya kondoo ni moja, kwenye uharibifu wa mazingira kondoo ndiyo inaongoza. Yeye akila, hali majani, anang'oa lile jani lote na mizizi yake. Maaana yake ni kwamba lile eneo litaota mmea ambao siyo rafiki kwenye eneo lile. Tunaenda kuua ule uwanda, na kile kivutio cha Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, tena nimesahau, hii shilingi bilioni ninayosema 148 au shilingi bilioni 150 iliyozalishwa mwaka 2018, siyo ya Ngorongoro yote kwa ukubwa wake, ni kale *crater* tu, kale ka-Ngorongoro *Crater* ndiyo kamezallisha hela zote hizo. Sasa *imagine*, eneo lote lile zingefanyiwa uwekezaji, kwa sababu *crater* pale ziko zaidi ya maja; ziko tatu sijui, zote zingefanyiwa uwekezaji, zote zingefanyiwa uendelezaji, nchi hii ingekuwa na fedha kiasi gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine watu wanajificha huko kwenu, ni majizi wengine. Yaani wanajificha chini ya siasa kumbe ndio ananyonya Taifa hili halafu mwisho wa siku anasema nawatetea; hawatetei watu, anatetea mali zake ambazo zimetunzwa ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, taarifa

SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Olelekaita.

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naomba tu nimpe taarifa mzungumzaji kwamba ukurasa wa 37 wa Ripoti ya Kamati, inasema hivi na ninaomba ninukuu: "Serikali imekuwa ikitumia mfumo wa matumizi ya ardhi mseto (*multiple land use system*) katika Hifadhi ya Ngorongoro kwa mujibu wa sheria na umeiletea Tanzania sifa ya kuitwa hifadhi na sehemu ya Urithi wa Dunia.

Mheshimiwa Spika, nataka nimpe tu taarifa mzungumzaji, wakati Ngorongoro inapewa hiyo hadhi ya Urithi wa Dunia, wafugaji hao walikuwepo na maisha yalikuwa yanaendelea; na sheria inaruhusu.

Mheshimiwa Spika, nampa mzungumzaji taarifa hiyo. Ahsante sana. (*Makof!*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimetoa ufanuzi hapa wa matumizi ya ile kanuni ya kutoa taarifa na ndiyo maana hapa mbele huwa kuna nafasi zinatolewa za Mbunge kuchangia. Taarifa alioitoa sijaelewa ni eneo gani la Mheshimiwa Salome, labda ni sehemu ya kwanza aliyokuwa anatoa takwimu au ulikuwa unampa taarifa hiyo kwenye hoja ipi? Kwa sababu mimi nasikiliza ule mtiririko unavyokwenda, yaani hii taarifa uliyoitoa hapa ni kwenye mchango wake upi?

MHE. EDWARD O. KISAU: Mheshimiwa Spika, napenda tu ku-*clarify*. Alianza kwa kuelezea Ngorongoro kutambuliwa na *UNESCO* na kwamba imepewa hadhi ya Urithi wa Dunia. Kwa hiyo, nataka tu nimwambie kwamba Taarifa ya Kamati inasema hivyo na hao watu walikuwepo tu kipindi kile.

SPIKA: Sawa.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hujasimama Mheshimiwa Salome; Kanuni ya 77 ngoja nisimame ili tuelewane vizuri. Kanuni ya 77 ndiyo inayozungumza kuhusu taarifa. Ukitoa taarifa sehemu ambayo siyo unayotolea ufanuzi, unamfanya kwanza mchangiaji asielewe kama apokee taarifa yako ama asipokee. Ndiyo nasema lazima msikilize anapoingia kwenye hoja nyingine. Kwa sababu hapa alishaingia kwenye hoja nyingine ya kuashiria kwamba kuna watu wengine ambao mifugo yao ipo kule na sio wale wakazi wa pale. Kwa hiyo, nilitarajia taarifa inayokuja inataka kuzungumza ufanuzi kuhusu uwepo wa mifugo ya watu wengine, kwa sababu kwenye hoja ile kuhusu maelezo ya tangazo la *UNESCO*, tangazo la *World Heritage Site* alikuwa ameshamaliza akahamia kwenye hoja nyingine.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nawaomba sana, taarifa unatakiwa uitoe pale ili pia hata taarifa zetu Rasmi za Bunge, ziweke vizuri, yaani kwamba kuna Mbunge alisimama akafafanua vizuri ama akampa taarifa Mbunge kuhusu hoja hii. Sasa ikiwa mbali kule, hata sisi huku kwenye taarifa zetu, mtu anakuwa haelewi Mbunge aliyetoa taarifa, ilihusu nini? Kwa sababu kanuni ya 77 inavyoeleza kuhusu taarifa, ni kwamba aidha mtu amesahau jambo fulani au kama hajasahau, basi unataka kufafanua labda kuna jambo yeze hajaelewa.

Nadhani hapo tumeelewa ni wakati gani tutoe hizi taarifa; na kama nilivyosema, leo taarifa nimewaachia mtaendelea kutoa, lakini mzeitoe wakati ule unaopaswa ili nasi taarifa zetu Rasmi za Bunge zikae sawa sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Salome Makamba.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba niendelee na mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, nasisitiza, kupanga ni kuchagua, maamuzi yako mikononi mwetu. Sisi kule kwetu Shinyanga ni moja kati ya watu ambao tumeathirika sana na hili suala la kuhamishwa kupisha maeneo ya migodi. Kwanza wamesema vizuri ambao wanawatetea Wamasai waendelee kubaki ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro, kwamba watu hawa miaka ya 1950 walitolewa Serengeti wakaletwa Ngorongoro na walikuwa ni watu 8,000; kwa maana walioletwa ni 4,000 na wale waliokutwa pale 4,000 wakawa 8,000.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi watu wale watu wameshafika laki moja na kitu. Asilimia 64 ya watoto wa wakazi walioko pale hawajui kusoma na kuandika. Utaenda wapi katika nchi ya Tanzania ukute asilimia 64 ya *population* hawajui kusoma na kuandika? Ilikuwa wakati ule wa Mwalimu Nyerere. Wako pale, wanasema madarasa yapo. Wale watoto hawasomi, kazi yao ni kuchunga ng'ombe za

mabeberu ambao wamewapelekea kuchunga kwa ajili ya kuwasaidia kuwapa hela.

MHE. EMMANUEL L. SHANGAI: Taarifa ya Spika. Taarifa!

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, kesho na keshokutwa twende pale tukatembelee...

SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba kuna taarifa.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, ukisimama na gari la *tour*, watoto wanakuja kuomba kwenye gari. Ile picha iliyopo kwenye gazeti siyo ya uwongo.

SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba kuna taarifa kutoa kwa Mheshimiwa Emmanuel Shangai.

TAARIFA

MHE. EMMANUEL L. SHANGAI: Mheshimiwa Spika, nimemsikiliza Mheshimiwa Salome, anasema kwamba qatoto wengi waliopo Ngorongoro hawapo shulenii, wanachunga tu. Naomba nimtaarifu tu kwamba Tarafa ya Ngorongoro ina shule 30 na watoto wanasoma. Waliofaulu mwaka 2021 ambao Mheshimiwa Mama Samia amewapeleka shule ni zaidi ya watoto 1,000 wako Sekondari.

SPIKA: Sawa. Sasa ngoja...

MHE. EMMANUEL L. SHANGAI: Mheshimiwa Spika, kama anasema kwamba watu asilima 64 hawajui kusoma na kuandika, hiyo ilikuwa ni taarifa ya *NBS* ya 2017 iliyopikwa ambayo ilisema Kata ya Olbalbal wananchi asilima 47 wanategemea...

SPIKA: Mheshimiwa ngoja tuongozane vizuri ili taarifa yako ikae vizuri. Yeye kasema asilimia 64, nawe unakubali kwamba ni kweli isipokuwa ilipikwa. Sasa nitakusamehe kwa sababu ndiyo umekuja, lakini kanuni za humu ndani maana yake unachokisema ni kwamba Mheshimiwa Salome

Makamba anasema uwongo; na kanuni zinazozungumza kuhusu Mbunge kusema uwongo ni kanuni nyingine, haiusiki hii ya taarifa. Ukishamtuhumu Mbunge kusema uwongo, tunaanza kufuata utaratibu wa wewe kuleta takwimu nyingine.

Kwa hiyo, ili nikuongoze vizuri utoe taarifa yako vizuri, kama siyo zile 64 wewe unazozijua, ni ngapi? Yaani ndiyo unaweza kusimama kwa kifungu hicho cha taarifa nilichoelezea. Yaani wewe unasmama unasema siyo 64 ila ni hizi.

Kwa mfano, sasa hivi hapa umesema watoto 1,000 wamefaulu. Swali litakuja, watoto 1,000 kati ya wangapi? Kwa sababu ndiyo utoaji wa taarifa. Yaani hapa ukisema 1,000 ukaniambia mimi ni asilimia 100, hilo linakuwa limeisha, kwamba watoto wamefaulu na wako shulen kwa asilimia 100. La sivyo, tunaanza kuulizana sasa maswali ya kitakwimu hapa halafu tunawenza kuwa hatuna. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nadhani tunaelewana vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Shangai, ulikuwa umemaliza? Nilikuwa nakuongoza ili taarifa yako itoke vizuri.

*(Hapa Mhe. Emmanuel L. Shangai aliinama kuashiria
kukubali kwamba alimaliza kutoa taarifa yake)*

SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kutuongoza vizuri. Kwanza Mbunge aliyekaa anasema anazidi kudhihirisha tu kwamba *population* ni kubwa. Yaani watu walioko pale ni wengi kuliko wale 8,000 waliotegemewa, walitungiwa hiyo sheria anayosema Mheshimiwa Olelekaita. Sheria ilitungwa kwamba wakae 8,000 kwa sababu *it was manageable*, lakini sasa hivi hali ni mbaya. Kwa mujibu wa NBS, asilimia 50 ya wakazi wa Ngorongoro ni masikini. Sasa hao unaosema asilimia 50 ni

masikini halafu kuna mifugo laki nane, wanakuwaje masikini na watu wana ng'ombe laki nane? Yaani ukiangalia tu hizi *data* unaona kabisa hapa kuna watu wachache wamepeleka mifugo yao ndani ya hifadhi ambao wanatetea maslahi yao binafsi, wameachana na maslahi ya Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ndani ya eneo la Ngorongoro ni *very potential* na kuna nchi jirani ambayo pia kuna vita ya kibiasara kwenye utalii. Juzi nimemwambia Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, ziko *NGOs* ambazo zimesajiliwa, ziko ndani ya nchi hii zinafadhiliwa na nchi Jirani; *headquarter* ni nchi Jirani. Ukienda kwenye *NGO*, wote wanaongea lafudhi ya nchi jirani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Ngorongoro ni yetu sote. Serikali ije na mkakati siyo kuwapiga watu mabomu, siyo kuwashamisha watu kwa nguvu. Hawa watu waandaliwe, wajengewe nyumba, wajengewe shule, Kituo cha Afya, wajengewe miundombinu ya kutosha, wahamishiwe pale na wenyewe waishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, amesema vizuri ndugu yangu kwamba ndiyo maana hujaona Masai aliyeavaa lubega amekuja hapa kuandamana kwamba hawataki kuhama. Nami nimeenda kwenye hifadhi, wale watu wapo ambao wameomba kwa barua, wameandika wanaomba kuhamishwa kwenye Hifadhi ya Ngorongoro. Wapo! Hata kesho Serikali itangaze, anayetaka kuhama Ngorongoro, uone kama watu hawajajitokeza! Wale watu wanaishi kwenye umasikini wa kutupwa. Watoto wao hawasomi, hao matajiri wenye ng'ombe na kondoo, ziko biashara.

Mheshimiwa Spika, pale Hifadhi ya Ngorongoro imeripotiwa; ukienda kusoma ripoti ya Ngorongoro, mwaka 2021 peke yake tembo zaidi ya 20 wameuawa na faru mmoja. Chanzo cha kifo cha tembo wale na faru ni sumu. Wanawekewa sumu na wakazi wa pale; au wanawekewa sumu na watu ambao ni adui wa tembo na adui na faru. Tunahitaji tuambiwe na nani ili tujue kwamba Hifadhi ya

Ngorongoro ni urithi wetu? Tunahitaji tuambiwe na nani ili tujue kwamba Hifadhi ya Ngorongoro ni utajiri wa dunia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakubali, inaweza kuwa yapo maslahi, lakini maslahi ya Taifa yanakuja kwanza. Hakuna mtu ambaye hapendi kuishi vizuri, hakuna! Pia hakuna mtu anayeweza kukubali kuona anazaa watoto hawajui kusoma, hawajui kuandika na mwisho wa siku anaishi kwenye umasikini. Kuna nyumba gani pale Ngorongoro? Nyumba wanazokaa, kwanza sheria haitaki waezeke zile nyumba kwa bati. Kwa hiyo, wanakaa kwenye nyumba ambazo zimewezekwa kwa manyasi. Leo Mbunge anasimama ndani ya Bunge hili anatetea watu wakakae kwenye nyumba za nyasi, mbona yeye hakai kwenye nyumba za manyasi? Kwa sababu Sheria ya Ngorongoro haikubali kujenga nyumba ya bati, yenye mbona anakaa kwenye nyumba nzuri ambayo imeezekwa vizuri! (*Makofi*)

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Salome kwa sababu nilikusudia kukuongeza dakika moja ya kuchangia, Mheshimiwa Ole-Sendeka.

TAARIFA

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKE: Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa dada yangu mpendwa Mheshimiwa Salome. Ngorongoro katika Wilaya zote za wafugaji ndiyo inayoongoza kwakuwa na wasomi wengi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; ni Ngorongoro ndiyo iliyomtoa Jaji wa Kwanza Mmasai ambaye ameteuliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Juzi; ni Ngorongoro ndiyo ina *Ph.D. holders* wengi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania... (*Kicheko/Makofi*)

MBUNGE FULANI: Ng'ombe wa nani? Ng'ombe wa nani? Ng'ombe wa nani? (*Kicheko*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ole-Sendeka. Mheshimiwa Salome Makamba.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, hii ni sehemu ya mkakati. Wanachokifanya sasa, wale watoto wakibahatika wakapenyapenya wanaambiwa mkasome sheria ili wakija kule ndani watetee wasitoke kule ndani. Ni sehemu ya mkakati, yaani hii ni sehemu ya mkakati. Waangalie Wamasai wengi waliotoka kule kwanza wana ufadhili, lazima wapate ufadhili wa kwenda Chuo Kikuu. Anayemfadhilli nani? Mimi sijapata mfadhilli, natoka Shinyanga. Akipata mfadhilli, *condition* namba mbili ni lazima akasome sheria ili kusudi aje akapambane nao. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, najua Serikali ina vyombo. Hii ni sehemu ya mkakati. Naomba Serikali ije na mpango wa kuwahamisha wananchi wanaoishi maisha ya kimasikini ya wanaoishi ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro na mpango huo ujumuushe hawa watu kujengewa nyumba nzuri, wapewe ardhi nzuri ya ufugaji na pia wawekewe miundombinu mizuri ya kutosha ambayo itawafanya waishi kwa raha.

Mheshimiwa Spika, juu ya yote, Serikali itangaze, wale Wamasai zile ng'ombe kuanzia leo ziwe zao. Hilo ndiyo litakuwa mwisho wa matatizo. Ng'ombe, kondoo, mbuzi, ziwe za wale Wamasai wa mle hifadhini. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Immanuel Elibariki Kingu, atafuatiwa na Mheshimiwa Muhamari Shabani Mkenge na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah ajiandae.

MHE. ELIBARKI I. KINGU: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nami niungane na Wabunge wenzangu kukupongeza wewe binafsi kwa nafasi ambayo Wabunge tumekuchagua kwa kishindo. Hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Taifa hili la Tanzania bado nina imani kwa dhati ya moyo wangu kwamba mambo mema

na ya msingi ambayo Taifa letu yameyarithi toka kuanzia zama za Waasisi wa Taifa letu, *it is my trust* kwamba kizazi hiki cha leo kiklamua kwa dhati na kwa dhamira ya kuangalia maslahi ya nchi mbele na maslahi ya vizazi vinyayokuja, tuna uwezo kabisa wa kulilinda Taifa hili tukafanya maamuzi Taifa hili likabaki moja, Taifa hili likabaki kuwa la mshikamano, Taifa hili likaendelea kuwa la upendo na likadumisha tunu za umoja na mshikamano ambazo ndizo zimekuwa asili ya Taifa hili ambalo limekuwa likipigiwa chepuo kwa mifano duniani bila kuleta migogoro. Tumekuwa na sifa hiyo ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Watanzania tumekuwa na sifa ya kutatua matatizo yetu wenyewe na kuliacha Taifa likiwa moja na likiwa na mshikamano. Naomba niseme maneno mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, *demographic projection* ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa miaka 35 inayokuja, naiona Ngorongoro ya miaka 35 inayokuja ikiwa na *population* ya zaidi ya watu 800,000 mpaka 900,000. Naiona Ngorongoro ya miaka 40 inayokuja ikiwa na viwanda ndani ya hifadhi, naiona Ngorongoro inayokuja ikiwa na mitambo ya mashine kwa ajili ya *ku-cater for population* ambayo itakuwa pale.

Mheshimiwa Spika na ndugu zangu Wabunge, naomba nzungumze haya kwa dhati ya moyo wangu, nikitanguliza maslahi ya Taifa langu mbele na kuweka ubinafsí wangu nyuma. Nataka niwaambie Watanzania, na naomba Bunge linisikilize kwa makini. Haya mambo tunayozungumza habari ya *heritage* ya dunia kwa Ngorongoro hatuzungumzii tu *heritage* ya dunia kwa sababu inaleta *revenue* zinazolisaidia Taifa letu, lakini tunazungumzia misingi ya historia ambayo Taifa hili Mungu amelipatia tuvirithishe vizazi vyá wajukuu zetu na wajukuu wa wajukuu zetu kwa *nature* ya utajiri ambaó Mungu amelipatia Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nayasema hayo kwa sababu na nitakuwa mtu wa hovyo sana kama nitatanguliza mambo ya ukabila kuzungumza sijui Umasai, kwangu mimi hoja siyo

Mmasai aliyeo Ngorongoro, kwa sababu wale ni Watanzania, raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hoja ninayoizungumza; je, Taifa hili la kizazi cha sasa hivi tuko tayari kuona *heritage* ambayo Mungu ametupatia kama nchi ikipotea bila kufanya maamuzi? Hiyo ndiyo hoja ya msingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tukienda kwenye hoja hiyo ya msingi wote kwa pamoja tatarudi kama Taifa, tutatengeneza *resolutions* za kwenda ku-*approach* lile eneo. Nataka nikuhamkishaie jambo hili litamalizika kwa amani na utulivu na maslahi ya Taifa hili yatakuwa yamelindwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu, nataka niwaambie kitu kimoja; ukiachilia mbali habari ya mifugo tunayoizungumza, lakini kuna taarifa ambazo kama siku moja ukiniruhusu nitazileta mezani kwako kama ushahidi. Kuna taarifa ambazo zinaonesha, sitaji kwa jina, mataifa ya jirani kuna hujuma kubwa inafanyika katika Hifadhi ya Ngorongoro. Kuna idadi ya wanyama wengi wanaletwa na mataifa jirani na lengo lake ni vita vya kitalii kupambana kati ya Mataifa ya *East Africa*. Sisi kizazi cha leo *we are not ready* kuona Ngorongoro inatufia katika mikono yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa uchungu mkubwa kwa sababu haya yanayofanyika kule ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro ukiachilia mbali *modernization* ya *housing* ambayo inaendelea kule ndani, lakini ninachotaka kusema ni kwamba *population* ya watu kutoka mwaka 1959, watu 8,000 na kwa kweli huwezi kuzuia watu walikuwepo mle kwa mujibu wa sheria, lakini tuijilize swalii; sheria ile iliundwa wakati ule ilikuwa imelenga nini kwa wakati ule? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama sheria tulikuwa tumeiunda sisi wakati ule Bunge hili ndicho chombo peke yake cha Kitaifa chenye mamlaka ya Kikatiba ya kubadili sheria na kutunga sheria zinazolinda maslahi ya nchi na kulinda maslahi ya vizazi vinavyokuja katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali na nataka niliseme hili kwa dhati kabisa kwa Serikali; mzigo huu tuisiutupe kwa ile jamiil ya watu walioko pale Ngorongoro peke yao. Serikali kwa upande mwininge kuna mahali ilikosea, kwa sababu haiwezekani nyumba za ghorofa zinajengwa Ngorongoro inaangalia, *modern houses* zinajengwa inaangalia, watu walitakiwa kuchukua hatua mapema. Hivi ninavyozungumza naona kabisa yaani kama vile maamuzi haya tulikuwa tuyafanye jana na siyo leo kwa maslahi ya kulinda ile Hifadhi ya Ngorongoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ya chama changu chini ya Rais wetu shupavu, mama Samia Suluhu Hassan, juzi Rais amefanya *royal tour* tumeona *impact* ya ongezeko kubwa la watalii katika Taifa letu. Tumeona *impact* kubwa ya ongezeko la mapato katika Taifa kutokana na *royal tour*. Ombi langu, Serikali ifanye *engagement* ya Kimungu kwa hawa watu walioko katika hifadhi. Imani yangu ni kwamba *engagement* ya kuzungumza na wafugaji hawa ikifanyika kwa ustaarabu Watanzania ni Taifa la watu wasikivu, tutamaliza mgogoro ule bila kuleta vurugu ambazo dunia inaweza ikatucheka kesho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa yale yanayoendelea katika Hifadhi ya Ngorongoro nitakuwa Mbunge ambaye nimeweka rekodi mbaya kwa Taifa langu nikisema Serikali msichukue hatua ya kulinda ile hifadhi. Hatua hii ya kulinda hifadhi inatakiwa ifanyike haraka na kwa maslahi mapana ya Taifa, lakini wakati huohuo tulinde mambo yote yanayohusiana na *humanity* kuhakikisha kwamba watu hawa wanatafutiwa mahali ambapo watakuwa *comfortable* na shughuli zao za ufugaji, watakuwa *comfortable* na shughuli zao nyingine za kiuchumi. Lengo ni kuhakikisha kwamba Taifa hili linabaki kuwa moja.

Mheshimiwa Spika, hizo *statistics* alizokuwa nazisema Mheshimiwa Salome Makamba, mimi nimekwenda mbali, hizo *statistics* nina orodha kama utaniruhusu naweza siku moja nikakuletea kwenye meza, ya baadhi ya watu ambaa ni wafanyabiashara wa mifugo, wamewatumia watu ndani ya

hifadhi na kuweka mifugo ndani ya hifadhi na ndiyo hao wamekuwa wakipaza sauti kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wewe jiulize kama *statistics* za Serikali zinaonesha ufukara ni asilimia 50, inakuwaje watu wawe na mifugo zaidi ya 800,000 au 900,000 wasemekane ni maskini? Hayo ni maswali ya kujuliza kama nchi.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu wetu yuko hapa.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Dakika niliyokuungeza inakaribia kwisha.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa unyenyekevu mkubwa...

SPIKA: Ngoja kwanza, nilikuwa nasema...

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: ...naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Haya. Mheshimiwa Cecilia Paresto, naona Mheshimiwa Kingu alikuwa hataki taarifa yoyote, kwa hiyo akamaliza kijanja, pamoja na kwamba alitaka kuongezewa muda.

Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah na Mheshimiwa Asya Mwadinii Mohammed ajiandae.

MHE. MUHARAMI S. MKENGE: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutumia nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja iliyo mbele yet una nitajikita zaidi kwenye upande wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kutumia nafasi hii, kwa niaba ya wananchi wa Bagamoyo, kukupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Spika wetu wa Bunge

la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia napenda kumpongeza Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, ambaye anatarajiwa kuwa Naibu Spika saa chache zijazo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda kwanza nizungumze kuhusu suala la mahusiano yetu ya Tanzania na nchi za nje. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa kuikuza diplomasia ya Tanzania nje ya mipaka yetu. Mama Samia anafanya kazi kubwa sana. Kwa kipindi kifupi toka ameingia madarakani amefungua milango mingi ya mahusiano ya kimataifa katika nchi yetu; tunampongeza sana kwa hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kama unavyotambua katika Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuna vyombo vingi ambavyo vinahusiana na Kamati hii, lakini nizungumze moja kuhusu suala la *NIDA*. Wananchi wa Tanzania kwa miaka mingi sana walikuwa wakisumbuka katika kupata vitambulisho vyao vya Taifa, lakini leo hii tunakoelekea baada ya Mheshimiwa Rais, mama Samia Suluhu Hassan kuchagua viongozi wapya katika taasisi hii mwelekeo wa upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa unaelekea kuwa mzuri katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, siku zilizopita Serikali ilikuwa ikisumbuka sana na suala hili. Mashine zililetwa, mitambo ililetwa lakini kwa bahati mbaya kazi iliyokuwa ikifanyika haikuridhisha Watanzania wengi; idadi kubwa ya watu wamesajiliwa lakini hawajapata vitambulisho vya Taifa. Leo hii Kamati imejiridhisha kwamba kazi inayokwenda kufanyika kwa ajili ya upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa ni kazi ambayo itakuwa yenye kutukuka. Tunawapongeza sana viongozi wa *NIDA* kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea nayo mpaka sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia hapa ni suala la mtangamano wa Jumuiya ya

Afrika Mashariki pamoja na Jumuiya ya *SADC*. Jumuiya hizi zimekuwa na faida kubwa kwetu sisi Watanzania na hasa baada ya Rais wetu, mama Samia Suluhu Hassan, kufanya ziara katika baadhi ya Nchi za Afrika Mashariki na kugundua fursa mbalimbali ambazo tunafaidika nazo hii leo kutokana na uwepo wa jumuiya hii.

Mheshimiwa Spika, katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ni mambo mengi sana ambayo yanafanyika na hasa fursa zilizopo za kibashara. Ni wajibu wa Serikali sasa hivi kuhakikisha kwamba fursa zilizopo za kibashara wanaziweka wazi ili wananchi waweze kuzitambua na kuweza kukimbizana nazo ili waweze kuiletea nchi yetu maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa Tanzania tuna matajiri wengi, tuna wafanyakibashara wengi, lakini bado mpaka leo hawajapata taarifa rasmi za fursa zilizopo. Kwa hiyo ni jukumu sasa hivi la Wizara zinazohusika pamoja na Serikali kuzitangaza fursa hizi ili wafanyakibashara wetu waweze kuziendea na kuhakikisha kwamba Taifa letu linapata mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, katika mtangamano wa *SADC* faida nyingi zinapatikana. Niipongeze Bohari yetu Kuu ya Dawa (*MSD*) kwa kupata tenda ya kuweza ku-supply dawa katika Nchi za *SADC*. Hii ni hatua kubwa sana ambayo Tanzania imeifikia. Tuna nchi nyingi za *SADC* lakini Tanzania imeteuliwa *MSD* kusambaza dawa pamoja na vifaatiba katika nchi hizo; hiyo ni hatua kubwa sana ya kimaendeleo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa napenda nipongeze Jeshi letu, Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Pamoja na kulinda mipaka, Jeshi lina shughuli nyingi ambazo wanazifanya ili kuiletea maendeleo nchi yetu. Ukiachilia mbali ulindaji wa mipaka, Jeshi linashughulika na shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze kwa kuendesha Kiwanda cha Nyumbu ambacho kinaendesha teknolojia ya

kutengeneza magari. Nafikiri kwa siku zijazo Tanzania itakuwa ni nchi moja wapo ambayo itakuwa inashughulika na mambo mengi sana ya kujitegemea na hasa katika uundwaji wa magari.

Mheshimiwa Spika, pia niwapongeze sana Jeshi letu katika suala zima la kilimo na hasa JKT, wanajihuisha sana katika kilimo na hiki kilimo kwa siku zijazo wataisaidia sana nchi yetu katika usalama wa chakula; niwapongeze sana kwa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH: Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* kwa kutujalia uzima, salama na afya njema.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru pia wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika ripoti hizi mbili muhimu za Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na ile ya wenzetu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kuwapongeza wenzetu wa Maliasili, Waziri, pamoja na Ardhi, Mawaziri pamoja na timu zao. Kwa kweli wamefanya kazi nzuri katika kipindi hiki cha utekelezaji wa kipindi cha miezi sita na tunaona matokeo chanya katika sekta zetu zote hizi za ardhi pamoja na maliasili.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni ombi langu kwa Wizara ya Fedha; sekta hizi tumezipelekea fedha kidogo. Maliasili kidogo wao wana afadhali, lakini sekta ya ardhi bado hali haijaridhisha, kwa hiyo tunaweza tukawalaumu utekelezaji siyo mzuri, lakini sababu kubwa ni kwamba kiwango cha fedha ambazo tunawapelekea hawa wenzetu hakiwezi kukidhi utekelezaji wa shughuli ambazo tumewapangia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo namwomba sana Waziri wa Fedha ajitahidi kwa sababu tuna malengo tumeyapanga katika llani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, tuweze kuyafikia katika miaka mitano na nyota njema huonekana asubuhi. Mpaka hivi sasa bado haionekani kwamba kuna uwezekano mzuri wa kuweza kuyafikia haya kama hatutaweza kuzipatia hizi sekta fedha za kutosha.

Mheshimiwa Spika, nami niungane na wenzangu na napenda kumfuata kaka yangu, ndugu yangu, Mheshimiwa Omar King. Kuna maneno ya maandishi yanazungumza "*idha dhwaharal-bidaa washarus-swahaba famankanalahul-ilma falyudh-har. Wamankudhwiat alayhi laanatu-llah*" kwamba unapodhihiri ujisadi au uzushi na kubughudhiwa au kutukanwa kwa wanazuoni, basi wale ambao wana utaaliam wanatakiwa waudhahirishe na watakaoficha basi laana ya Mwenyezi Mungu inatakiwa iwaandame. Sasa mimi binafsi sitaki laana ya Mwenyezi Mungu ije iniandame kwa sababu tayari nina ujuzi katika haya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo suala la Ngorongoro nafikiria tatizo kubwa kwamba tumewaacha wataalam wetu na sasa tunaongozwa na vichwa vyetu. Kwa sababu wataalam toka mwaka 1959 wamefanya tafiti za kutosha za kutupa dira ya kufanya maamuzi sahihi viyi tutalifikia hili suala, lakini matokeo yake vitabu tumeviweka pemberi na tunaongozwa na hisia na vichwa vyetu. Kwa hiyo kama walivyozungumza wenzangu kwa kweli tunakwenda kuipoteza Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kama hatutachukua hatua sahihi hivi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika masuala ya uhifadhi, suala la muda ni suala muhimu sana. kama muda ukiuacha, nakumbuka kuna Profesa mmoja, Profesa Kajembe, alifanya utafiti kule Duru-Haitemba katika kuwashirikisha wanajamii katika kuhifadhi msitu. Wananchi wale walikabidhiwa msitu katika kipindi cha mwaka mmoja walienda msitu ukawa umepotea wote umekwisha. Nafikiri wale ambao ni wenyeji wa Duru-Haitemba wanansikia hapa watakuwa wanafahamu kule Babati ukweli jinsi ulivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo na sisi katika hali halisi ya Mamlaka ya Ngorongoro kama hatutachukua hatua hivi sasa basi tujia ndae Tanzania kwenda kupoteza urithi wa dunia. Kwa sababu kila sababu zinaonekana kama tulikuwa watu 8,000 sasa hivi tupo zaidi ya 120,000; tulikuwa na ng'ombe 12,000, sasa hivi kuna ng'ombe zaidi ya 800,000. Hapa *projection* ya ndani ya miaka 20 hadi 40 inayokuja unaitegemee itakuwaje; tutakuwa na ng'ombe zaidi ya bilioni moja na kuendelea, tutakuwa na watu zaidi ya 300,000 hadi 500,000. Kwa hiyo naomba tu, muda wa maamuzi ni sasa, lazima tuchukue hatua.

Mheshimiwa Spika, katika uhifadhi huuhuu ambao tunauzungumza ndani ya Ngorongoro tulikwenda tukapoteza faru mpaka wakabakia faru watano. Jitihada zimefanyika sasa hivi tumeweza kurejesha faru angalau idadi inatia matumaini.

Mheshimiwa Spika, sambamba na suala la Mamlaka ya Ngorongoro, kuna hali ambayo inafanana na hiyo ya Bonde la Kilombero. Bonde la Kilombero nako hali siyo salama kwa sababu tumeshaweka fedha, trilloni sita pale na hizi fedha kama hatukwenda kulishughulikia Bonde la Kilombero nako hatari inatunyemelea.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu maji ambayo yanatoka katika Mto Kilombero ni asilimia 60 mpaka 65. Kuna vijiji kama Kijiji cha Ngombo; kuna vitongoji karibu vinane katika Wilaya ya Malinyi; kuna vitongoji vitatu katika Wilaya ya Ulanga na kuna kitongoji kimoja katika Wilaya ya Kilombero kutohaka na *data* za wataalam wetu vinatakiwa viondoke. Kama tukichelewa kuviondosha hivi, basi tusitegemee Mradi wa *Stiegler's Gorge* wala tusitegemee Mradi wa *SGR* kwa sababu hii miradi miwili inategemeana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nimalizie tu kwa kuwapa pongezi wenzetu wa maliasili hasa *TAWIRI* kwa kuweza kufanya ile *International Conference* ambayo ilikuwa ikifana vizuri na ninampongeza sana Mkurugenzi wa *TAWIRI* na Mkurugenzi wa Wanyamaporu pamoja na Waziri. Namwombwa

Profesa Mkenda tuwahamasishe vijana wetu wa Vyuo Vikuu, basi waweze kuhudhuria katika makongamano hayo kwa sababu yana tija kubwa na yataweza kuwasaidia Watanzania kuweza kukuza vipaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Asya Mwadini Mohammed, atafuatiwa na Mheshimiwa Agnes Mathew Mara na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde ajiandae.

MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi nami niweze kuchangia michango ya Kamati kutokana na taarifa ambayo imewasilishwa hapa Mezani.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la Ngorongoro mimi itabidi niliruke, naona wadau wenzangu wamelichangia vizuri vya kutosha. Sasa ni kazi kwa Serikali kulichukulia hatua na kwenda kulifanyia kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze zaidi katika sekta ya utalii na hapa nitazungumzia kuhusiana na Serikali yetu kujikita na utalii wa aina moja, nao ni utalii wa wanyamapori. Tunaona utalii wa wanyamapori unatuletea mapato mengi ndani ya Taifa letu, lakini kwa nini tunajisahau kuwekeza zaidi katika sekta nyingine? Maana yake kuna utalii wa masuala ya bahari ambapo nakumbuka kwenye Bunge la Bajeti nilisimama hapa na nikachangia vizuri sana. Tuna utalii wa malikale ambapo leo malikale zetu ukizitembelea kwa kweli ni masikitiko makubwa sana kama Taifa. Ninaumia kama mdau wa Taifa hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ni ushauri; ukipitia ripoti ya CAG, ameshauri kwamba sasa kama Taifa tuna haja ya kwenda mbele kujiwekeza zaidi katika sekta ya utalii na tuachane na sekta ya wanyamapori, twende na sekta nyingine. Kwa sababu tunategemea sekta hii ya wanyamapori peke yake, leo ikitokea janga la Taifa, Mungu aliepushe, wanyama wamepata magonjwa ama wamepoteza maisha, maana

yake hatuna utalii Tanzania. Kwa hiyo, kuna haja kama Serikali kujivekeza zaidi katika sekta nyingine. Tuna utalii wa kiutamaduni, utalii wa masuala mazima ya bahari, lakini kuna utalii wa wafuga nyuki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hizi sekta za utalii wa utamaduni pamoja na wafuga nyuki nimekuwa *interested* nazo sana kwa sababu ni sekta pekee ambazo wanaweza kupewa akina mama na wakaziendesha vizuri. Kwanza wataisaidia Serikali kupata mapato na akina mama hawa watatengeneza fedha kujitia sekta hizi. Utamaduni ni muhimu sana. Sasa hivi katika Taifa letu watu wanaiga sana utamaduni wa nje, itafika kipindi hapa wajukuu zetu watasahau asili ya Mtanzania. Sasa tukiwekeza zaidi katika sekta ya utamaduni tunaweza kulisaidia Taifa hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia nishauri, kama haitoshi, Serikali kama inaona ni mzigo mkubwa kutumia nguvu katika sekta nyingine, kuna haja pia ya kuita ama kuwapa nafasi wawekezaji aidha wa ndani, ama wa nje, kwa ajili ya kuendeleza utalii wetu katika nafasi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie sera. Kamati yangu pendwa ya Ardhi na Maliasili imeshauri hapa na ikawaambia kwamba kama Taifa linahitaji kupeleka mbele utalii wetu, kuna haja sasa ya kubadilisha sera zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukiipitia Sera ya Utalii ya mwaka 1999, hebu tuangalie kuna *gap* ya miaka mingapi mpaka kufikia 2022 leo tunapouzungumza utamaduni wa 1999 na 2022? Hapo tunaweza kupata picha kwamba bado tuna safari ndefu. Kwanza tubadilishe sera zetu. Hata hivyo nishauri katika kubadilisha sera; tusikimbilie kama Wizara tu na *department* ya utalii wakajifungia peke yao kuanza kuzichambua sera. Ni lazima wajaribu kuwaalika wadau wengine wa Wizara nyingine. Kwa sababu sekta ya utalii ni sekta mtambuka, ukizungumza; uvuvi inaikuta ndani ya sekta ya utalii, ukizungumza mazingira utakuta ndani ya utalii, ukizungumza maji, unakuta ndani ya utalii na Wizara nyingi kama ardhi na kadhalika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba Wizara ya Utalii ikae sambamba na Wizara nydingine wakati wanatengeneza hii sera, iwe ya utalii ama ya nyuki kwa maslahi mapana ya Taifa ili tupunguze zile *contradiction* zinavyokuja hapa. Maana yake wakati mwengine unakuwa na swali hujui ulipeleke kwenye Wizara ipi? Kwa hiyo, Mawaziri wakikubaliana kwamba hiki ni kitu cha utalii, lakini kinamhusu wa maji au wa kilimo, au mfugaji, ama mazingira, watakubaliana kwa pamoja ili tuweze kwenda mbele kama Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niendelee kujikita zaidi kwenye suala zima la masoko na utalii. Sekta yetu ya utalii bado hairidhishi ama haturidhiki na masoko ambayo yanafanywa ndani ya sekta hii. Kamati imeshauri, nami pia nashauri zaidi waweze kijiwekeza zaidi katika matangazo. Kwa sababu kuna msemo unasema, "*biashara itakangazwayo ndiyo itokayo.*" Kwa hiyo, wajijekeze zaidi kwenye matangazo kwa njia mbalimbali ili tuweze kuisaidia sekta hii iweze kukua zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, sekta hii ya utalii kuna TV wanaita *Safari Channel*. Ukiifungua hii TV *sometime in-bore*, kwa sababu ukifungua tu unakutana na wanyamapori tu. Yaani dakika kumi, ishirini wanyamapori; baada ya dakika kumi, ishirini, wanyamapori. Kwa hiyo, mtu ataangalia wanyamapori, kesho akifungua akikuta tena wanyamapori, hawezи kufungua tena hiyo TV. Ataangalia vitu vingine. Kwa hiyo, tunatakiwa tubadilishe zile ladha ili tuweze kulisaidia Taifa na kutangaza vyema utalii wetu na vivutio vyetu kwa maslahi mapata ya Taifa hilli ili tuweze kupata mapato ya Serikali kuweza kupiga hatua. (*Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, nizungumze kidogo katika suala zima la...

SPIKA: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ajiandae.

MHE. AGNES M. MARWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuongea siku ya leo. Kwanza nikupongeze wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia nimpongeze sana kaka yangu Mheshimiwa Zungu kwa kuchaguliwa na Chama chetu; Chama cha Mapinduzi, kuwa mwakilishi wa Chama cha Mapinduzi kwa nafasi ya Unaibu Spika. Naamini kabisa, kama kawaida, hiyo imekwisha hiyo, yeeye ndiye Mungu amemeoneshea njia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nianze moja kwa moja na kuchangia katika Wizara yangu ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Mimi niseme tu namshukuru sana Mheshimiwa wetu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu kipenzi sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wake wa kutukubalia sisi wanakamati kwa kurasimisha ardhi kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa wale wanaouliza Mheshimiwa Rais, Mama Samia kafanya nini; wanapaswa kujuia kwamba kati ya shughuli au kazi nzuri au upendo mkubwa aliotuonesha Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan ni huu wa kumtaka kila Mtanzania amilliki ardhi yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nampongeza sana mama, Mwenyezi Mungu aendelee kukubariki, unaupiga mwingi. Wale waliokuwa wanafikiri huwezi, unaweza, unatosha na chenji inabaki. Naamini 2025 kwa mapenzi ya Mungu mama tutakupa kura nydingi sana. Sisi kama Wana-Mara, nami kama mwakilishi wa wanawake kutoka Mara tutampa Mheshimiwa Rais kura za kishindo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee suala la ardhi. Kwa kweli Mabaraza ya Ardhi yamekuwa yakileta kero nyingi sana tena kero zenyewe ni chefuchefu na hasa pale Mabaraza yanapoendesha kesi kwa muda mrefu sana. Mabaraza haya yamekuwa yanaendesha kesi kwa muda wa miaka 10, 20 mpaka 30. Hii wakati mwengine hupelekeea mtu mwenye kesi hiyo anafikwa na umauti hajafaidi ardhi yake; mtu mwengine anakuwa ameshazeeka na mtu mwengine anakuwa ameshazaa watoto na watoto wameshakuwa na wajukuu. Ni suala ambalo siyo zuri sana na ambalo linaleta shida kila siku kwenye ardhi na migogoro isiyokwisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wao kama viongozi, kama waosimamia wasimamizi wa kesi za ardhi, tunawaomba wabadilishe taratibu zao. Hii yote ni kwa ajili ya kutengeneza rushwa ambazo hazijaisha katika ardhi yetu ya Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Waziri wetu, Mheshimiwa Mabula, lakini naomba afanye kazi kubwa sana katika mabaraza haya. Ikiwezekana awabadijishe badilishe, wasikae muda mrefu na ikiwezekana pia afuatilie kujua kwamba ni nani anayesababisha shida hizi zinaendelea? Kwa sababu shida hizi zinazoendelea ni baina ya masikini na matajiri. Ikionekana katika ardhi hiyo masikini au mtu wa hali chini alikuwa anaimiliki ardhi hiyo kama mmiliki namba moja, halafu akatokea tajiri, naye anakuwa na Hati, tena unaiona hati yenyewe inafanana kama ya wiki mbili, lakini inakuwa eti ni Hati ya miaka 20. Ni kitendo ambacho siyo kizuri sana, ni uonevu kwa Watanzania. *Tum-support* mama yetu Mheshimiwa Samia kwa upande wa umilikishaji kwa ili kila Mtanzania aweze kumiliki ardhi na hasa Watanzania wanawake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali; naomba Serikali ifanye *auditing* ya mara kwa mara kwa ajili ya kuangalia kesi hizi: Je, zimetumia muda gani? Zinaendaje? Kusudi kesi hizo ziwe zinatumia muda mfupi kwisha, siyo kesi zinakaa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, suala la ardhi limekuwa ni tatizo kubwa sana na hasa hapa Dodoma. Nasema Dodoma kwa sababu naamini kabisa hata sisi wenyewe Wabunge huku ndani, wengi sana tuna matatizo hayo. Sisi tunataka kulipia malipo ya Serikali ili tupate Hati, tulipie kodi za Serikali lakini wao wanakaa nazo maofisini muda mrefu bila ya kuzifanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili sulla linatakiwa liondolewe kwenye maofisi, wamekuwa wanakula rushwa kupitiliza. Kama wamepewa kazi mtoto wa baba, mtoto wa shangazi kwamba wote ni wakazi wa hapa hapa ambao hawatoki ndani ya ofisi hizo, basi wapishe, kuna watu wengi sana wanatembea na vyeti wamesoma Vyuo Vikuu, wengine ni Maprofesa wanatembea na vyeti vyao mkononi, wapewe kazi hizo wafanye kama wao kazi za ardhi zimewashinda.

Mheshimiwa Spika, pia mimi ni semetu kuhusu viongozi wangu wa Dodoma. Imefikia hatua viongozi kutoka ardhi muone aibu na haya. Kuna vitu mnavifanya vinapitiliza. Mimi kama Mbunge nina mfano hai. Nilinunua kiwanja miaka 10 iliyopita, Iakini hawakuwa wanajua kama ni kiwanja cha Mbunge, bahati mbaya kipindi hicho mimi sikuwa Mbunge. Nikiwa Mbunge sasa nimekuja kufuatilia, eti kiwanja changu kimechukuliwa, kimepelekwa Polisi, kwamba Polisi wanafanya uchunguzi. Hivi sasa uchunguzi unachukua miaka, badala ya waniamble kwamba hiki kiwanja kama ni cha mtu, basi mimi kama Mbunge nitakubali mtu masikini akapewe kile kiwanja. Hata hivyo, ninavyo vielelezo vyote na *document* zangu ambazo ni *original*, ni kwa sababu tu kuna mtu alikuwa anataka kumilikishwa ambaye ameshawapa rushwa, sasa yamewakwama wameshindwa la kufanya.

Mheshimiwa Spika, kama natendewa mimi Mbunge, hivi raia wa kawaida wanatendewa nini? Wanafanyiwa vitu vingapi? Sisi kama Wanakamati kutoka Kamati ya Ardhi tumeshauri mara nyingi, basi wale Maafisa au viongozi walioko hapa maofisini, tunaamini kabisa wala rushwa wanawajua. (*Makofi*)

Mhshimiwa Spika, hili suala linatokea kote ikiwepo hata kwangu Mkoa wa Mara. Kuna wamama masikini wanalia sana, wanaonewa. Kama yeye ni mmiliki namba moja, huyu mmiliki namba mbili anayekuja na Hati ambayo inaonekana ni kama Hati ya jana, lakini huyu mama ana Hati yake ya miaka mitano hadi sita ambayo yeye ndiye mmiliki namba moja. Basi yeye awe na haki kwenye haya Mabaraza ya Ardhi ili kusudi yeye apewe haki yake na huyu namba mbili wakamtafutie hivyo viwanja nya matajiri amilikishwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ardhi imenuka rushwa, imejaa rushwa. Naomba Mheshimiwa Waziri iwe ni sehemu yake ya kwanza sasa kuchanganua au kuwatoatoa wale watu ambao ni wala rushwa na wanafahamika.

(Hapa kengele lilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. AGNES M. MARWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Agnes Marwa kwa sababu wewe ni Mbunge mzoefu, umetoa tuhuma nzito hapo za Ofisi ya Ardhi hapa Dodoma; na kwamba unavyo vielelezo. Kwa sababu Naibu Waziri atapata nafasi ya kuchagia hapa; na sitaki kumwambia kwamba achangie kwenye hoja hiyo, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri ni vizuri kujiridhisha na hiki anachokisema Mheshimiwa Agnes kwa sababu kakisema hapa Bungeni kwamba kiwanja chake na rushwa na vitu kama hivyo. Sasa huenda sababu ni nyngine, siyo rushwa na tuhuma hizo ni nzito kuzisema hapa Bungeni; kwa hiyo, mimi sitaki kulipeleka mbele sana, lakini wewe ufuatilie hiyo hoja halafu utanilettea taarifa.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamwitwa Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo

ya Makazi na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ajiandae.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, nami namshukuru Mungu sana kupata nafasi hii ya kuzungumza katika hii hoja ya Kamati mbili. Hoja yangu kwanza nitajikita kwenye Kamati ambayo imevuta hisia za watu wengi, Kamati ya Maliasili.

Mheshimiwa Spika, sitaki kuchukua muda mwingi kwa pongezi. Umeshapongezwa sana, nami nakupongeza wewe pamoja na wote waliochaguliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengi sana yamezungumzwa hapa na Waheshimiwa Wabunge, lakini kama mtakumbuka siku Mheshimiwa Rais anawaapisha Makatibu Wakuu, alisema tuchague jambo moja kati ya mambo mawili; au tuache Hifadhi ya Ngorongoro ife iwe makazi ya watu moja kwa moja au tuihuishe ile hifadhi iendelee kuishi kwa manufaa yetu na ya vizazi vyetu. Hii ni kauli nzito sana kutoka kwa mkuu wa nchi. Mheshimiwa Rais anataka sisi Watanzania tuchakate halafu tuishauri Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa ushauri wangu ni huu; Waheshimiwa Wabunge, wamesema hapa lakini kwa bahati mbaya sana ukweli huwezi kuufunika. Ukitazama maudhui ya kuwaruhusu wale watu 8,000 waishi mle na wanyama, kulikuwa na masharti yake; usijenge nyumba ya kudumu, jenga nyumba za kimila, ambazo zitawavutia watalii watakapokuja. Sasa ghorofa ni nyumba ya kimila? Siyo nyumba ya kimila!

Mheshimiwa Spika, sasa unapojenga nyumba za kudumu, kwanza wale watu upande mwingine tumewatia umasikini, kwa sababu mle ndani ya hifadhi mtu hamilikishwi ardhi, siyo yake. Sasa kwa nini Wizara isiweke utaratibu mzuri kuwatafutia eneo zuri wale wafugaji na kuwamilikisha? Wapeni hati ili siku nyingine msije mkawafukuza huko

watakapoenda. Wapeni hati za kumiliki ardhi yao pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wapewe hati ili siku nyingine wasije kufukuzwa hapo watakapokwenda, wapewe hati za kumiliki ardhi yao pale na huu utaratibu wa kusema kuna watu maskini wamepewa mifugo, sio tu wa kabilia la Kimasai, hata sisi Wagogo na makabila mengi ya Wasukuma. Sisi tunaita *Ng'ozwa*, mtu anakuwa hana kitu anapelekewa ng'ombe 200, yeye pale anafaidi maziwa kidogo, lakini anakula nyama mpaka ng'ombe afe, sio kwamba achinje hapana, mpaka afe na ngozi anakuwekea tajiri.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Ukija tajiri anakuja kukuonyesha ng'ombe wako fulani alkufa, hao ndio wanaishi mle. (*Makofi*)

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Taarifa inatokea wapi? Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nimpe mwongeaji taarifa kwamba, amesema wale watu Serikali inaweza kuwajengea nyumba sehemu nyingine na kuwahamisha. Nakubaliana naye kwa kumpa taarifa kwamba, wale watu wanatumia shilingi bilioni tatu kwa mwaka kwa ajili ya chakula.

Kwa hiyo, fedha hizo zikienda kujenga nyumba zao wakamilikishwa ardhi, wakajengewa shule hospitali na kadhalika, inawezekana. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Kweli.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, hilo nimelipokea na ndio maana nilitaka nijenge hoja yangu... (*Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Lusinde subiri kidogo. Naona unafanya haraka sana, lazima nikuite tena ndio uzungumze. Mheshimiwa Lusinde.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana tuna Spika wa viwango. Hebu mpigieni makofi Spika haraka sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ndio maana nilitaka nijenge hoja yangu hivi katika nchi nzima ambayo watu wote sisi tunaishi kwa usawa, leo unakuwa na Tarafa moja ambayo ukifuga humo ndani ya hiyo Tarafa hao wote wanaoishi humo watanunuliwa chakula bure. Hao watu wanaoishi humo madawa ya mifugo yote watapata bure, hao watu wanaoishi humo watoto wao watasomeshwa mpaka Chuo Kikuu bure. Nani atakataa kwenda kuishi kwenye hiyo Tarafa? Sisi wenyewe tuna mpango hapa wa kuhamia huko. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, maana yake kuzuri kuna kila kitu ambacho unapewa bure. Kwa hiyo, nataka kusema hivi kama tumefuatilia mitandao na tumeona zile picha, kama za uongo Serikali wasimamie hili jambo ili kutenda haki. Mle ndani wameonekana mbwa kama yule mbwa wa Wema Sepetu anaitwa Nunu, wako kule Ngorongoro, wako. Kuna mbwa *German Shepherd* wako mle Ngorongoro. Sasa tunajiuliza hivi mbwa kama yule atakaaje na wanyama wa kawaida? Ndio maana wanyama wanakimbia wanawaacha watu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nikwambie kengele ile ya kufunga ng'ombe shingoni ile sisi tunaita *chidodolo* kwa sisi Wagogo. Ile kengele ikilia paaaa mara moja hivi, faru anakwenda kusimama Morogoro *speed* yake. Sasa niambie huyo faru atarudi saa ngapi mpaka mtalii aje amwone? Kwa hiyo, ndugu zangu tukubaliane kwamba haiwezekani, kwa hali tuliyonayo sasa kuchanganya kati ya watu pamoja na hifadhi kuishi mule ndani haiwezekani. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ukitaka upime kwamba utajiri sasa unaanza katuondolea utu. Tumepata taarifa mle kuna vijana

watatu wameliwa na simba na picha zao zimeonyeshwa. Umeona hata mtu mmoja hata Mbunge wa eneo hilo au wahusika wa eneo hilo wametoa hata pole? Jamani maisha gani haya, haya ni maisha gani? Nataka niwape pole familia ambazo kwa namna moja au nyngine wamewahi kudhurika na wanyama. Tuwape pole wenzetu ambaao wamepoteza watoto wao kwa nyakati fulani kwa kuliwa na simba. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hatuwezi tukaishi maisha hayo yaani mali inatuondolea hata utu wa kushindwa kuthamini kwamba wenzetu wanaishi mule wengine wanajeruhiwa. Haiwezekani, vinginevyo watuambie kwamba ule ni uongo na wachukuliwe hatua. Hata hivyo, kama unaweza ukafuga mbwa mle hatari kabisa, mbwa wakubwa kama wale, niwaombe matajiri wachache ambaao wananaufaika na ile mifugo na Serikali twende tukafanye sensa. Serikali ikitaka *ku-prove* hilo wafanye sensa, wale kondoo wamebekwa mpaka bei. Kondoo mmoja anauzwa Shilingi laki tano halafu mimi nibaki masikini, nani kakudanganya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni wazi huyo kondoo sio wake. Kwa hiyo, watu wanafuga kondoo wakubwa mle kwa sababu huduma zote ni za bure, halafu wanakwenda kuuza wanapata fedha wanununa VX, yule mchungaji yuko mule anabaki na umasikini wake. Asikudanganye mtu zile familia za wale wanaochunga haziwezi kusoma, kwa sababu baba hachungi kila siku, siku ya pili anaachia watoto. Wanaacha kwenda shule anasema mkafanye kazi ya tajiri, ndio wale watoto ambaao tunaona picha zao zinarushwa kwenye mitandao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka *ni-conclude*, sio kwamba naunganisha kama Waziri, lakini nataka niseme hivi, naunga mkono hoja hii. Serikali naomba niwashauri wale watu watafute namna ya kuwaondoa mle kwa namna mbili; wanaotaka kuondoka kihiarri waondoke kihiarri kuanzia sasa. Wakajipange waorodhoshe watu wanaotaka kuhama, wahame, wwaape kifuta jasho chao, watafute eneo la kuwapeleka. Wanaotaka kuondoka kwa sheria, Serikali ilete

sheria tubadilishe waondoke kwa sheria. Yote hayo mawili yafanyike, (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba yote mawili yafanyike; anayetaka kuhama kwa hiari ahame kwa hiari, anayetaka kuhama kwa sheria, sheria sio msahafu, iletwe hapa tuibadili, sisi ndio watunga sheria, aondoke kisheria. Yote hayo yanawezekana nchi si ya kwetu jamani? Wataondoka kwa sheria, kama kuna mafao walipwe waende na huko wanakokwenda wapewe hati za kumiliki ardhi. Tusiwapeleke tena kwenye eneo la kuwapangisha. Maisha yao yakishaanza kuwa mazuri tutasema tena hapo hameni hapana. Tuwatengenezee *structure* nzuri ya shule. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2018 wote kulikuwa na kipindupindu kwa mwaka mzima hakikuondoka. Leo hii tunashindwa kuhurumia hawa watujamani? Mtu anawezaje kukaa na kipindupindu kwa mwaka mzima watu wangapi wamepotea pale? Watu wangapi wamedhurika pale? Lazima tuangalie maisha ya watu. Pia mle ndani kuna minada, jana nimeona kwenye gazeti limeandika. Kuna minada miwili kila wiki, minada unajua inavyokusanya watu wengi, magari mengi, sasa mnyama gani atastahimili hiyo hali jamani? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Serikali Waziri alete hapa habari wanaohama kwa hiari waorodheshwe, wahamishwe, Serikali ikafanye sensa. Kila mtu asimame na mifugo yake utashangaa hali za wale watu na mifugo wanayomiliki pale. Hapo ndio tutajua akina nani wanafugia pale na inawezekana, hata wale wanaochunga ile mifugo hawalipwi hata fedha. Anaambiwa kunywa maziwa tu, ng'ombe hizi ni za bwana mkubwa. Hii haiwezekani katika nchi yetu, mtu unaishi unawafanya wenzako kama watumwa, katika nchi ambayo tumedai uhuru na tumepigania uhuru wa nchi hii. Hilo jambo haliwezekani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niiombe Serikali ije na tamko rasmi wanaohama waanze kuhama mara moja sio suala la kuchelewa. (*Makof*)

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. LIVINGSONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, sio suala la kuchelewa.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Lusinde kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ole Sendeka.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, nataka nimpe rafiki yangu na mdogo wangu Mheshimiwa Mbunge wa Mtera taarifa, kwamba, kama pendekezo ni kuwahamisha wafugaji au kuleta sheria ya kuwaondoa wafugaji waliko Ngorongoro, mkataba uliokuwepo ni kwamba walitoka Serengeti kuja Ngorongoro. Kama mna mawazo hayo maana yake mtenge, mrudishe...

SPIKA: Hapana. Mheshimiwa Ole-Sendeka ngoja kwanza. Unazungumza kana kwamba Bunge limefanya maamuzi, hayo ni mawazo ya Mbunge mmoja aliyesimama kuchangia. Tusije tukatuma ujumbe huko nje kana kwamba kuna watu wamekaa mahali halafu msemaji wao ni Mheshimiwa Lusinde hapana. Yeye anachangia kama Mbunge mwengine sasa usifike mahali unasema kama mawazo yenu, akina nani sasa? Kama maamuzi yenu, akina nani sasa? (*Makofi*)

Hapana, ni Mheshimiwa Lusinde anachangia na wewe unataka kumpa taarifa kama unayo taarifa mpe. Kama ni hicho ulichotaka kusema nadhani hicho ukishikilie kwanza. Bunge halijafanya maamuzi yoyote mpaka sasa. (*Makofi*)

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, nakuheshimu sana, nakaa.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Lusinde malizia mchango wako.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, basi nami nachukulia kwamba, kaka yangu hajasema chochote, naendelea. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naendelea kuishauri Serikali ifanye mambo mawili. Ilete hapa orodha ya wananchi wanaotaka kuhama kwa hiari, iwasaidie kuhama. Wasije kuwa wanatishwa, wengine wanakaa mule kwa nguvu kwa sababu, kuna mabwana wakubwa wana mabavu wanawatishia. Wanaotaka kuhama kwa hiari Serikali iweke wazi orodha yao na waondoke eneo lile. Wanaotaka kuhama kwa mujibu wa sheria Serikali ilette sheria tubadilishe, wahame kwa mujibu wa sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete. Atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii ajiandae.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote na mimi niungane na wenzangu kukupongeza. Pamoja na hayo yote pia niendeleee kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya yako na unavyoendelea kutuongoza.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja nzuri iliyowekwa mezani hapa na Kamati yetu, kwa sababu ukiangalia hoja zao zote wametoa mawazo mazuri. Mawazo ambayo yanaendelea kutuimarisha sisi kama Wizara ya Ardhi, lakini pia kuishauri Serikali juu ya nini kifanyike. Yapo maeneo ambayo nataka nichangie kidogo ili kuweka zile taarifa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza limezungumzwa hoja ya kukwama kwa miradi mikubwa minne ya Shirika la Nyumba. Pale katika Mkoa wa Dar es Salaam wakimaanisha *Plot No.*

300 ya *Regent*, Plot No. 711 na nyingineyo ikiwemo ya *Morocco Square*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika moja ya mawazo mazuri yaliyotolewa na Kamati ni kwa...

Mheshimiwa Spika, nisamehe kidogo unajua tumeshazoea. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Hakuna neno Naibu Spika ni msaidizi wangu kwa hiyo usiwe na wasiwasi. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA

MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wewe ndio mkuu wa Mhimili basi watu wote wako chini yako.

Mheshimiwa Spika, nataka nieleze kwamba Serikali imefanya juhudni kubwa sana kuhakikisha kwamba, miradi ile inakwamuka kutoka pale ilipokwama ili sasa iweze kukaa vizuri. Katika hatua ambazo tumefanya ndani ya Wizara ilikuwa ni kuomba Serikali itupe ruhusa, ya kuchukua fedha au kupata fedha kutoka ndani ya vyanzo vyetu. Ikiwepo *almost* karibu Shilingi bilioni 700 ili twende tukafanye utaratibu huo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan akaelekeza Kamati, inayosimamia madeni iangalie vizuri juu ya yale ambayo sisi tumeyaomba. Katika kuchakata kwake ikaturuhusu tukope, Shilingi bilioni 44.7 ili tuweze kumalizia miradi hiyo. Katika fedha hizo ambazo zilielekezwa Shilingi bilioni 19 ilikuwa ni kwa ajili ya mradi uliopo katika Plot No. 300 na iliyobakia iende kumalizia *Morocco Square*.

Mheshimiwa Spika, juu ya lile eneo la Kawe maelekezo yako wazi kwamba, tukae na mbia katika ule Mradi wa Kawe ili tuweze kuzungumza naye na baada ya kumaliza kuzungumza naye, basi makubaliano tutakayokubaliana nayo tuone tunakwendaje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hatua iliyofikiwa mpaka sasa baada ya mikutano mitatu ni kwamba mbia wetu anakwenda kuwasiliana na wenzake ndani ya Bodii yao, ili yatakayokuwa yamekubaliwa basi tuje kuzungumza kwa pamoja ili tuweze kwenda vizuri. Kwa faida ya kikao hiki eneo ambalo limejengwa yale maghorofa unayoona Kawe pale, ni eneo ambalo miliki yake iko chini ya *National Housing*. Kwa hiyo, mazungumzo yanayofanyika ikiwezekana ni kutoa kile kipande, cha lile eneo ili sasa tuweze kupewa nafasi sisi wenyewe. Tuweze kujenga majengo yale ili majengo yakae vizuri na Watanzania, wapangishe na yanayouzwa yauzwe ili sasa tuweze kupata faida ya mradi ule.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo pia ndani yake limezungumzwa na ushauri mzuri umetolewa na Kamati, juu ya Serikali kutochangia fedha katika miradi ya upimaji, upangaji na umilikishaji. Nataka nillhakikishie Bunge lako kwamba, neno hili halina ukweli wowote. Serikali imekwishatoa fedha na maelekezo yametolewa juu ya kuhakikisha kwamba, miradi hii inakwenda kupangwa vizuri. Katika kufanya jambo hilo fedha Shilingi bilioni 50 zimetolewa na zimekwenda kwenye Halmashauri zaidi ya 44 ili Serikali au Halmashauri zetu zikapime vizuri maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa furaha kubwa zaidi katika bajeti inayokuja Serikali inapanga kutumia zaidi ya Dola milioni 150, ambayo ni sawa na Shilingi bilioni 400 kwenda kuwasaidia zaidi kuendelea kupanga nchi yetu. Pia kuendelea *ku-finance* hii miradi ya upimaji, upangaji na umilikishaji.

Mheshimiwa Spika, yako mengi ambayo Serikali inaendelea kufanya, lakini nataka niwahakikishie kwamba mifumo, iko tayari kwa ajili ya kukabiliana na changamoto za ardhi nasi ndani ya Wilzara tunaendelea kutoa elimu pale ambapo tunapata nafasi. Sera zile ambazo zimepitwa na wakati, zimeendelea kupelekwa katika vikao husika ili ziweze kuhusishwa. Halafu baada ya hapo Serikali au wadau mbalimbali, tuendelee kuhimiza katika mipango mizuri ya usimamizi wa ardhi ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mhandisi Hamad Masauni Yusuf, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii na Waheshimiwa Wabunge baada ya hapo, atazungumza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii ya kuweza kuchangia. Nianze kukupongeza wewe binafsi kwa kuweza kuchaguliwa kwa kura za kishindo, kuwa Spika wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia nichukue nafasi hii kuishukuru sana Kamati yetu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Zungu, ambaye na ye ye nimpongeze kwa kuweza kuitishwa na Chama chetu kuwa Mgombea wa Naibu Spika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Kamati hii kwa muda mfupi ambao nimeweza kushirikiana nayo imetupa ushirikiano mzuri sana. Nafarijika sana kuwa ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati hii. Kwa hiyo nawashukuru sana, nawapongeza sana kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kufanya. Hata hivyo, pamoja na taarifa nzuri ambayo imewasilishwa hapa leo, nataka njikite katika maeneo kama matatu hivi ambayo Kamati iliyazungumzia lakini na baadhi ya Wabunge waliyagusia ni kwa upande wa Jeshi la Magereza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja mbili kwenye Jeshi la Magereza. La kwanza, ilikuwa ni jinsi gani Jeshi la Magereza linaweza likajitosheleza na chakula, lakini na la pili, ilikuwa linahusu hoja ya kupunguza msongamano kwenye Magereza yetu. Sasa nasema hoja hizi mbili naweza nikazichangia kwa pamoja kwa sababu zinaingiliana. Kwa nini nasema zinaingiliana? Tunapozungumzia dhana nzima ya Magereza kujitosheleza na chakula ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Spika, haiingii akilini kabisa kwamba Jeshi la Magereza, ambalo lina rasilimali ardhi yenyе rutuba ya kutosha, lakini tunasema ina nguvu kazi pia ya kutosha, iwe inaendelea kutegemea ruzuku ya Serikali katika kuhudumia wafungwa. Imani yangu ni kwamba sio tu kwamba linaweza kujitosheleza na chakula, lakini linaweza likazalisha ziada kwa ajili ya kuweza kulipatia Jeshi la Magereza mapato yatakayosaidia kupunguza changamoto mbalimbali za Jeshi letu. Sasa ninaposema hizi hoja zinaingiliana nina maana gani? Hivi tunavyozungumza mpaka leo tuna takribani watu bilioni 32, ambao kati ya hao kama milioni 18.2 ndio wafungwa, lakini kuna milioni 13.8, hawa ni mahabusu.. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunapozungumzia suala la wafungwa kuwatumia kama nguvu kazi ya kulima ili tujitosheleze na chakula, kuna changamoto lazima tuje na mawazo na ubunifu mwингine wa ku-*address* jambo hili. Kwa sababu, hatuwezi tukasema kwamba katika karne hii tunayoendelea wakati hoja ya kutaka kupunguza wafungwa Magerezani inakuwa ina umuhimu wake mkubwa, halafu tuseme tuwa-*retain* wafungwa hawa kwa sababu, eti tunataka watusaidie kujitosheleza na chakula.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapa kuna vitu lazima tuvi-*address* kwa kutumia ubunifu wa hali ya juu. Ndio maana tumeamua sasa hivi kuja na utaratibu ambao nataka niueleze hapa kwa ufupi. Utaratibu huu utasaidia sana kulifanya Jeshi letu la Magereza, liweze kujikita zaidi na lile jukumu lake la msingi la kurekebisha wafungwa. Kumekuwepo na baadhi ya hoja kwa baadhi ya watu wanasema, baadhi ya wafungwa wanaweza wakaachiwa sasa hivi, halafu baada ya muda mfupi wanarudi kuwa wahalifu. Nasema pengine kwa sababu labda, Jeshi la Magereza linajikita sasa katika kufanya mambo mawili kwa pamoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo Jeshi la Magereza tunasema lirekebishe wafungwa ambalo ni jukumu lake la msingi, lakini tunasema wakati huo Jeshi la Magereza tunataka lijitosheleze na chakula, liweze kubuni miradi

mbalimbali, viwanda na kadhalika. Basi mambo haya tunataka tuyafanye kwa pamoja, lakini kwa utaratibu ambao utatenganisha majukumu yake. Ndio maana tuna mkakati kabambe wa kuhakikisha kwamba mashirika yote ya uzalishaji mali katika Majeshi yetu, ikiwemo Jeshi la Magereza yanasisimama na kuijendesha kibiashara. Ili kuliacha Jeshi la Magereza kama Jeshi kufanya kazi zake za msingi za kurekebisha wafungwa na mengineyo yaliyopo kwa mujibu wa Katiba pamoja na Sheria za Nchi yetu na Kanuni zake. Katika kufanya hivyo ni imani yetu kwamba... (*Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Sekunde chache malizia.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, kuna mambo ambayo kama Serikali yanaendelea kufanyika. Nimpongeze sana Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, katika sherehe za Uhuru hivi karibuni amesamehe wafungwa, zaidi ya 5,704. Hizi ni katika jitihada za kupunguza msongamano magerezani. Kana kwamba hiyo haitoshi, kuna hatua nydingi ambazo tunaendelea, kuzichukua na tunaamini hizi zitasaidia kupunguza msongamano wa wafungwa. Moja, tuna sheria zetu kuna Sheria ya *Parole*. Kuna Sheria ya... (*Makofi*)

SPIKA: Sasa, Mheshimiwa Waziri muda umetutupa mkono.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita Waziri wa Maliasili na Utalii, kanuni ya 34(5) inanipa fursa ya kuongeza muda kwa kadri nitakavyoona inafaa na sio lazima niwahoji Wabunge. Kanuni hiyo niliyoitaja inasema hivyo. Kwa hiyo, naongeza muda mpaka tutakapomaliza shughuli hii iliyo mbele yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ya kuweza kuongea na Waheshimiwa Wabunge waliopo humu ndani na kupitia Bunge lako Tukufu kwa Watanzania wote. Nina mambo manne ambayo ningependa kuyasema. Jambo la kwanza nichukue nafasi hii kuishukuru sana, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Kwa taarifa nzuri ambayo wamewasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu. Wameainisha maeneo ambayo tumefanya vizuri na pale kwenye changamoto wametueleza ili sisi tuweze kutekeleza vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikuahidi, Wizara tumepokea ushauri huo na tutaenda kuutekeleza; na utekelezaji huo unaanza leo. Kwa hiyo, kuanzia kesho mkiona utekelezaji unaendelea, msishangae, Serikali hii ni Sikivu. Tunasikia maoni ya Waheshimiwa Wabunge na tunayaafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, watu wameongea sana na wanaendelea kuongea. Jambo moja lilioongelewa ni kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii inataka kuwapokonya ardhi Wamasai. Naomba nitoe angalau ufanuzi kidogo. Tanzania hakuna mwenye ardhi, hakuna kabilia lenye ardhi Tanzania, ardhi yote ni mali ya Mheshimiwa Rais. Kwa mujibu wa sheria tulizozitunga humu ndani, anaweza akaitwaa muda wowote. Haki ya wewe ambaye ardhi hiyo inatwaliwa ni fidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wameongea Waheshimiwa Wabunge hapa kuhusiana na mambo ya fidia. Hii dhana ambayo inakwenda na mpaka vyombo vyua nje vinaandika: "*Government of Tanzania is Grabbing Maasai Land,*" ni upotoshaji! Hakuna sheria hiyo. Tukienda huko tutarudi wakati wa ukoloni, tutasema *Ngoni Land, Sukuma Land, Nyakyusa Land*; tulishatoka huko toka mwaka 1963. Kwa hiyo, turudi kwenye msimamo, tuelewe mwenye ardhi ni nani; na mamlaka yake ni yapi kwa mujibu wa sheria ambazo

tumezitunga? Tukitaka kumnyang'anya Mheshimiwa Rais mamlaka hayo, tuje tutunge sheria, tuseme kuanzia sasa ardhi imilikiwe na makabila kama zamani. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri hapo kwenye ardhi kumilikiwa na Rais, nadhani upaweke vizuri kisheria. Ardhi inamiliikiwa na Umma, Rais anaishika kwa niaba ya Umma. Sasa isije ikaleta picha ambayo pengine inaweza kusababisha mkanganyiko. Ardhi ni ya Umma wote wa Watanzania lakini Rais anaishikilia hiyo ardhi kwa niaba yetu sisi sote. (*Makofi*)

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa mwongozo wako. Nilichokuwa ninasisitiza hapa ni kwamba, kwa sababu ardhi ni ya Umma, hakuna kabilia moja linalomiliki ardhi. Ni Umma wa Watanzania wote; ndiyo maana ukienda Zanzibar utawakuta Wangoni wanakaa kule; ukija Songea utawakuta Wamasai wapo kule, kwa sababu ardhi ni ya Umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu ambayo ningependa kuiongea ni suala la haki za binadamu, limeongelewa sana hapa. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tazania inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, ni Serikali inayojali haki za binadamu. Hatutafanya chochote kinyume cha haki za binadamu. Kwa kuwa tunaheshimu haki za binadamu, pia hatutaingilia uhuru wa vyombo vyahabari kwa sababu ni haki za binadamu, lakini kama umekwazwa na vyombo vyahabari, mamlaka za kisheria zipo. Unaweza ukaenda Mahakamani au *TCRA* kwenda kuvishtaki. Ila Serikali ikikifungia chombo cha Habari, ni ukiukwaji wa haki za binadamu, hatutafanya hilo.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo ningependa kulisema, watu wameongelea hapa Sheria ya Ngorongoro ya Mwaka 1975. Toka imetungwa ni miaka mingi sana. Mliyoyaongea Waheshimiwa Wabunge yameonesha mapengo yaliyopo kwenye sheria ile. Msingi wa sheria ile ni nguzo tatu; nguzo ya uhifadhi, nguzo ya utalii na nguzo ya maendeleo ya jamii. Inaonekana nguzo hizi sasa

zimeshindikana kushikiliwa kwa Pamoja. Kwa hiyo, sasa kwa mapendekezo ya Kamati na maoni yenu, sisi kama Wizara mapema iwezenkenavyo tutaleta mabadiliko ya sheria hii na endapo Bunge hili Tukufu litaridhia, basi yataweza kupita na kuamua kwa mujibu inavyofaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nisistize kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo Mheshimiwa Rais amenipa mimi na Mwenzangu Mheshimiwa Mary upendeleo wa kuisimamia, tutahakikisha haki ya kila Mtanzania wakiwemo Wamasai walipo Ngorongoro inalindwa. Hakuna litakalofanyika kinyume cha sheria wala kuvunja haki zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge kabla hajawa Mbunge alishakuja ofisini akiwa Mwenyekiti na alikuja kuongelea haki za watu wa Ngorongoro. Hakuwa Mbunge lakini nilimpokea, tukakaa na tukaongea na nikamweleza msimamo kwamba tunapenda haya mambo yaende kwa kuelewana, kwa kukaa Mezani pasipo kumkandamiza mtu. Hiyo ndiyo *approach* ya Serikali, tufike sehemu tutatue tatizo pasipo kukwaruzana; wale wapate haki yao na Serikali ipate ambacho ni haki ili Ngorongoro isife. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii na ninawapongeza sana Kamati kwa taarifa hiyo nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, leo naye anapata nafasi ya kuchangia Bungeni. Karibu sana. (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu kwamba nimesikiliza mjadala unaogusa maeneo ya Ngorongoro na Loliondo juu ya mahitaji makubwa ya uhifadhi wa maeneo haya kwa maslahi ya Taifa. Ni kweli upo mgongano mkubwa unaotokana na sheria tulizonazo, lakini pia matakwa binafsi ya mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, vile vile Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo ya kukutana na ndugu zetu waliopo pale. Kazi hiyo tumeshalianza. Jumapili iliopita nilianza na kazi hiyo nikakutana na Uongozi wa Mkoa wa Arusha, nimewasikiliza, nimekutana na Wizara pale Arusha, nimewasikiliza na sasa hatua iliyobaki ni kwenda Ngorongoro. Nitafanya mikutano na wananchi wa eneo la Ngorongoro, nitafanya mikutano na wananchi wa eneo la Loliondo ambako pia mwaka 2017/2018 tulifanya mikutano mingi sana kueleweshana juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, haya yote na mjadala unaoendelea hapa Bungeni wapo ambao wanaelewa mazingira yaliyopo kule, lakini wapo Wabunge ambao hawajui mazingira yaliyopo pale. Huku tukiwa tunazungumza na wananchi kule, naiagiza Wizara ya Maliasili na Utalii kufanya semina siku moja kwa Wabunge wote ili Wizara iwaambie kuna nini kule Ngorongoro? Nini kilikuwepo awali na ni hali gani ambayo ipo sasa? Hii itasaidia tuwe na uelewa wa pamoja hata haya mapendekezo ya Mheshimiwa Waziri ya kutaka kuja kubadilisha sheria, mnaweza kuunga mkono au kutokuunga mkono baada ya kujua nini kinaendelea kule? Hatua hii ndiyo itawezesha kuendesha zoezi hili kwa amani kabisa kadri itakavyokuwa imeamiриwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo njia sahihi ambayo pia nilliona nipate muda huu niweze kutoa maelekezo kwa Wizara na pia Wabunge mpate kuelewa jambo hili. Tutakwenda kwa wananchi; tumeanza kwa hatua hizo ambazo nimezieleza, tumzungumza na Wizara, tumezungumza na Mkoa ambao unasiimamia jambo hili ambapo pia TAWA, TANAPA pamoja na Ngorongoro walikuwepo, na hao sasa nawataka kupitia Wizara waje hapa Bungeni wawaelimishe Wabunge, mjue mazingira yaliyopo pale. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ili kumaliza jambo hili, kwa kadri ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kutatua tatizo hili bila kuwa na mgongano kati ya wananchi walipo pale na maamuzi ambayo yanaweza kufikiwa, lazima tukae pamoja ili tuweze kumaliza.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hayo tu. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tunaamini hayo maelekezo ya semina Mheshimiwa Waziri yupo hapa na Naibu Waziri, basi watafanya utaratibu mzuri kwa kadri ya maelekezo hayo ili wote tuwe na uelewa wa pamoja, itatusaidia.

Waheshimiwa Wabunge sasa niwaite watoa hoja ambao watatumia muda mfupi sana ili waweweze kuturuhusu Wabunge tufanye maamuzi juu ya mapendekezo na maoni ambayo wameyatoa kwetu. Nianze na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii aje ahitimishe hoja yake.

MHE. ALLY J. MAKOA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGЕ YA ARDHІ, MALIASILI NA UTALII:
Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri ambayo kwa kweli imezidi kutuimarisha na ninadhani Serikali imesikia. Ninawashukuru Mawaziri waliochangia lakini kipekee kabisa nimshukuru Waziri Mkuu kwa maelekezo yake mazuri ambayo ameyatoa hapa mbele ya Bunge, ni matumaini ya Kamati kwamba sasa Serikali itakwenda kuyafanya kazi mawazo ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, pamekuwa na hisia kubwa sana kwa upande wa Ngorongoro lakini lazima na Bonde la Kilombero na lenyewe litiliwe mkazo kama jinsi ambavyo Ngorongoro inavyotiliwa mkazo kwa sababu Bonde lile na lenyewe likiachiwa yatakuja kutokea madhara makubwa pengine kama haya yanayoweza kutokea Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, sasa ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge likubali kupoipokea taarifa yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja iliitolewa iamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana. Sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambayo taarifa hii ina maoni na mapendekezo ambayo yaliletwa kwetu na sasa tunafanya maamuzi juu ya yale mapendekezo yaliyoko kwenye hiyo taarifa. Wanaokubali waseme ndiyo.

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

SPIKA: Wasiokubali waseme siyo.

WABUNGE FULANI: Siyo.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hizi taarifa ni za Bunge, sasa ukisema siyo, sijui unakuwa una lengo gani? Illa waliosema ndiyo wameshinda.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilipitishwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Vita Kawawa anakuja kuhitimisha hoja.

MHE. VITA R. KAWAWA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGЕ YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Spika, kwanza nami naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuja kuifunga hoja yetu hii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi, Usalama. Katika eneo letu walichangia watu watatu na mmoja ni Waziri wa Mambo ya Ndani, kwa sababu mijadala hii inaonekana eneo kubwa limechangiwa sana na Kamati

ya Maliasili na Utalii. Kwa hiyo, waliochangia kwenye Kamati yangu ni Mheshimiwa Chumi, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na Mheshimiwa Mkenge.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Chumi alizungumzia sana ongezeko la biashara (*balance of trade*) katika Kanda zetu za Afrika Mashariki na Jumuiya ya *SADC*. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwanza kwa kuifungua nchi yetu. Rais wetu Mheshimiwa Mama Samia alipoapishwa alifanya ziara katika nchi za Afrika Mashariki na nchi za *SADC*. Hii imesaidia sana katika biashara yetu na tumeelezwa katika Kamati kwamba Itifaki ya Biashara ya mwaka 1996, nchi wanachama wa *SADC* zinatekeleza na zinaondoa vikwazo ambavyo vinasababisha biashara isifanyike vizuri.

Mheshiwa Spika, kwa hiyo, hii imesaidia baada ya Mheshimiwa Rais kwenda kuzungumza, sasa urari wa biashara umeongezeka kwa asilimia kubwa. Kwa mfano, nchi yetu katika kipindi hiki tumeweza kuuza na kupandisha biashara katika kipindi cha mwaka 2021 kutoka dola 1,235,000 mpaka dola 1,458,000 katika ukanda wa *SADC*. Takwimu zinaonesha kwamba *balance of trade* kwa mfano kati yetu na *South Africa*, sisi tunauza zaidi *South Africa* kuliko wao wanavyonunua kwetu sisi. Hii imetokana na juhudini kubwa za Mheshimiwa Rais na Wizara ya Mambo ya Nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Chumi alizungumzia kidogo kuhusu Kamati ya Mawaziri Nane ambao walienda kutaka kutatua migogoro vijijini. Mwaka 2021 Kamati ililetewa tatizo lilitokuwa limejitokeza Mbarali; kuna vijiji ambavyo vilikuwa vinaingiliana na eneo la maliasili na kulikuwa na mauaji ya watatu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika kulishughulikia suala lile, tulilopewa na Spika tuliwaita pia Mawaziri wa Kisekta ambao mmojawapo walikuwa hawa wanane na tulishauriana nao tukawaambia waende wakakamilishe lile zoezi walilolifanya la kuzunguka nchi nzima na wallifanya kazi hiyo, wamezunguka na wakatoa kauli. Sasa Kamati inaishauri

Serikali imalizie ile kazi nzuri waliyoifanya ya kuwapa vijiji vile maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, mwisho Mheshimiwa Mkenge naye alizungumzia mambo ya *NIDA*, pia amepongeza sana; amezungumzia mtangamano wa Jumuiya ambao nimishauelezea. Vile vile amezungumzia kuhusu *MSD* kuteuliwa kuwa *supplier* wa dawa katika nchi za Kikanda za *SADC*. Sisi tunaipongeza sana juhudini ambazo zimefanywa na Wizara ya Mambo ya Nje kushawishi mpaka nchi yetu kuteuliwa kuwa eneo ambalo litakuwa *supplier* mkubwa wa dawa katika nchi za *SADC*. Kwa hiyo, hili tunaliunga mkono. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia tunaipongeza Nyumbu kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kamati inaishauri Serikali kwamba iendelee kuipa Nyumbu fedha za kutosha kuweza kufanya kazi yake nzuri kwa sababu sasa hivi inatengeneza magari ya *fire* ambapo tuna uhada sana wa magari ya *fire*. Kwa hiyo, tunapenda sana iwe inapewa fedha za kuweza kufanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Spika, mwisho Mheshimiwa Chumi alizungumzia pia kuhusu Maafisa wa juu wa Magereza, ni kweli ili kuleta mageuzi katika Jeshi letu la Magereza, Kamati inaishauri Serikali kuziba nafasi zile za Maafisa wa Juu kulingana na Muundo wa Jeshi la Magereza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naliomba Bunge lako Tukufu kuunga mkono hoja Kamati yetu ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja lliamuliwa na Kuafikiwa)*

SPIKA: Hoja zote mbili zimeafikiwa.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Naomba ukae Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge, kazi yetu ya leo ilikuwa ni hizi Kamati zetu mbili za Kudumu za Bunge ambazo zimeleta taariza zake mbele ya Bunge letu hili ili watueleze mambo yaliyofanyika na ambayo hayajafanyika na watoe maoni na mapendekezo, halafu kwa utaratibu wa Kanuni zetu, wakishalea kwetu maoni yao, ndiyo maana tunatoa michango. Pia wanaleta mapendekezo ambayo nasi tukiafikiana nayo, ndiyo mwishoni hapa tunahojiana kwamba tunakubaliana nayo. Ndivyo Kanuni zetu zinavyosema.

Sasa tukishahojiana hapa ndani na wale waliosema ndiyo wakawa wameshinda, maana yake maoni tuliyoyatoa humu na mapendekezo tuliyoyatoa kwenye zile taarifa, sasa yale ni maoni ya Bunge kuelekea kwa Serikali na ni mapendekezo ya Bunge kuelekea kwa Serikali.

Kwa hiyo, Serikali inachofanya, inayachukua maoni na mapendekezo yetu na kuanza kuyafanyia kazi. Ndiyo utaratibu ulivyo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa niweke vizuri hili kwa sababu Waheshimiwa Wabunge hatujapata muda sana wa kusoma Kanuni zetu nyingi. Muda umeenda sana, lakini Kanuni ya 64; ikiwa Mbunge ana jambo lolote ambalo baada ya taarifa ile kuwasilishwa anataka jambo fulani hivi libadilishwe; Kanuni ya 64 inamruhusu kufanya hivyo. Yeye anamwandikia Katibu hapa, kwa sababu taarifa zile huwa zinaanza mwanzoni kabisa kabla hata watu hawajaanza kuchangia.

Kwa hiyo, inaposomwa hapa na Mwenyekiti na wewe unafuatilia unaona mapendekezo haya hapa wangeongeza neno hili, hapa wangepunguza neno hili, ni wakati ule tunapoendelea na mjadala unamwandikia taarifa hiyo Katibu unaweka Saini yako. Halafu Bunge tutaangalia yale uliyoyaleta wewe na yale walijoyaleta Kamati, tuchukue wazo lipi, tuwahoji Wabunge?

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa sababu hapa nimewahoji na sikupokea taarifa yoyote kwamba kuna mabadiliko sehemu yoyote kwenye hizi taarifa za Kamati, maana yake maoni na mapendekezo kama yaliivoletwa na kamati ndivyo Bunge hili linavyoyapeleka Serikalini. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, hili ambalo limeleta changamoto kidogo ama limeleta mjadala mkubwa pengine siyo changamoto; ukurasa wa 37 mpaka ukurasa wa 38 ndiyo utakaoeleza sasa kwamba Bunge limeamua nini kuhusu jambo hili? Tuelewane vizuri Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu tumeshahojiana kuhusu maoni haya na mapendekezo haya.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu hili la Ngorongoro na watu wasije wakaleta upotoshaji wakaanza kutoa maneno ambayo hayamo kwenye yale ambayo Bunge limeamua, hayo nalazimika kidogo kutoa huo mwongozo kwa sababu tumeshapata changamoto hapa karibuni.

Waheshimiwa Wabunge, ukurasa wa 37 na nitaenda moja kwa moja, "KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kutekeleza mambo ya fuatayo; Moja, kuharakisha mchakato wa kufanya tathmini ya kina kuhusu mfumo wa matumizi ya ardhi katika eneo hilo ili kusaidia kufanya marekebisho ya sheria iliyoanzisha Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ili kuendana na hali halisi iliyopo sasa.

Pili, (ukurasa wa 38) Serikali itafute namna bora ya kushughulikia changamoto za eneo la Hifadhi Ngorongoro juu ya wananchi na mifugo ndani ya eneo hili."

Hayo, hayo ndiyo mapendeleko ya Bunge hili kwa Serikali. Sasa usitokee upotoshaji hapa na pale wa kuonesha kwamba Bunge pengine limeamua tofauti na hilo.

Sasa nitampa fursa Mheshimiwa Masauni kwa dakika moja, kuna takwimu alikuwa amezitaja hapa kuhusu idadi ya mahabusu na idadi ya wafungwa ili Taarifa zetu Rasmi za Bunge zikae sawa sawa. Mheshimiwa Masauni.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii. Ni kweli mfupa hauna ulimi. Ulimi hauna mfupa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba *Hansard* iweke sawa kuhusu wafungwa na mahabusu. Kwenye eneo ambalo nilitoa takwimu kuhusu wafungwa na mahabusu, usahihi ni kwamba tunakadiria waliopo Magerezani ni 32,000 ambaao tunakadiria mionganoni mwa hao kumi na nane elfu na laki mbili ndiyo wafungwa...

SPIKA: Kumi na nane elfu na mia mbili.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, samahani. 18,200 ni wafungwa na 13,800 ni mahabusu. Kwa hiyo, naomba *Hansard* irekebishe.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ole-Sendeka.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Spika, nilisimama tu kuomba mwongozo na mwongozo wenyewe ni baada ya maelezo mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba tutakuwa na semina ya kujenga ulewa wa pamoja juu ya suala la Ngorongoro na Wizara imeagizwa.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo kama itawezekana kwa sababu hii ni Wizara ambayo inaweza kuwa inavutana kidogo na wananchi waliopo katika maeneo yale, naomba kama inaruhusiwa kuwakaribisha wawakilishi

wachache kutoka Tarafa ya Ngorongoro na Tarafa ya Loliondo ili kuweza ku-*balance*, kuweka uelewa huo wakati wa kujadili mambo hayo kama haitagongana na taratibu za uendeshaji wa Bunge.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka kuomba mwongozo kuhusu maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni yetu ya 76 inazungumza kuhusu mwongozo na inaeleza masharti ya mwongozo ni yapi? Unaweza kuomba mwongozo kwenye jambo la aina gani? Kanuni zetu zinatuongoza kwamba unapoomba mwongozo, unataka kuuliza, hivi kwamba jambo hili lilitofanyika au kusemwa humu ndani linaruhusiwi au haliruhusiwi?

Sasa Mheshimiwa ni wazo lake, siyo mwongozo. Kwa hiyo, nitoe kabisa kwenye hoja ya mwongozo. Ila yeje ana wazo kwamba yale aliyoyasema Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu semina kwa Wabunge, pengine wangekuja na wawakilishi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu yeje katoa wazo, na kwa sababu ameniomba mimi mwongozo wangu kwenye wazo lake, siyo mwongozo wa kikanuni, huo nimesema haupo; ila anaomba mimi nimwongoze kwenye hilo wazo lake.

Hilo wazo lako kwa sababu semina inahusu kuwajengea Wabunge uwezo, maelezo ya Wizara na utaratibu wao watakaoufanya na Wawakilishi kule, nadhani tuache utaratibu huo uchukue mkondo wake, kwa sababu tukichanganya kila mtu hapa, Waheshimiwa Wabunge amba ni Wawakilishi wa hao wananchi, mpo hapa. Ndiyo maana hasa ya kila mtu kuwa anatoka kila mahali ili wewe ubebe hoja za wananchi wako, maana wewe ndio Mbunge, kwa hiyo, unazifahamu. Nasi Wabunge tutakapokuwa tunajengewa huo uelewa, nawe Mheshimiwa Mbunge una

haki zote za kuwepo pale, kuuliza maswali ili wote tuwe tunaelewa.

Maana kama unavyosema, Serikali inaweza kuwa inavutana, sasa sisi hatujaua bado. Kwa mfano, mimi sijui kama Serikali itavutana hiyo siku ya semina au haitavutana, sijui. Ama itakuja na maelezo ya aina gani, hatujui. Humu ndani msiwe na wasiwasi hasa Mheshimiwa Ole-Sendeka na pengine Wawakilishi wengine mnaotoka maeneo hayo kufikiri pengine Wabunge wote wana mwelekeo sijui wa namna gani, hapana.

Waheshimiwa Wabunge, wanawasikiliza ninyi na wao zinasikilizwa hoja zao. Nami kama Kiongozi wenu wa Bunge msiwe na wasiwasi, mna haki zenu kabisa kama Wabunge, wote mtasikilizwa na wote tunawakilisha wananchi na wote tunataka nchi hii isonge mbele. Ndijo maana hilli ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuna muda tutazungumza mambo ya Majimbo yetu ya watu wetu walitutuma na kuna muda tutazungumza mambo ya Kitaifa kwa sababu yote yanajadiliwa humu ndani. Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi, tulifanye hili la Wabunge kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyotoa maelekezo.

Waheshimiwa Wabunge, mniwie radhi kidogo, leo inabidi njisemee mwenyewe. Kanuni ya 175 imeniwitia ngumu kidogo kuwazuia watu, kwa sababu mimi ndio mhusika na kwa hiyo sikuweza kujipongeza mwenyewe ili sasa nizuie watu wengine kunipongeza kwa sababu ya masharti ya Kanuni ya 175.

Sasa nawaomba kwa sababu kama ninavyosisitiza wakati mwininge Wabunge tupo wengi na muda wetu wa kuchangia ni finyu kidogo. Nadhani wale waliofanikiwa kusema pongezi, wawe wamezisema kwa niaba yetu sote, nami nimezipokea kwa unyonyeketu mkubwa kabisa.

Kwa hiyo, wale wametuwalisha, wengine tutakapokuwa tunauliza maswali, tutakapokuwa tunachangia, basi twende moja kwa moja. Wengine hapa

wamempongeza kabisa atakayekuwa Naibu Spika. Yeye nitamtolea mimi pongezi halafu wote tutakuwa tuko sawa. Ahsanteni sana. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 8.00 mchana.

*(Saa 1:28 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,
Tarehe 10 Februari, 2022 Saa Nane Kamili Mchana)*